# Nipashe

Jumanne Agosti 27, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 05780007

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

## Waziri aonya vipodozi bandia chanzo cha saratani, ukichaa

UKURASA 3


Nipashe TESA

JE, WAJUA?

Jumanne Agosti 27, 2019

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Mradi wapunguza mimba, ndoa za utotoni Shinyanga

Mkenya avunja rekodi ya dunia kwa kupika

SIMANJIRO KATIKA TANZANIA YA VIWANDA

UKURASA 13

# Pingamizi dhidi ya Lissu latupwa

**MAHAKAMA** sasa yasisitiza kuendelea na kesi ya msingi kupinga kuvuliwa ubunge...*Endelea uk. 2*



Wakili Peter Kibatala (kulia), akiwa na mawakili wenzake, Fredy Kalonga (katikati) na Omari Msemwa, katika kesi ya kumtetea mteja wao, Tundu Lissu ya kuvuliwa ubunge wa Singida Mashariki, katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

### MENO YA TEMBO YAMPA MWALIMU WAKATI MGUMU

MWALIMU wa shule ya msingi na wenzake wawili wamekamatwa na polisi wakiwa na vipande sita...

UKURASA WA 8

### VIFO VYA AJALI LORI LA MAFUTA VYAFIKIA 102

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea mkoani Morogoro Agosti...

UKURASA WA 26

### SABABU NDEGE ATCL KUKAMATWA A. KUSINI

SERIKALI imesema ndege yake aina ya Air Bus A220-300 inayoshikiliwa Afrika Kusini ...

# Mtoto anusurika kifo kwa kubwia cocaine

UKURASA 2

## Mtuhumiwa wa ubakaji ashtakiwa uhujumu

UKURASA 3

**MICHEZO** BURUNDI WAMHOFIA NDAYIRAGIJE STARS UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Mahakama yatupa pingamizi dhidi ya Lissu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imetupilia mbali pingamizi la awali la Spika wa Jamhuri ya Muungano, Job Ndugai na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) la kutaka maombi ya kuvuliwa ubunge dhidi ya Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu.

Pia, mahakama hiyo imekubali kusikiliza maombi hayo ikiwamo kupinga kuapishwa kwa mbunge mteule wa jimbo hilo, Miraji Mtaturu, mpaka maombi ya msingi yatakaposikilizwa na kutolewa uamuzi.

Uamuzi huo ulitolewa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Sirilius Matupa.

Jaji alisema mahakama yake ilisikiliza hoja za pingamizi la awali la walalamikiwa hazina mashiko kisheria ameziondoa kwa sababu kiapo kinatakiwa kupingwa na kiapo kinzani.

"Mahakama yangu imetupilia mbali pingamizi la awali la walalamikiwa na kwamba maombi ya Lissu yatasikilizwa pamoja na zuio la kupinga mbunge mteule kuapishwa,"alisema Jaji Matupa.



Akisoma uamuzi wake alisema mlalamikaji kupitia wakili Peter Kibatala, alidai kuwa mlalamikiwa wa kwanza Spika Ndugai ameshindwa kumwalifu Lissu sababu zilizomwondolea sifa ya kuwa mbunge ili ajitetee.

Hoja nyingine ya kujibu pingamizi hilo kwamba Lissu amehukumiwa kwa kuvuliwa nafasi hiyo bila kujua kosa lake.

Vile vile, Spika Ndugai amefanya maamuzi ya kumvua ubunge Lissu bila kupata ukweli kwa sababu alijua kwamba alijeruhiwa kwa kupigwa risasi mapema mwaka 2017 na kupelekwa jijini Nairobi, nchini Kenya na baadaye nchini Ubelgiji anakoendelea na matibabu.

Jaji aliendelea kusoma hoja za mlalamikaji za pingamizi la awali kwamba, Lissu katika kipindi chote cha utumishi wake kama mbunge amefanyakazi kwa audilifu na kujipatia heshima kubwa.

Hata hivyo, Kibatala katika hoja zake alidai kuwa Spika Ndugai alikula njama ya kumtoa Lissu na kumvua ubunge huo na kwamba alimnyima haki yake ya kupata matibabu.

Akizungumzia hoja za pingamizi la awali lililowasilishwa na jopo la Mawakili wa Serikali 14 wa walalamikaji wakiongozwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dk .Clement Mashamba, jaji alisema kwa nyakati tofauti limeomba maombi hayo yatupiliwe mbali na mlalamikaji alipe gharama ya kesi dhidi ya walalamikiwa.

Alisema walalamikiwa wamewasilisha pingamizi lenye sababu nane kupinga maombi yaliyowasilishwa na Lissu kupitia mawakili wake Peter Kibatala, John Mallya na Jeremiah Mtobesya.

Alisema Wakili wa Serikali Mkuu, Abubakar Mrisha, alidai maombi yaliyowasilishwa mahakamani hayana nguvu za kisheria kwa sababu maombi au mashauri yanapofikishwa mahakamani lazima yawe yamezingatia vigezo sita.

Jaji Matupa aliendelea kuchambua uamuzi huo kuwa Mrisha alidai kwamba kigezo cha kwanza kama maombi yaliletwa ndani ya miezi sita baada ya jambo husika kutolewa uamuzi, pili mwombaji awe anaelewa vizuri shauri, maamuzi yawepo kisheria, iwe hakuna namna nyingine ya kufanya kuhusu huo uamuzi, kama mahakama itasikiliza na kuona kuna haja ya kutoa uamuzi na sita maombi yanatakiwa yawe katika nia njema na wala si kwa kupotosha au kuwa na lengo la kujinufaisha binafsi.

Alisema hoja nyingine ilitolewa na Wakili wa Serikali Mkuu, Lucas Malunde, kwamba si Spika anayetoa tamko, Spika anatoa taarifa na hajishughulishi na kitu kingine chochote, katika kesi hiyo mwombaji hakuwepo katika kiti chake cha ubunge.

Wakili Marunde alidai hakuna maamuzi yoyote kutoka kwa Spika hivyo wanaomba maombi yatupwe kwa gharama.

Hoja zingine ziliwasilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, George Mundepo, anadai kwamba mleta maombi Alute Mughwai, hana sifa ya kufungua maombi hayo kwa niaba ya Lissu.

Alidai sheria inaruhusu madai kufunguliwa na mhusika au anayemwakilisha mwenye mamlaka kisheria, lakini shauri lililopo limewasilishwa na Lissu kupitia mwakilishi wake Alute Mughwai.

Kutokana na hoja hizo aliomba mahakama iyatupe maombi hayo kwa kuwa pamoja na mambo mengine aliyeyaleta hana sifa ya kufanya hivyo.

Jaji Matupa juzi alitakiwa kusikiliza maombi ya zuio la muda la kuapishwa kwa Mbunge mteule, Jimbo la Singida Mashariki, Miraji Mtaturu na maombi ya kupinga kuvuliwa ubunge aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Lissu, lakini haikuwezekana baada ya Jamhuri kuwasilisha pingamizi la awali.

Maombi ya kupinga kuvuliwa ubunge yalifunguliwa na aliyekuwa Mbunge wa zamani wa jimbo la Singida Mashariki, Lissu kupitia mawakili wake.

Alifungua shauri hilo chini ya hati ya dharura, kupitia kwa kaka yake Wakili Alute Mughwai, ambaye amempa mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Maombi hayo dhidi ya Spika wa Bunge la Tanzania na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akiomba kibali cha kufungua shauri la kupinga uamuzi huo.

Kwa mujibu wa ombi namba 18 la mwaka 2019, Lissu anaiomba mahakama hiyo, impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika Ndugai ampe (Lissu) taarifa yake ya kumvua ubunge.

Anaomba mahakama hiyo itengue na kutupilia mbali uamuzi huo wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

Pia anaiomba mahakama itoe amri ya kusimamisha kuapishwa kwa mbunge mteule wa jimbo hilo, Miraji Mtaturu wa Chama cha Mapinduzi.

Katika hati ya dharura Lissu anaiomba mahakama hiyo isikilize na kutoa uamuzi wa maombi yake haraka vinginevyo, Mtaturu ambaye Julai 19, mwaka huu alitangazwa na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo ataapishwa kushika wadhifa huo.

Hivyo, anadai atakuwa ameathirika kwa kuwa atapoteza haki zake zote, kinga na maslahi yake yote yanayoambatana na wadhifa wake huo wa ubunge.

Uamuzi wa kuvuliwa ubunge ulitangazwa na Spika wa Bunge, Ndugai, Juni 28, 2019, wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge.

Spika Ndugai alizitaja sababu mbili za kuvuliwa ubunge Lissu kuwa ni kushindwa kuhudhuria vikao vvya bunge kwa muda mrefu bila kumjulisha Spika kwa maandishi mahali aliko na sababu ya pili ikiwa ni kutokutaja taarifa za mali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Hata hivyo, Spika Ndugai alijitetea kuwa si yeye aliyemvua ubunge bali ni Katiba ya nchi.

TAARIFA KWA UMMA



SADA SIRATHO ALI

Mtajwa hapo juu sio mfanyakazi wa **Access Medical and Dialysis Centre** tangu tarehe **24/06/2019** hivyo kampuni haitajihusisha na chochote atakachokifanya kuanzia tarehe tajwa hapo juu.

215388802

# Mtoto anusurika kifo kwa kubwia cocaine

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MTOTO mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi sita amenusurika kifo baada ya kudaiwa kubwia dawa za kulevya aina ya cocain.

Mtoto huyo (jina linahifadhiwa), alifikishwa Hospitali ya Mnazi Mmoja Agosti 18, mwaka huu, kwa ajili ya matibabu.

Akizungumza na Nipashe, Katibu wa hospitali hiyo, Hassan Makame, alisema mtoto huyo alifikishwa hospitalini hapo majira ya saa mbili usiku Agosti 18, mwaka huu na daktari aliyempatia matibabu aligundua kuwa alikula unga aina ya cocain.

Alisema maelezo ya daktari yanasema mtoto alipofikishwa hospitalini alikua analia sana hivyo alichomwa sindano ya usingizi na kuwekewa maji ya dripu.

Alisema mama mzazi wa mtoto alieleza kuwa mtoto wake aliokota dawa hizo za kulevya majira ya asubuhi siku hiyo ya Agosti 18.

Alisema baada ya kula unga huo walimpa maziwa na kuanza kutapika, lakini baadaye hali yake ilibadilika na kumpeleka hospitali moja binafsi na kupatiwa huduma.

Baada ya kurejea nyumbani, alisema hali yake haikuwa nzuri na ndipo majira ya saa mbili usiku alilazimika kumpeleka Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Thobias Sedeyoka, alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kubaini mazingira ya mtoto jinsi alivyoupata unga huo.

Alieleza kuwa mama wa mtoto huyo yupo chini ya uangalizi wa jeshi hilo kwa ajili ya upelelezi.

Kwa upande wake mtaalamu wa saikolojia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hamida Naufil Kasim, alisema kuwa endapo mtoto huyo atapata harufu ya dawa za kulevya anaweza kuathirika kisaikolojia.

Alieleza kuwa mtoto huyo anahitaji uangalizi mzuri ili kumnusuru afya na uhai wake.

"Kama wazazi wanatumia dawa za kulevya ni vyema wakaacha mara moja ili kumlinda na watoto wengine ambao wanaishi katika maeneo hayo," alisema.

HABARI KITAIFA

# Waziri: Vipodozi chanzo saratani, kuchanganyikiwa

**Mariam Magili na Jovin Lamwel**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameitaka jamii kutumia vipodozi vya asili ili kuepukana na madhara yanayosababishwa na matumizi ya vipodozi vyenye kemikali.

Katika uzinduzi wa Chama cha Waandaji na Wazalishaji wa Vipodozi nchini uliofanyika jana jijini Dar es Salaam, Mwalimu alisema vipodozi vyenye kemikali vimekuwa na madhara makubwa kwa afya ya binadamu.

Aliitaka jamii kuachana na matumizi ya vipodozi vyenye kemikali ambavyo havijaidhinishwa na Shirika la Viwango (TBS) kwa kuwa ni chanzo cha magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.

Alibainisha kuwa utafiti uliofanyika mwaka 2005 chini ya Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), ulionyesha wagonjwa 2,416 walipata kutokana na kutumia vipodozi vyenye kemikali na kwa sasa idadi imefika wagonjwa 7,649.

Waziri huyo aliwapongeza wajasiriamali walioamua kuunda chama hicho ambacho kitatambulisha vipodozi asilia vinavyotengenezwa nchini.

Mwalimu pia alisema iko haja serikali kupitia Wizara ya Afya kurasimisha mitaala inayohusiana na masuala ya vipodozi ili kuwapa nafasi watu wanaotengeneza vipodozi asilia kupata masoko ndani na nje ya nchi.

Aliwataka wanachama wa chama hicho kutoa ushirikiano kwa kuzipa taarifa mamlaka za serikali pale wanapobaini mtu yeyote anayeuza au kutengeneza vipodozi feki.

Mwakilishi wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Sabanitho Mtega, alisema: "Ipo haja ya kufanya uchunguzi mbalimbali juu ya bidhaa zinazotumika na kusimamia matumizi sahihi ya vipodozi."

Alisema mbali na kuunguza ngozi na kunyonyosha nywele, matumizi ya vipodozi vyenye kemikali pia husababisha matatizo ya akili na kuathiri mfumo wa uzazi.



Wachuuzi wa bidhaa mbalimbali wakifanya shughuli zao chini ya transfoma ya umeme mkubwa kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, jambo ambalo ni hatari endapo itatokea hitilafu ya umeme. **PICHA: JOHN BADI**

# Mtuhumiwa wa ubakaji wake za watu afunguliwa kesi ya uhujumu uchumi

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI wa Mashtaka nchini (DPP), Biswalo Mganga, amesema Ahmed Mohamed anayetuhumiwa kubaka wake za watu, wamemfungulia mashtaka yakiwamo ya uhujumu uchumi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Mganga pia amewataka watu wote waliofanyiwa vitendo vya udhalilishaji ikiwamo kubakwa au kuingiliwa kinyume cha maumbile, kujitokeza na kutoa taarifa kwa kuwa kesi hizo zitaendeshwa kwa usiri wa hali ya juu na majina yao hayatatajwa.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu Mohamed ambaye anadaiwa kutumia majina tofauti kufanya vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake.

Mganga alidai Mohamed amekuwa akienda hoteli mbalimbali na kuweka dawa kwenye vinywaji vya wanawake kisha kuwabaka, kuwaingilia kinyume cha maumbile na kuwaibia.

Alidai awali mtuhumiwa huyo alifunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni na kupatiwa dhamana.

"Baada ya kutoka, aliendelea na vitendo vyake hivyo vya uzalilishaji kwa wanawake, na wengine ni wake za watu," Mganga alidai.

Aliongeza kuwa tayari wameshafuta kesi iliyokuwa katika Mahakama ya Kinondoni na walimfungulia kesi nyingine Agosti 21, mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na mashtaka mbalimbali likiwamo la uhujumu uchumi.

Mganga alisema hakuna haki isiyo na mipaka na ni lazima kuangalia madhara yaliyojitokeza kwa watu kwa kuwa wapo wengi kutoka Dar es Salaam waliofanyiwa vitendo hivyo wakiwamo wake za watu.

Aliwaomba watu waliofanywa vitendo hivyo kujitokeza kutoa ushahidi kwa kuwa kesi hizo zitaendeshwa kwa siri na tayari mahakama imekubali kuendesha kesi hizo kwa msingi huo wa usiri na kutotaja majina ya mashahidi.

Mganga pia aliwataka watu kufuata sheria ikiwa ni pamoja na kusajili televisheni za mitandao, akieleza kuwa kasi ndogo ya serikali kuzisajili, siyo mwanya wa watu kuvunja sheria.

"Mwanafunzi wa mwaka wa pili katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Julius Warioba (23), amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni tano au kwenda jela mwaka mmoja, baada ya kukiri kuchapisha maudhi katika mtandao bila kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA).

"Warioba ambaye ni mshereheshaji (MC), amehukumiwa kifungo hicho leo (jana) Agosti 26, 2019 na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Kisutu, Janeth Mtega, baada ya kumtia hatiani kwa makosa ya aina hiyo," alisema.

**United Nations Development Programme**

Empowered lives. Resilient nations.

**ADVERTISEMENT**

**CALL FOR PROPOSALS FOR PROVISION OF LEGAL AID IN ZANZIBAR**

UNDP in collaboration with the Ministry of Constitution and Legal Affairs (MoCLA) - Zanzibar is soliciting proposals from Legal Aid providers with proven experience and track record in providing legal assistance in Zanzibar.

Interested and competent Legal Aid providers with proven experience and track record in providing legal assistance and support are therefore invited to submit Technical and Financial proposals on or before Monday, 23 September 2019 at 14.00 hours (EAT) to:

**United Nations Development Programme (UNDP)**
**UN Compound**
**182 Mzinga Way, Osterbay**
**P.O. Box 9182**
**Dar Es Salaam, Tanzania**

**Attn: UNDP Registry**

The Terms for Reference (ToR) may be downloaded from the following link:
**http://procurement-notices.undp.org/view_notice.cfm?notice_id=58605**

Requests for clarification should be sought in writing from the following e-mail address:
**paul.turay@undp.org** or **fridah.mwakasyuka@undp.org**

Proposals in one original plus four copies, duly completed and marked **"Call for Proposal for provision of Aid in the Criminal Justice Sector, DO NOT OPEN BEFORE MONDAY, 23 September 2019 at 14.00 hours (EAT)"** must be submitted before closing time.

All proposals must be delivered by hand/courier services and reach UNDP Tanzania before the deadline as indicated above.

**Late proposals will not be accepted.**

215388702

Plot No.182, Mzinga Way, Oysterbay. P. O. Box 9182, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255-22-2112576 Fax: +255-22-21111668 Website: http://www.tz.undp.org/ Email: registry.tz@undp.org

TOLEO MAALUMU

# JAPAN INAJIANDAA KWA AJILI YA MKUTANO MUHIMU WA KIMATAIFA KWA MAENDELEO YA AFRIKA (TICAD)

Mkutano wa Kimataifa wa Tokyo wa Maendeleo ya Afrika (TICAD) ni mkutano wa kimataifa unaoongozwa na Serikali ya Japan na kushirikiana katika udhamini na Umoja wa Mataifa, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Tume ya Umoja wa Afrika (AUC) na Benki ya Dunia.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, azma ya nchi zilizoendelea kuzisaidia nchi nyingi za Kiafrika ilianza kufifia. Katika mazingira hayo, Japan ndiyo ilikuwa nchi mwasisi wa wazo la kuona umuhimu wa kuisaidia Afrika, na kuanzia hapo mkutano wa TICAD ulikuwa ni sehemu ya mchango wa Japan kutekeleza kwa vitendo azma hiyo.

Mkutano wa kwanza wa TICAD ulifanyika mnamo mwaka 1993 ukiongozwa na Japan ikishirikiana kwa karibu na Umoja wa Mataifa na taasisi ya Global Coalition for Africa, na kuwavutia washiriki kutoka nchi 48 za Kiafrika, ikijumuisha wakuu wa nchi wapatao watano (5).

Azimio la Tokyo la Maendeleo ya Afrika ambalo lilipitishwa na mkutano huo wa kwanza , lilirudisha suala la misaada na maendeleo kwa ajili ya Afrika kuwa ajenda ya kimataifa. Tangu hapo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 20,TICAD imekua na historia ya kuboresha mazingira ya kijamii na kiuchumi ndani ya Afrika kwa kutumia rasilimali za umma na binafsi ikijumuisha misaada ya kiufundi kutoka Japan, utaoji wa misaada, na mikopo ya kawaida.

Kuanzia mwaka 2016 na kuendelea, mikutano ya TICAD hua inafanyika kila baada ya miaka mitatu (3) barani Afrika na Japan. Mkutano wa TICAD wa sita (6) ulifanyika Kenya na mkutano ujao wa TICAD wa saba (7) utafanyika Yokohama kuanzia Agosti 28 mpaka Agosti 30, 2019.

Kauli mbiu ya mkutano ujao wa TICAD wa saba (7) ni **"Kuendeleza Maendeleo ya Afrika kupitia Watu, Teknolojia na Ubunifu"**Kauli mbiu hiyo inaendana na umahiri wa Japan katika uendelezaji wa rasilimali watu sambamba na sayansi, teknolojia na uvumbuzi. Katika kauli mbiu hii, Japan inalenga kuboresha maendeleo ya Afrika kupitia misaada mbalimbali ambayo ni ya kipekee kwa Japan. Kupitia kauli mbiu hii ya mkutano wa saba wa TICAD Japan inatarajia thamani ya bara la Afrika itaongezeka katika ngazi zote za kitaifa na kimataifa.

## TICAD na JICA

Mkutano wa TICAD kufanyika Afrika kwa mara ya kwanza ulikuwa ni ule uliofanyika jijini Nairobi, Kenya mwezi Agosti 2016. Azimio la Nairobi liliubeba mkutano huo wa sita (6) wa kihistoria wa TICAD uliosisitiza mabadiliko ya muundo wa kiuchumi kupitia uchumi mseto, viwanda, mifumo ya afya endelevu kwa ubora wa maisha na utulivu wa jamii kwa ustawi wa pamoja ndio masuala makuu ya kushughulikia changamoto mpya ambazo Afrika imekuwa ikikabiliana nazo. Kwa changamoto hizo, Serikali ya Japan ilijitolea katika mkutano wa sita (6) wa TICAD kuwekeza kwa mustakabali wa Afrika kwa kuunga mkono ujenzi wa miundombinu bora, kujenga mfumo wa afya thabiti, na kuchagiza amani na utulivu kuanzia mwaka 2016.


Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) ambalo ni Shirika la Serikali ya Japan linalosimamia Misaada ya Maendeleo (ODA), inayotolewa na Serikali hiyo, limekuwa likichukua hatua kadhaa na kuonyesha matokeo madhubuti kwa mustakabali wa Afrika, kwa lengo la kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). JICA imekuwa ikichukua hatua hizo kupitia njia tatu ambazo ni: ushirikiano wa kiufundi, utoaji wa mikopo ya masharti nafuu (ODA concessionary loans), na utoaji wa misaada isiyokua na sharti la kulipa (grant-aid) kwa nchi za Kiafrika sanjari na dira yake ya **"Kuongoza dunia kwa uaminifu".**

Pamoja na malengo ya TICAD, mipango ya JICA barani Afrika imejengwa kupitia nguzo tatu kama ifuatavyo: Afrika Bora, Afrika yenye Utulivu na Afrika Thabiti.

## Afrika bora

Kutokana na kuporomoka kwa bei ya bidhaa za ulimwengu baada ya 2013, JICA inawezesha mabadiliko ya muundo wa uchumi kupitia ujumuishaji wa uchumi na masuala ya viwanda barani Afrika. Kutekeleza hilo JICA inakuza maendeleo ya miundombinu bora kwa kuwekeza takriban dola bilioni 10 katika maendeleo ya rasilimali asili na maendeleo ya nishati, na maendeleo ya miji.

JICA pia inakuza shughuli za sekta binafsi kupitia ukuzaji rasilimali watu na stadi za kiutendaji kwa viwanda vya Kiafrika ambavyo pia vinakidhi mahitaji ya kampuni za Japan. Hii ni pamoja na programu za mafunzo ya waalimu wa hesabu na sayansi, msaada wa mafunzo ya ufundi na elimu ya juu, na juhudi za KAIZEN katika viwanda vya utengenezaji/uzalishaji wa bidhaa na sekta ya biashara. Kwa kuongezea, JICA inatoa fursa kwa vijana wa Kiafrika kusoma katika kozi za shahada ya uzamili huko Japan na kupata mafunzo tarajali ya uzoefu katika kampuni za Kijapani kupitia mpango wa ABE Initiative (African Business Education). JICA pia inafuatilia vijana hawa baada ya kurudi katika nchi zao, kwa lengo la kukuza rasilimali watu ambao wanaweza kuwezesha Makampuni ya Japan kupanua biashara zao katika bara la Afrika.




## Afrika yenye utulivu

JICA inatilia mkazo katika kujenga mfumo wa afya bora kwa maisha bora.Wakati ikizingatia haki ya kila nchi kumiliki shughuli zake, JICA inasaidia Mpango wa Afya kwa Wote (UHC) kupitia ushirikiano wa kifedha na kiufundi kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa huduma ya afya na kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na fedha za afya. JICA pia inasaidia afya ya mama na mtoto, afya ya uzazi, na hatua za magonjwa ya kuambukiza na yasiyoweza kuambukiza kufikia Mpango wa Afya kwa Wote (UHC).

## Afrika thabiti

JICA inasaidia katika kujenga msingi madhubuti wa utulivu wa kijamii katika kukabiliana na ukuaji wa vurugu zinazotokana na siasa za misimamo mikali, vita na mabadiliko ya hali ya hewa. Katika suala hili, JICA inakusudia kuongeza uzalishaji wa mpunga maradufu katika miaka 10 kupitia Mipango ya Maendeleo ya Mpunga ya Kitaifa ya kila nchi chini ya mpango wa Jumuiya ya Maendeleo ya Mpunga Afrika (CARD) ambayo ilianzishwa mnamo 2008. Aidha JICA inasaidia mnyororo mzima wa thamani kama upanuzi, uzalishaji, utunzaji baada ya mavuno na utafutaji masoko kupitia ushirikiano wa kiufundi na kifedha na shughuli za utafiti kwa kushirikiana na washirika wengine wa maendeleo.

## JICA nchini Tanzania

Ili kufikia malengo ya TICAD, JICA Tanzania inafanya shughuli katika sekta mbalimbali nchini ambazo ni Kilimo, Sekta Binafsi na Maendeleo ya Viwanda, Umeme na Nishati, Uchukuzi, Maji, Serikali za Mitaa, Usimamizi wa Fedha za Umma na Afya. Kwa kuongezea, JICA imekuwa ikipeleka watu wa kujitolea zaidi ya 1,500 nchini Tanzania tangu 1967. Zaidi ya hayo, JICA ina program ya mafunzo ambayo zaidi ya Watanzania 3,500 wametembelea Japan na takriban watu 100 kila mwaka wanashiriki katika programu hiyo. Kwa sababu ya nafasi, katika makala haya tunataja shughuli chache tu ambazo husaidia maendeleo ya nchi: miongoni mwa mambo hayo, ni maendeleo ya uchukuzi wa mijini, uwezo wa uwezeshaji wa biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki, uboreshaji wa ubora na tija katika viwanda vya uzalishaji "5S KAIZEN", na mafunzo ya shahada ya uzamili katika mpango wa African Business Education (ABE Initiative), na Kilimo.

## Maendeleo ya usafirishaji mijini



DARAJA LA JUU MFUGALE, DAR ES SALAAM

Maendeleo ya usafirishaji wa mijini ni muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote. Tanzania imebarikiwa kuwa na Bahari ya Hindi huku ikiwa na nchi tano za jirani zisizokuwa na bahari. Kwa maana hii, ina faida ya kijiografia kama kitovu cha usafirishaji wa kikanda. Ukizingatia ukuaji endelevu wa uchumi ulioshuhudiwa katika miaka ya hivi karibuni na kuongezeka kwa kasi kwa shehena, changamoto ya msingi ni kusaidia kukuza mitandao ya barabara, reli na bandari kwa kanda kwa kutumia fursa ya jiografia ya Tanzania kikamilifu.

Misaada wa JICA katika sekta hii ilianza mnamo mwaka 1980 kwa ujenzi wa Daraja la Selander, ikifuatiwa na ukarabati wa barabara nyingi katika eneo la Kariakoo la Dar es Salaam na katika Wilaya ya Kati ya jiji hilo la kibiashara katika miaka ya 1990. Katika siku za hivi karibuni, barabara kama vile Kilwa, Ali Hassan na Kawawa za jijini Dar es Salaam zilijengwa kwa msaada wa JICA. Hivi majuzi, JICA ilichangia katika ujenzi wa Daraja

# TOLEO MAALUMU

la Juu la kwanza nchini Tanzania (Mfugale Flyover) kwenye makutano ya Tazara ambalo lilikamilika mnamo Septemba 2018. Kufuatia kukamilika kwa Daraja hilo la Juu, msongamano katika Makutano hayo (ambayo ni moja ya maeneo yenye shughuli nyingi zaidi nchini) umepunguzwa sana.

Muda wa kusafiri katika sehemu hii umepunguzwa sana; ni ahueni kwa wasafiri waliokuwa wakipata kizuizi/ugumu kwenda na kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA). Kwa kuongezea, eneo la ujenzi lilisimamiwa vizuri na mkandarasi na mshauri wa Kijapani. Mradi huo haukufanikiwa tu kuweka rekodi ya zaidi ya masaa milioni 2.5 bila ajali yeyote lakini pia ulikamilishwa kama ilivyopangwa. Daraja hilo la juu (Flyover) ni ishara ya kudumu ya kumbukumbu ya ushirikiano na urafiki wa muda mrefu kati ya Tanzania na Japan. Miradi ya maendeleo ya mijini ambayo ipo katika hatua za utekelezaji ni pamoja na Mradi wa Upanuaji wa Barabara mpya ya Bagamoyo (Mwenge – Morocco) na ujenzi wa mradi wa daraja la Gerezani jijini Dar es Salaam.

### Ukuzaji uwezo wa uwezeshaji wa biashara katika Ukanda wa Afrika Mashariki

JICA Tanzania kwa kushirikiana na mamlaka za mapato tano (5) za nchi za Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda wamekuwa wakitumia mradi wa ushirikiano wa kiufundi unaojulikana kama "Mradi wa Kukuza Uwezo wa Uwezeshaji Biashara katika Afrika Mashariki" tangu 2017. Kusudi la mradi huu ni kuhakikisha utendaji kazi mzuri wa Kituo cha Huduma za Pamoja Mpakani "One-Stop- Border Post" (OSBPs) kwenye mipaka lengwa na kuboresha ujengaji uwezo wa shughuli za forodha katika udhibiti wa majanga /hatari na mipaka ndani ya Afrika Mashariki. Ili kuongeza uwezeshaji wa kibiashara ndani ya Ukanda wa Afrika Mashariki na zaidi, JICA ilichangia katika uanzishwaji wa OSBPs huko Rusumo kwenye mpaka wa Tanzania / Rwanda na Namanga kwenye mpaka wa Tanzania / Kenya. Kupitia vituo hivi vya OSBPs, muda wa uondoshaji mizigo katika mipaka hiyo umepungua sana. Kwa mfano huko Rusumo, muda wa uondoshaji wa mizigo umepunguzwa kwa takriban asilimia 73.

### Mradi wa uboreshaji tija viwandani (KAIZEN)

Uboreshaji wa tija katika sekta ya uzalishaji ni moja ya shughuli kuu za JICA nchini Tanzania. Kutokana na ombi la Serikali, JICA ilianzisha Mradi wa Kuongeza Ubora na Uzalishaji Viwandani (KAIZEN) mnamo 2003. Hapo awali mradi huu ulishughulikia Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro. Kupitia mradi huu, kampuni zaidi ya 50 na zaidi ya watu 2000 walifundishwa kuhusu mkakati huo wa KAIZEN. Jambo hilo lilisababisha kuongezeka kwa tija sambamba na kuongezeka maradufu kwa uzalishaji na kampuni nyingine kumudu kupunguza kiwango cha uharibifu wa bidhaa (defective rate) kwa asilimia 70. Awamu ya 2 ya mradi huo itahusu Mikoa mingi zaidi na kampuni nyingi zaidi. Lengo la mwisho la mradi huu ni kusambaza mbinu za mradi wa KAIZEN kwa kampuni 100 na kuzalisha wakufunzi 150 wa KAIZEN kote nchini. Wakati huo huo Kiwanda cha kutengeneza nguo kilichopo mkoani Arusha cha A to Z kiliibuka mshindi wa shindano la tuzo za KAIZEN za bara la Afrika. Kampuni hiyo iliyoko Arusha, ambayo inatumia mbinu ya KAIZEN katika shughuli zake, ilipewa tuzo hiyo katika shindano ambalo lilifanyika Tunis, Tunisia mnamo Juni 2019. Nchi nyingine ambazo zilishiriki katika mashindano hayo zilikuwa Tunisia, Kenya, Afrika Kusini, Ethiopia, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Namibia.

*Angalizo: "KAIZEN" ni neno la Kijapani linalomaanisha "uboreshaji". Ni moja ya falsafa za kijapani ambazo hukakikisha uzalishaji ulio bora na wa gharama nafuu.*

### Programu ya Shahada ya Uzamili ya Mpango wa Elimu kwa Afrika (ABE Initiative)

Mpango wa ABE Initiative ulianza mnamo 2014 kwa lengo la kuziba pengo/nafasi iliyopo baina ya Japan na Tanzania kupitia kuwajengea uwezo vijana wa Kiafrika. Kufikia sasa vijana 85 wa Kitanzania wamefaidika na programu za shahada za uzamili zinazotolewa katika Vyuo Vikuu vya Kijapani na mafunzo tarajali kutoka katika kampuni za kati za biashara za Kijapani huko Japan kupitia mpango huu. Wahitimu wa ABE wanatarajiwa kuchangia katika maendeleo ya viwanda nchini na kujenga mitandao na sekta binafsi ya Japan.

### Kilimo

Katika kilimo, msaada wa JICA Tanzania ulianza mnamo 1974 na "Mradi wa Maendeleo ya Kilimo Kilimanjaro". Hii ilifuatiwa na Mradi wa Umwagiliaji wa Moshi Chini (Lower Moshi Irrigation Scheme) na Kituo cha Maendeleo ya Kilimanjaro na kwa sasa Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Kilimanjaro (KATC). Tangu wakati huo, JICA imekuwa ikisaidia kilimo cha mpunga kupitia Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Mpunga (TANRICE 2) ambao sasa unahusisha Tanzania nzima.

Kupitia mradi huu zaidi ya wakulima 15,000 wamepatiwa mafunzo na kuanza kutumia teknolojia bora za kilimo cha mpunga. Zaidi ya hayo, wakulima ambao walishiriki katika mafunzo kama haya wameongeza mavuno yao ya mpunga kwa takriban asilimia 40. Katika miaka ya 2000, JICA ilipanua shughuli zake katika sekta ya kilimo kwa kuimarisha mfumo wa ukaguzi na utathmini wa Serikali (M&E). Hii ilisababisha maendeleo ya mfumo wa taarifa wa wavuti unaoitwa "Mfumo wa Takwimu za Kilimo (ARDS)". Mnamo mwaka 2017 zaidi ya 90% ya taarifa za kilimo kote nchini zilisomwa na mfumo huo kila mwezi.

Mapema mwaka huu Mradi wa Uimarishaji wa Mipango na Uwezo wa Utekelezaji wa DADP kupitia Matumizi ya Njia ya SHEP (TANSHEP) ulianzishwa. Hii inakusudia kukuza sekta ndogo ya kilimo cha mbogamboga inayolenga Mamlaka ya Serikali za Mitaa 12 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga na katika maeneo mengine ya kipaumbele cha kilimo hicho kulingana na vipaumbele vya Serikali. Madhumuni ya mradi huu ni kuwezesha Wilaya katika maeneo yaliyolengwa kuongeza kipato cha wakulima katika maeneo hayo kupitia njia ya "Kulima kwa ajili ya kuuza" na sio njia ya "Kulima na kuuza".



MRADI WA UMWAGILIAJI MOSHI

### Ofisi ya JICA, Tanzania

Shughuli za Ofisi ya JICA Tanzania zilianza mnamo 1962, mwaka mmoja tu baada ya uhuru wa Tanganyika, wakati ambao ni Mtanzania mmoja tu alikubaliwa kujiunga na mafunzo ya ufundi huko Japan. Tangu wakati huo shughuli kama hizo ziliendelea kukua na kupanuka kwa miaka mingi na sasa hazijumuishi tu ushirikiano wa kiufundi lakini pia utoaji wa mikopo ya masharti nafuu na misaada isiyokuwa na masharti ya kulipa (grant-aid).

Ili kufanya shughuli kama hizi, Ofisi ya JICA Tanzania imeajiri zaidi ya wafanyikazi 50 (wanaume kwa wanawake) ambao wanafanya kazi ili kuhakikisha kuwa shughuli za JICA nchini zinafanywa kwa ustadi kwa faida ya watu wa nchi zetu mbili za kirafiki za Tanzania na Japan.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 'Waacheni wakimbizi warudi nyumbani'

**KILA** la kheri Tanzania na Burundi kwa kuafikiana kurejesha wakimbizi 2,000 kila wiki nchini kwao kuanzia Oktoba mwaka huu, jambo ambalo litawarudisha nyumbani maelfu ya wakimbizi ambao pamoja na kutengwa na familia zao wanapata wasaa mwingine wa kuungana na kujenga taifa lao.

Hatua ya kuwarejesha nyumbani wakimbizi hao inakuja baada ya kujiridhisha kuwa kuna amani na utulivu nchini Burundi na raia wanastahili kurejea makwao hatua inayotangazwa na Waziri wa Mambo ya Ndani Kangi Lugola kwa upande wa Tanzania na Paschal Barandagiye wa Burundi.

Tangazo hilo kama lilivyoelezwa linawahusu wakimbizi waliokuwa wanaishi kwenye makambi ya Nduta na Mtendeli mkoani Kigoma.

Ni jambo la mafanikio katika kulinda maisha na uhuru wa asili wa raia wa Burundi ambao walizaliwa huru na wanatakiwa kupata haki hiyo hadi mwisho wa maisha na si kuishi ugenini.

Kuwa mkimbizi ni jambo lisilotabirika na pengine hata kukwepeka kutokana na mivutano ya kisiasa iliyoko duniani leo.

Hata hivyo, jumuiya za ushirikiano za kanda mbalimbali Afrika kama Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ile ya Maendeleo ya Uchumi ya Kusini mwa Afrika (SADC) moja ya majukumu yake ni kuwa na sera na taratibu zinazolinda amani na utulivu miongoni mwa mataifa wanachama ili kuepusha vita na wakimbizi.

Vurumai za kisiasa ni mambo yanayowanyima raia uhuru wa asili wa kuishi katika mataifa waliyozaliwa na kuendesha maisha yao.

Hivyo ni vyema Burundi ikapigania uwapo wa haki na usawa ili kuondoa vita katika nchi yake na kuwapa raia wake haki ya kuwa huru ndani ya ardhi yao.

Burundi imejinasibu kuwa iko salama na raia wake walioko Tanzania wanaweza kurudi nyumbani, lakini yakatolewa maelezo na wakimbizi hao kuwa wanatishiwa na mashiriki ya kuhudumia wakimbizi kuwa Burundi hakuna amani ili wafanyakazi hao waendelee kuishi na wakimbizi hao makambini.

Licha ya kwamba Waziri Lugola ameagiza ufanywe uchunguzi ili kuwafahamu wanaowaongopea wakimbizi ukweli ni kwamba, Waswahili wanasema hakuna lisilo na mwisho au marefu yasiyo na ncha.

Wakimbizi hawawezi kuishi kambini muda wote au maisha yao yote, kisa kuna maofisa wanaowatishia kuwa nyumbani kwao hakuna amani. Hata hao maofisa nao watafakari mienendo yao kwa kuwa ukimbizi ni kama 'utumwa'.

Ukimbizi una athari kisaikolojia, kiuchumi, kihisia na wakati mwingine ni kama kukwama kimaisha kutokana na changamoto kama hizo za ukosefu wa amani nyumbani.

Wakimbizi wengi wanakumbuka nyumbani pamoja na wale waliobaki huko nyumbani hawa ni wana familia kuanzia wazazi, dada na kaka, wenza na watoto. Lakini pia kuna kile walichokiacha iwe mali, malengo na hata kazi zilizofanyika zikiwamo hati za ardhi, vyeti vya kitaaluma na mambo mengi ambayo kabla ya kuwa mkimbizi mtu aliyafanya.

Chondechonde waacheni wakimbizi warudi nyumbani, msiwarubuni kwa lolote wapeni nafasi ya kuungana tena na familia zao, kuziona tena kazi walizozifanya na kutimiza ndoto zao kabla hawajawa katika hali ya kukimbia nchi zao.

Itoshe tu kusema kuwa wakimbizi nao ni watu waliozaliwa huru wanaohitaji kuwa huru na kufurahia maisha yao. Waacheni warudi Burundi msiwazuilie kwa lolote kwa kuwa uraia wao ni haki yao ya kuzaliwa, lakini ardhi yao ni zawadi waliyopewa na Mungu alipoumba ulimwengu na kutawanya mataifa.

Kila la heri wakimbizi wanaorudi nyumbani tunawatakia mafanikio na fanaka zote kila wanapoanza tena maisha yao ndani ya ardhi waliyopewa wakati wa kuumbwa ulimwengu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanufaika mikopo elimu ya juu walipe walichokopeshwa

Na Raphael Kibiriti

**GAZETI** hili limekuwa na habari kubwa katika ukurasa wake wa mbele kwa nyakati tofauti mwezi huu, zilizoandikwa zikieleza kwa kina namna mikopo ya elimu ya juu ilivyogeuka shubiri kwa wanufaika.

Mikopo ambayo inatolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), kwa lengo la kuwezesha wanafunzi wenye sifa kugharimia masomo ya vyuo vya juu.

Na kimsingi walengwa wakiwa hasa wanafunzi wanaotoka katika familia maskini, ambazo hazina uwezo wa kulipia gharama za masomo yao.

Habari hizo zinatokana na malalamiko ya wanufaika ya namna deni linalotokana na mikopo waliyopewa, linavyozidi kuongezeka kila mwaka.

Linapaa kutokana na masharti ya vifungu vya mwongozo wa HESLB wa utoaji mikopo na ruzuku kwa wanafunzi wanayoyaita ni ya 'uonevu.'

Vifungu walivyovilalamikia ni pamoja na kile kinachowataka wanufaika kulipa tozo ya kulinda thamani ya fedha walizopewa, ambapo hukatwa asilimia sita kwa mwaka tangu tarehe mnufaika aliyoanza kupokea mkopo.

Vilevile kifungu kinachotaka bodi ikate asilimia moja ya ada ya uendeshaji kwa mnufaika.

Aidha, kifungu kinachoeleza kwamba iwapo mnufaika atashindwa kulipa mkopo baada ya kipindi cha neema cha miezi 24 akishahitimu masomo yake, ataongezwa makato ya adhabu ya asilimia 10.

Wanufaika wanabainisha kwamba vifungu hivyo vimekuwa shubiri kwao kiasi cha kuathiri ustawi wao kwa ujumla na kwamba kwa masharti hayo inaweza ikachukua hadi miaka 20 kwa wengine kumaliza madeni yao.

Muungwana ana imani kuwa maadamu serikali ya awamu ya tano ni sikivu, itakuwa imesikia kilio hiki.

Hata hivyo, Tulonge ambaye ni mmoja wa waumini wa usikivu wa serikali hii, anaishauri ichukue hatua moja mbele katika kushughulikia malalamiko ya wanufaika wa mikopo hii.

Kwamba kwa kuwa mikopo inatolewa hasa kwa watoto wanaotoka familia maskini ili kuwapa fursa ya kupata elimu ya juu, ni bora wanufaika wakalegezewa zaidi masharti ili lengo la kuwapa mikopo hiyo liwe na manufaa kwao.

Muungwana anashauri wanufaika watakiwe kurejesha kiasi cha fedha walizokopeshwa kugharimia masomo, bila ya tozo ama ada nyingine yoyote kama inavyofanyika sasa.

Msingi wa ushauri huu unajikita kwenye ukweli kwamba wengi wa wanufaika wanatoka familia maskini.

Hivyo kuwawezesha kupitia mikopo hii ni kama kuwanyanyua ili wapatapo ajira ama wanapojiajiri waweze kuziinua familia zao na hatimaye kuondokana na umaskini.

Sasa mnufaika anapotumia miaka zaidi ya 10 kurejesha mkopo aliopewa ukiambatana na makato ya ada na tozo, inakuwa ni kumpa mzigo wa kuufanyia kazi badala ya kuwa fursa ya kusaka maendeleo yake binafsi, familia, jamii na hatimaye taifa kwa ujumla.

Kwa maoni ya Muungwana, mantiki ya kumpa mkopo mnufaika inakuwa na nguvu zaidi pale anapowekewa mazingira mazuri baada ya masomo yake.

Mazingira hayo ni pamoja na kumtaka arudishe kiasi halisi cha mkopo aliopewa bila ya nyongeza.

Lakini msingi mwingine wa ushauri huu unatokana na ukweli kwamba elimu ni haki ya kila mtu kwa mujibu wa Katiba, na serikali ina wajibu wa kuhakikisha watu wote wanapata fursa sawa na za kutosha kuwawezesha kupata elimu.

Na ndiyo maana inatoa elimu bure kuanzia shule za awali hadi kidato cha nne ili kutimiza moja ya majukumu yake ya kikatiba kwa wananchi wake.

Hivyo kuwapa fursa wanufaika ya kurejesha kiasi halisi cha fedha walizokopeshwa bila ya ada na tozo zingine, ni suala la kikatiba vilevile.

Aidha, ni ukweli vilevile kwamba, serikali haifanyi biashara katika elimu na ndiyo maana imeondoa ada na tozo zilizokuwa zikitozwa kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Sasa kuweka ada na tozo kwa wanufaika wa mikopo elimu ya juu ni sawa na serikali kufanya biashara katika elimu kwa maoni ya Muungwana.

## TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU
# KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
# WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)

Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),
Simu Na: +255- (0)22 -2760548/276055
Nukushi Na: (022) 27605
Barua pepe: info@osha.go.tz

P.O Box 519,
**DAR ES SALAAM.**

# TAARIFA KWA UMMA

## JITIHADA ZA OSHA KATIKA KUWEZESHA UCHUMI WA VIWANDA NA KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA NA UWEKEZAJI NCHINI.

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli imedhamiria kuwainua watanzania kutoka katika kipato cha chini kwenda kipato cha kati kupitia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ambayo mkazo wake ni kujenga uchumi wa viwanda. Serikali imeendelea kufanya jitihada mbali mbali ili kufikia lengo hilo ambapo miongoni mwa jitahada hizo ni kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kupitia andiko lake (Blue Print) ambalo limeainisha changamoto ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na taasisi mbali mbali ili kufikia azma hiyo.

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ukiwa ni miongoni mwa taasisi za serikali zinazohusika moja kwa moja na uwezeshaji wa biashara, unapenda kuwafahamisha wadau wake na umma kwa ujumla kuwa umefanya maboresho mbali mbali katika utoaji wa huduma kwa wananchi ikiwa ni utekelezaji wa maazimio yaliyomo kwenye andiko tajwa.

Baadhi ya mambo yaliyoainishwa katika andiko ni pamoja na upunguzaji wa gharama za uendeshaji katika biashara na uwekezaji kwa kupunguza tozo na ada mbalimbali pamoja na kuondoa urasimu katika kutoa huduma ikiwemo kuondoa mwingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi zake. Katika kutekeleza andiko hilo OSHA imefanya mambo yafuatayo;

**1. Marekebisho ya sheria kuhusiana na Tozo na Ada.**
Wakala umefanya marekebisho ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, 2003 kupitia GN 719 ya Tarehe 16 Novemba 2018 kwa kuondoa tozo mbalimbali kama ifuatavyo;

(i) Ada ya Usajili wa eneo la kazi iliyokuwa ikitozwa kati ya **Sh. 50,000 hadi Sh.1, 800,000;**
(ii) Ada ya fomu ya usajili sehemu za kazi iliyokuwa ikitozwa **Sh. 2,000;**
(iii) Faini zinazohusiana na vifaa vya kuzimia moto ya Sh. 500,000 ambayo ilikuwa inaingiliana na taratibu zinazosimamiwa na Jeshi la Zimamoto ya Uokozi.
(iv) Ada ya Leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama iliyokuwa inatozwa **Sh 200,000 kwa mwaka**; na
(v) Tozo ya ushauri wa kitaalamu wa Usalama na Afya ya **Sh 450,000 kwa saa kwa mtaalam mmoja.**

Matokeo ya kuondoa tozo na ada hizi ni pamoja na ongezeko kubwa la sehemu za kazi ambazo zimesajiliwa. Kwa mfano: kwa mwaka wa fedha 2018/19 sehemu za kazi zipatazo 16,457 zilisajiliwa ukilinganisha na 3,354 zilizosajiliwa kwa mwaka 2017/18 kabla ya kuondoa tozo hizo. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 491(491%). Katika utekelezaji wa Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003, ongezeko hili linamaanisha kwamba sehemu nyingi za kazi zimefikiwa na OSHA na idadi ya kaguzi zimeongezeka na hivyo hali ya usalama na afya mahali pa kazi inazidi kuimarika nchini.

**2. Kuondoa Urasimu**
Katika Kuondoa urasimu wa utoaji huduma, Wakala umefanya mapitio ya Mlolongo wa Biashara **(Business Process Review)** ili kubaini maeneo yanayoleta urasimu katika utekelezaji wa majukumu na katika mapitio hayo OSHA tumefanikiwa kufanya yafuatayo:

(i) Kupunguza muda wa kupata Cheti cha Usajili wa sehemu ya kazi (Registration Certificate) kutoka **siku 14** hadi **siku 1** baada ya mwombaji kukamilisha mahitaji yote ya usajili.
(ii) Kupunguza muda wa kushughulikia na kutoa Leseni ya Kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (Compliance License) kutoka **siku 28** hadi **siku 3** baada ya kukamilisha taratibu zote muhimu.

**3. Usimikaji wa Mfumo wa Tehama**
OSHA ipo katika hatua za mwisho za kusimika mfumo wa TEHEMA ujulikanao kama (Workplace Inspection Management System (**WIMS**) ambapo kupitia mfumo huo usajili wa maeneo ya kazi utafanyika kwa njia ya kielektroniki hivyo kusogeza huduma zaidi na kupunguza mlolongo wa kupata cheti na huduma zingine za kaguzi. Aidha, mfumo huu utakuwa na uwezo wa kuunganishwa na mifumo mingine ndani ya serikali, hivyo kurahisisha upatikaji wa taarifa.

**4. Kuongeza Uwajibikaji**
Wakala umeongeza uwajibikaji na kuimarisha mifumo ya usimamizi. Hii ni pamoja na kuanzisha dawati la kushughulikia kero na malalamiko mbali mbali ya wadau. OSHA imeanzisha pia utaratibu wa wakaguzi wake kufanya kaguzi kwa timu badala ya mkaguzi mmoja mmoja. Utaratibu huu unalenga kuongeza uwazi katika ukaguzi na hivyo kuongeza ubora na ufanisi katika utoaji huduma na kuondoa usumbufu kwenye maeneo ya kazi kwa kila mkaguzi kuingia eneo la kazi kwa wakati wake. Utaratibu huu umesaidia sana kupunguza malalamiko na kuongeza ufanisi.

**5. Uratibu wa Ukaguzi kupitia Makao Makuu ya taasisi/kampuni (Corporate Inspections)**
Wakala umeendelea kuwahamasisha wafanya biashara, makampuni ama wawekezaji wenye ofisi na matawi mengi katika mikoa mbalimbali nchini kuratibu shughuli za ukaguzi, mafunzo na upimaji afya kwa kupitia ofisi zao za Makao Makuu ili;

(i) Ziweze kufanyiwa ukaguzi, mafunzo na upimaji afya kwa wakati mmoja badala ya kila ofisi kufanya ukaguzi kwa wakati wake.
(ii) Kurahisisha upatikanaji wa Leseni ya kukidhi matakwa ya usalama mahali pa kazi kwa ambayo hutolewa kwa ofisi na matawi yote nchini kwa wakati mwafaka.
(iii) Kuwarahisishia waajiri kupanga ratiba ya ukaguzi na masuala ya kibajeti yanayohusu Usalama na Afya katika sehemu zao za kazi.
(iv) Kuwezesha menejimenti kupata mrejesho wa hali ya Usalama na Afya katika maeneo yao yote nchini kwa wakati kwaajili ya utekelezaji kwa mujibu wa Sheria.

**6. Kuongeza uelewa wa masuala ya Usalama na Afya miongoni mwa wadau hususani katika sekta isiyo rasmi.**
Katika kipindi cha hivi karibuni, serikali kupitia OSHA imekuwa ikigharamia mafunzo kwa wenye viwanda vidogo, wajasiriamali wadogo na vikundi vya walemavu wanaojishughulisha na usindikaji wa vyakula, ushonaji na utengenezaji batiki, wachimbaji wadogo, mafundi, wakulima, wanaofanya usafi wa barabara na sehemu nyingine zinazotumiwa na umma. Jumla ya wajasiriamali wadogo 28,275 walinufaika na programu hii ya mafunzo katika mikoa ya Tabora, Mtwara, Ruvuma, Dodoma, Arusha, Mbeya, Mwanza, Iringa, Shinyanga, Pwani, Songwe, Singida, Kilimanjaro, Rukwa na Dar Es Salaam. Matokeo ya programu hii ambayo ni endelevu, yalipelekea kupata uelewa wa namna ya kujikinga na vihatarishi vinavyoendana na shughuli zao za kiuchumi.

Hivyo, mafunzo haya na mengine wanayoyapata husadia kuwahamasisha kujua umuhimu wa kurasimisha biashara zao bila kuwa na hofu ya tozo na ada kwani wanatambua kuwa afya na usalama wao ndio rasilimali kubwa katika uzalishaji. Programu hizi ni muhimu hasa kwa kuzingatia kuwa sekta isiyo rasmi inaajiri watu wengi na ndio yenye mazingira hatarishi zaidi kwa kukosekana mifumo rasmi ya usimamizi.

**7. Kuimarisha ushirikiano na Taasisi nyingine za umma na binafsi.**
Miongoni mwa changamoto zilizoainishwa katika Andiko la Blueprint ni pamoja na mwingiliano wa majukumu ya OSHA na taasisi nyingine kama TBS, TFDA, ERB n.k. Katika kushughulika changamoto hii, OSHA inafanya yafuatayo;

(i) Kushirikiana na taasisi nyingine za serikali kama vile Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ( WCF), Shirika na Viwango la Taifa (TBS); katika kuandaa viwango, Mkemia Mkuu wa Serikali katika kubadilishana taarifa, ERB na CRB; katika kutambua miradi ya ujenzi inayoanzishwa nchini pamoja na NBS,BRELA;TRA katika kupata taarifa za maeneo ya kazi nchini.
(ii) Kushiriki katika kutoa elimu ya masuala ya Usalama na Afya kwa wadau katika sekta ya umma na makampuni binafsi.
(iii) Kushirikiana na taasisi nyingine ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu (OWM- KVA) kufanya kaguzi za pamoja kama vile Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Idara ya Kazi, NSSF, PSSSF na nyinginezo.
(iv) Kushiriki kikamilifu katika kutoa huduma katika dawati la pamoja lililopo chini ya **Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC).**
(v) OSHA inashirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taasisi nyingine katika programu ya Kliniki ya Biashara **(Business Clinic)** inayoratibiwa na Mamlaka ya Uendelezaji Biashara ya Tanzania (TANTRADE).

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA); ni taasisi ya umma yenye dhamana ya kulinda Usalama na Afya wa wafanyakazi wanapokuwa katika sehemu zao za kazi kupitia usimamizi wa **Sheria Na. 5 ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.**

Majukumu ya msingi yanayotekelezwa na OSHA chini ya Sheria tajwa ni pamoja na; Kufanya ukaguzi wa Usalama na Afya katika sehemu za kazi, kupima afya za wafanyakazi kulingana na kazi wanazofanya, kutoa mafunzo ya Usalama na Afya mahali pa kazi, kuchunguza ajali zinazotokea katika sehemu za kazi pamoja na kuishauri serikali katika utungaji wa Sheria, Sera, Kanuni, Miongozo na Mikataba ya Kimataifa inayohusu usimamizi wa Usalama na Afya katika sehemu za kazi.

Hivyo, tunawakumbusha wadau wetu na umma kwa ujumla kuendelea kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, 2003 kwa kusajili maeneo yao ya kazi na kuhakikisha kwamba yamefanyiwa ukaguzi ili kukidhi matakwa ya Sheria na kuboresha usalama na afya katika sehemu za kazi.

**Usalama na Afya kazini kwa maendeleo ya uchumi wa viwanda**

***Kwa taarifa zaidi;***
***Tembelea tovuti yetu (www.osha.go.tz);***
***Tupigie kupitia simu ya bure: 0800110091/0800110092 au;***
***Tutumie barua pepe kupitia: info@osha.go.tz.***

**IMETOLEWA NA;**
**KAIMU MTENDAJI MKUU**
**WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)**

215390002

# Mwalimu abambwa na meno ya tembo

**Na Hamisi Nasiri, MASASI**

MWALIMU wa Shule ya Msingi Chikunja, Masasi mkoani Mtwara, Karimu Daudi (35), na wenzake wawili wamekamatwa na polisi mkoani hapa wakiwa na vipande sita vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilo 15.

Kamanda wa Polisi mkoani Mtwara, Blasius Chatanda, alisema jana kuwa mwalimu huyo na wenzake hao, walikamatwa juzi majira ya 11 jioni katika mtaa wa Wapiwapi kata ya Napupa wilayani Masasi.

Alisema polisi waliwakamata watu hao wakati wa doria wakiwa na meno hayo aliyokuwa wameyapakia kwenye gari aina ya Toyota Paso lenye namba za usajili T 663 CWD na kuhifadhiwa kwenye mfuko wa salfeti.

Kamanda Chatanda alisema baada ya polisi watuhumiwa hao, waliwakuta na vipande hivyo ambavyo haijajulikana vina thamani gani ya fedha.

Chatanda aliwataja watuhumiwa wengine waliokamatwa kuwa ni Mohamed Salum (39) mkazi wa Kitunda mkoani Dar es Salaam na Selemani Ally Mkazi wa kijiji cha Muwesi, Nanyumbu mkoani Mtwara.

Alisema Jeshi la Polisi linatarajia kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao pindi uchunguzi utakapokamilika na kwamba litaendelea na msako dhidi ya watu ambao wanajihusisha na utoroshaji wa nyara za serikali.

"Natoa wito kwa watumishi wa serikali kutii kiapo cha kazi zao kwani inashangaza kuona mtumishi wa umma anajihusisha na biashara haramu tena ya rasilimali za taifa. Watumishi fanyeni kazi kutii maadili na kuwa waadilifu na kazi zenu," alisema Chatanda.

Alisema kitendo cha watumishi wa serikali kujiingiza kwenye utoroshaji wa rasilimali za umma hakileti picha nzuri ilhali watumishi hao wameapa kiapo cha kazi kwa mujibu wa sheria za nchi, hivyo Jeshi la Polisi halitamfumbia macho mtu yeyote ambaye anakiuka taratibu za nchi hata iwe ni mtumishi wa umma. Chatanda alisema polisi wataendelea kuweka msako mkali usiku dhidi ya watu wanaosafirisha nyara za serikali, huku wakimaliza rasilimali za nchi kama vile tembo na wanyama wengine kwa manufaa yao binafsi.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa jamii kushirikiana kwa pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama katika kudhibiti rasilimali za taifa na pale wanapoona baadhi ya watu wanasafirisha nyara hizo watoe taarifa ili sheria ichukue mkondo wake.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kulia), akipokea moja ya zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Buchi Herbal Products, Hazim Rungwa, kabla ya kuzindua Taasisi ya Urembo na Vipodozi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri abaini ufisadi ukarabati shule

**Na Boniface Gideon, TANGA**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amebaini ubadhirifu mkubwa wa fedha katika ukarabati wa Shule kongwe ya Sekondari ya Galanos iliyoko jijini hapa.

Ole Nasha alibaini hayo alipotembelea maagizo mazito kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Daud Mayeji, kumchukulia hatua mhandisi wa jiji kwa kujenga mradi huo chini ya kiwango.

Alisema serikali ilipeleka Sh. milioni 900 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa maeneo mbalimbali kwenye shule hiyo ikiwa ni sehemu ya mpango wa ukarabati wa shule kongwe nchini.

Hata hivyo, alisema ukarabati katika shule hiyo umefanyika kwa asilimia 40, hali ambayo alisema kazi hiyo iko chini ya kiwango hasa katika maeneo ya madarasa.

Ole Nasha alisema mkandarasi alipaswa kutengeneza uzio wa chuma lakini alitumiamatofali ya simenti haliambayo inahatarisha maisha ya wanafunzi kwa kuwa uzio umejengwa juu ya ghorofa.

"Wasiwasi ni kwamba unapoandika mchoro halafu ukakiuka ni kinyume cha taratibu. Hali hiyo inaweza kuharibu uimara wa jengo na hapa panaonyesha pamefanyika matumizi mabaya ya fedha. Nimemwagiza mkurugenzi wa jiji afuatile na kujua kwa nini kuna ukiukwaji wa makusudi wa kuacha kufuata maelekezo ya mchoro," alisema.

Alisema ni lazima maagizo ya serikali yanapotolewa yazingatiwe na kama kuna utofauti ni lazima kuhakikisha kuna makubaliano kabla ya kuendelea na utekelezaji wake.

Naibu Waziri alisema katika ujenzi huo, Mhandisi wa Jiji, Priscus Massawe, hawezi kukwepa kuwajibika kwa sababu ni kitu ambacho yeye mwenyewe amechora, lakini ndiye amehusika kubadilisha gharama za ujenzi (BOQ) jambo ambalo limesababaisha mvutano na kamati ya ujenzi.

Mkurugenzi wa Jiji, Mayeji, alikiri kuwapo kwa dosari hiyo na kuahidi kuifanyia kazi mara moja.

SOMA GAZETI LAKO LA THE GUARDIAN NA NIPASHE POPOTE ULIPO KUPITIA
epaper.ippmedia.com
UTAPATA GAZETI LA THE GUARDIAN NA NIPASHE KWA URAHISI ZAIDI
UTAPATA HABARI MPYA KILA SIKU
UTAPATA TAARIFA ZA ZABUNI (TENDER) NA NAFASI ZA KAZI



Ingia kwenye GooglePlay au ios (Apple Store) kisha tafuta **The Guardian-IPP Media**
Superbrands East Africa's Choice · The Guardian · GET IT ON Google Play · Available on the App Store · Nipashe

# Majeruhi mwingine ajali lori mafuta afariki dunia

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kutokana na ajali ya lori la mafuta iliyotokea mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka huu, imefika 102 baada ya majeruhi mwingine kufariki dunia juzi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Vilevile, imeelezwa na uongozi wa MNH kuwa majeruhi sita kati ya 13 wanaoendelea kupatiwa matibabu katika hospitali hiyo, hali zao zinaendelea kuimarika.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alimtaja aliyepoteza maisha juzi kuwa ni Greyson Ndabiti (29).

Alisema kufuatia kifo hicho, jumla ya majeruhi waliobaki MNH ni 13. Kati yao, saba wako katika chumba za uangalizi maalum (ICU) na wengine sita hali zao zinaendelea vizuri na wanafanya mazoezi. "Wagonjwa hawa sita wako wodi za kawaida wanaendelea na mazoezi na ushauri wa kisaikolojia na hali zao zinaendelea kuimarika, lakini hawatarajii kutoka wodini mapema kwa sababu matibabu yao ni endelevu," Aligaesha alisema.

Aliongeza kuwa kuna wagonjwa wengine ambao wanahitaji kufanyiwa upasuaji kutolewa ngozi na kuhamishia maeneo ya mwili yenye majeraha makubwa.

Aligaenda alisema hospitali hiyo inaendelea na jitihada za kuhakikisha inaokoa maisha ya majeruhi wengine waliobaki kwa kuwa ina wataalamu na vifaa tiba vya kutosha.

Tangu Agosti 10, mwaka huu, MNH ilianza kupokea majeruhi ambao walifika 47 na kati yao, 34 tayari wamepoteza maisha wakati wakiendelea kupatiwa matibabu.

Ajali hiyo ya moto ilitokea baada ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, kuanguka eneo la Msamvu Itigi mkoani Morogoro na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.

# Wakulima 'walivyovuna' mabilioni ya ufuta

**Na Said Hamdani,** LINDI

WILAYA ya Kilwa mkoani Lindi, imevuna jumla ya kilo 15,800,000 za ufuta kwa msimu wa kilimo wa mwaka huu, hivyo kuvuka lengo lililowekwa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Christopher Ngubiagai, aliiambia kuwa Kilwa ni miongoni mwa wilaya tano za mkoa huo unaozalisha kwa wingi ufuta, ambapo kwa msimu wa mwaka huu, ulijiwekea lengo la kuzalisha kilo milioni 15, lakini kutokana na jitihada zilizoonyeshwa na wakulima, wamevuka lengo kwa kuzalisha kilo milioni 15.8.

"Matarajio yalikuwa kuvuna kilo milioni 15, lakini tumefanikiwa kuvuka lengo kwa kuzalisha kilo milioni 15.8," alisema Ngubiagai.

Ngubiagai alisema kwa bei ya Sh. 2,600 na kuendelea kwa kilo moja, zao la ufuta limeweza kuwaingizia wakulima wa Wilaya ya Kilwa zaidi ya Sh. bilioni 48 kwa msimu wa mwaka huu wa 2019 pekee ukilinganisha na wa mwaka jana.

Alisema pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto kubwa zinajitokeza katika zoezi zima la ukusanyaji, uuzaji na usafirishaji wa zao hilo kutoka kwa baadhi ya vyama vya msingi na ushirika (Amcos).

Alisema Wilaya ya Kilwa ina Amcos 22, lakini kati ya hivyo tisa vimebainika kuwa na ubadhirifu mkubwa, kutokana na kile kilichoelezwa viongozi na watendaji wake kujenga mashirika na wafanyabiashara wasio waaminifu kuwadhulumu wakulima.

Alisema Agosti 20, mwaka huu kikosi kazi kilichoundwa na halmashauri ya wilaya hiyo kufuatilia utoroshaji mazao, kilikamata lori moja aina ya Scania na tela limebeba kilo 32,000 za ufuta ukisafirishwa kutoka Chama cha Linare Amcos Kijiji cha Likawage kwenda jijini Dar es Salaam bila ya kuwa na kibali.

Alisema ameamuru kukamatwa kwa viongozi na watendaji wa chama hicho kwa mahojiano na watakapothibitishwa kuhusika, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao, ikiwamo kuwafikisha mahakamani kwa hatua zaidi.

**Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto kubwa zinajitokeza katika zoezi zima la ukusanyaji, uuzaji na usafirishaji wa zao hilo kutoka kwa baadhi ya vyama vya msingi na ushirika (Amcos).**

# Waumini wa AICT watakiwa kujiandikisha daftari wapigakura

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAUMINI wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha na kurekebisha taarifa zao kwenye daftari la kudumu la mpigakura pamoja na kujitokeza kuchagua viongozi ambao watawasimamia katika shughuli za maendeleo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mkuu wa AICT nchini, Josephati Mtebe, wakati wa ibada ya ufunguzi wa kanisa lililojengwa kwa nguvu ya waumini na kugharimu Sh. milioni 902.3.

**Katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu, ni vyema waumini wakafanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi wenye sifa.**

Mtebe alisema kila muumini anatakiwa kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la mpigakura pamoja na kurekebisha taarifa zake na kuwataka viongozi wa makanisa, wachungaji na manjirista kugombea nafasi za uongozi.

"Viongozi wa kanisa, wachungaji wetu hakikisheni waumini wote wamejiandikisha kwenye daftari la mpigakura na ikiwezekana ninyi wenyewe mkagombanie nafasi za uongozi kwenye mitaa yetu na uchaguzi mkuu mchukue nafasi kwenye kata na majimbo," alisema Mtebe.

Alisema kuwa, katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka huu, ni vyema waumini wakafanya maamuzi sahihi ya kuchagua viongozi wenye sifa, wasiokuwa watoa rushwa na walevi ambao si waadilifu wanaotaka madaraka kwa maslahi yao binafsi.

Mwenyekiti wa ujenzi na katibu wa AICT Lahama Charles alisema kanisa limejipanga kujenga shule ya msingi, ujenzi wa sekondari na zahanati pamoja na ukamilishaji hosteli ya kanisa kupitia idara ya vijana.

Askofu Mkuu wa Makanisa ya AICT, Mussa Masanja Magwesela, alisema bila michango ya waumini kanisa lisingejengwa, na kuwataka waumini kulitumia kanisa hilo kwa matumizi yaliyopangwa badala ya kulitumia kuanzisha mabishano ya kisiasa.




Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Saruji Tanga, Lau Masha (wa nne kushoto), akizungumza wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa wa kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Reinhardt Swart na baadhi ya wajumbe wa bodi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tanga Cement yatangaza faida bil.14.9/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tanga Cement (TCPLC) imetangaza kupata faida ya uendeshaji ya Sh. bilioni 14.9 kwa kipindi cha mwaka kinachoishia Desemba 31, 2018 kutokana na hasara iliyotokana na uendeshaji ya Sh. bilioni 10.99 kwa mwaka 2017.

Akizungumza wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa wanahisa wa kampuni hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Bodi ya TCPLC, Lau Masha, alisema pia kuwa utendaji wa mwaka 2018 umesaidia kupunguza hasara baada ya kodi ya Sh. bilioni 11.3 kutoka Sh. bilioni 26.3 kwa mwaka 2017.

"Mauzo ya kundi letu yalipanda kwa asilimia 25 na kufika Sh. bilioni 214.9 kutoka Sh. bilioni 171.8 zilizopatikana kwa mwaka uliopita wakati faida ghafi kwa mwaka iliongezeka kwa asilimia 91 na kuwa Sh. bilioni 56.2 kutoka Sh. bilioni 29.4 zilizopatikana mwaka uliopita," alisema.

Mwenyekiti huyo aliongeza kuwa ukuaji wa biashara ulijikita katika ukuaji wa simenti na sekta ya ujenzi nchini Tanzania. Matumaini ya miundombinu chini ya mipango ya dira ya maendeleo ya serikali ya mwaka 2025.

Alisema kutokana na Tanzania kuwa soko la pili kwa ukubwa kwa masuala ya ujenzi Afrika Mashariki, uzalishaji wa saruji unatarajiwa kuongezeka, hivyo kampuni yao imejipanga kuhakikisha inanufaika na ukuaji huo katika soko la kanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Reinhardt Swart, alisema, kampuni iliongeza uzalishaji kwa kipindi chote hiki cha mwaka na kuzalisha mapato ya ziada kutokana na mauzo ya ziada iliyozalishwa.

Aliongeza kuwa mkataba wao na Shirika la Reli Tanzania (TRC) umewawezesha kupata mabehewa zaidi ambayo yapo kwa ajili ya usafirishaji katika maeneo yao ya kimkakati ya usambazaji.

Unafuu huo unapunguza gharama za kuhifadhi na usafirishaji huku ukiupa nguvu usafiri wa reli na usambazaji nchini.

"Ingawa kushuka kwa thamani ya fedha na riba tunayolipa kutokana na mkopo tuliochukua kwa ajili ya mtaji wa uwekezaji mpya wa kinu namba mbili (TK2) vimeendelea kubakia kuwa matumizi ya gharama kubwa, hasara baada ya kodi kwa mwaka 2018 ilipungua," aliongeza mkurugenzi huyo.

Pamoja na mafanikio hayo kampuni haikutangaza gawio la mpito kwa wanahisa wake kwa mwaka 2018 kutokana na sababu zilizoelezwa mahali hapo kuwa ni hali iliyotokana na utendaji wake wa kifedha kwa mwaka 2017, hivyo bodi kuamua kutumia busara kutotangaza gawio la mwisho ili fedha iliyopo kutumika katika shughuli za utendaji na kulipia madeni.

# Kizimbani kwa tuhuma za kumfanyia ukatili mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

VUAI Faki Ali (32), mkazi wa Kisiwa Panza Wilaya ya Mkoani Pemba, amefikishwa katika Mahakama ya Mkoa Chakechake kwa kosa la kutorosha, kubaka na kumfanyia udhalilishaji mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 13.

Mwendesha Mashtaka wa Mahakama hiyo, Seif Mohamed Khamis, mtuhumiwa alikana kutenda makosa hayo na kuiomba mahakama impatie dhamana.

"Mheshimiwa hakimu, mimi sijafanya makosa hayo, lakini pia naiomba mahakama inipatie dhamana," alidai mtuhumiwa.

**Mheshimiwa hakimu, mimi sijafanya makosa hayo, lakini pia naiomba mahakama inipatie dhamana.**

Hakimu wa mahakama hiyo, Luciano Makoye Nyengo, alilikataa ombi la dhamana kwa mshtakiwa na kuamuru apelekwe rumande hadi Septemba 3 mwaka huu.

Ilidaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alitenda makosa matatu, ambapo kosa la kwanza alitenda Julai 5, mwaka huu saa 1:00 usiku, kwa kumtorosha mtoto huyo kutoka nyumbani kwao na kumpeleka nyumba anayoishi yeye.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume cha kifungu cha 113 (1) (a) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

Kosa la pili ni kumbaka saa 1:05 usiku Kisiwa Panza, baada ya kumtorosha.

Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 108 (1) (2) (a) na kifungu cha 109 (1) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

Kosa la tatu ni kumdhalilisha kwa lengo la kukidhi matamanio yake. Kufanya hivyo ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 139 (1) (a) na (2) (b) cha Sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.



Fundi wa kampuni ya Estim, akiendelea na ujenzi wa upanuzi wa Barabara ya Morogoro, katika eneo la Kimara Temboni, jijini Dar es Salaam jana, itakayojengwa kwa njia sita kuanzia Kimara hadi Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri Ulega: Tumeuzika uvuvi haramu

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema kwa sasa inatarajia ongezeko kubwa la mazao ya baharini na katika maziwa baada ya kufanikiwa kudhibiti uvuvi haramu wa kutumia mabomu.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo juzi baada ya kutembelea mnada wa uuzaji samaki Kunduchi jijini Dar es Salaam.

Alisema uvuvi haramu wa kutumia mabomu umepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyo kuwa miaka ya nyuma kutokana na kazi kubwa ambayo imefanywa na serikali kuudhibiti na kwamba ndani ya mwaka huu hakuna tukio lolote la uvuvi haramu lililoripotiwa

Ulega alisema moja ya siri zilizofanikisha kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu ni ushirikiano kati ya serikali na wavuvi waaminifu ambao wamekuwa wakiwafichua wenzao baada ya kubaini kufanya vitendo hivyo.

"Uvuvi haramu tumefanikiwa kuuzika, iwe baharini au katika maziwa, hakuna mlipuko wa mabomu kwa sasa, hivyo tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa na naomba tusirudi huko tena kwa sababu mbali na kuathiri mazao ya baharini na mazingira, lakini kuna watu wamebaki vilema kwa ajili ya hayo mabomu," alisema na kuongeza:

"Ninyi mnatakiwa mtuunge mkono kuhakikisha hamrudi nyuma, serikali ya awamu ya tano ipo kwa ajili ya kushirikiana na wananchi wake."

Akijibu malalamiko ya wavuvi kuhusu uvuvi unaotumia nyavu za kisasa maarufu kama Ringnet, Ulega alisema serikali italifanyia kazi katika kipindi hiki ambacho wanafanya uboreshaji wa kanuni za uvuvi.

Alisema lengo ni kuboresha mazingira katika sekta ya uvuvi na kuhakikisha mazingira ya bahari yanahifadhiwa pamoja na kutoathiri upatikanaji wa dagaa ambao ni biashara kubwa kwa wavuvi hao na kinamama ambao hufika hapo na kununua kwenda kuuza na kujipatia kipato cha kukidhi mahitaji yao.

Kuhusu leseni, Ulega aliwatoa wasiwasi kwamba mvuvi hapaswi kuwa na leseni zaidi ya moja na kwamba mvuvi anapokuwa na leseni moja inamtosha kuendesha shughuli za uvuvi mahali popote

"Leseni ya uvuvi ni moja ukikata Mkulanga utatamba nayo mpaka Mtwara, ukikata Mtwara utatamba nayo mpaka Lindi mpaka Tanga," alisema Ulega.

Salimu Said Ali, mvuvi katika eneo hilo, alisema baadhi ya samaki ambao walipotea tangu mwaka 2000 kutokana na uvuvi haramu, wameanza kupatikana akiwamo jodari.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, aliwaahidi wavuvi wa eneo hilo kushughulikia suala la ujenzi wa choo ili ifikapo Desemba mwaka huu uwe umekamilika.

# DC aitaka TRA, halmashauri kuifuatilia CITL

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Machana, ameitaka Mamlaka ya Mapato (TRA)mkoa maalumu wa kikodi wa Kahama na Halmashauri ya Mji wa Kahama kuhakikisha wanatembelea ofisi ya uwekezaji ya CITL ili kuona uhalali wake katika kufanya uwekezaji wilayani hapa.

Macha aliyasema hayo juzi wakati akizindua ofisi mpya ya kampuni ya CITL ambayo inajihusisha na uendeshaji wa biashara kwa njia ya mtandao na uwekezaji wa mwananchi mmoja mmoja, ambapo alisema hatua hiyo itasaidia kuwaondoa hofu wananchi katika uwekezaji wao.

Aidha, alisema wananchi wengi wamekuwa waathirika kutokana na taasisi kama hizo kwenda katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kuchangia kupoteza fedha zao na kuibua migogoro kati ya pande hizo mbili.

Macha alisema, kabla ya kufungua ofisi alitaka kujua uhalali wa kampuni hiyo mpya ya uwekezaji na kuona usajili wake, hali ambayo alijiridhisha kwa kupata nyaraka mbalimbali za uendeshaji wake, hivyo kukubali kuizindua ofisi hiyo.

Pia aliwataka wakazi wa Kahama kuchangamkia fursa zilizopo katika kampuni hiyo, huku akisisitiza viongozi wa CITL kuhakikisha kuwa wanatoa semina kwa wananchi ili kuwa na upeo wa kuwekeza na umuhimu wake.

"Wahusika wa kampuni hii toeni elimu kwa wananchi, ili wawe na upeo wa kuelewa kabla ya kuwekeza na kuwaeleza tofauti ya taasisi hii na benki upo wapi," alisema na kuendelea:

Sitaki mwananchi awekeze leo halafu kesho aje ofisini kwangu kudai fedha zake.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, George Lucas, alisema kampuni imeamua kuwekeza katika mji wa Kahama kwa kuwa mji huo unakua kwa kasi hasa katika shughuli za kibiashara na kama wananchi watajaribu kuwekeza watayaona mafanikio kwa mwaka mmoja.

Alisema wameamua kuweka ofisi Kahama ili waweze kuwafikia watu wa aina zote ili kujua mfumo huo mapema badala ya kusubiri hadi baadaye ambapo watakuwa wamechelewa.

# RC Gambo ataka kamera ukaguzi magari ya utalii

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameagiza kufungwa kamera za usalama (CCTV), katika vituo maalum vya ukaguzi wa magari ya kusafirisha watalii ili kudhibiti matukio ya rushwa kwa askari wa usalama barabarani.

Gambo alisema hayo juzi wakati akizungumza na askari polisi mkoani hapa, wakiwamo wa usalama barabarani ikiwa ni moja ya vikao kazi alichojipangia kufanya ili kuboresha utendaji kazi wa jeshi hilo.

**Lazima ifike mahali kila mmoja katika sehemu yake ya kazi atangulize maslahi ya taifa badala ya kutanguliza maslahi binafsi.**

Alisema vituo hivyo vitakavyofungwa kamera ni vya maeneo ya Kikatiti, Engikareti, Makuyuni na Karatu ambavyo licha ya ukaguzi huo pia watakagua vileo kwa madereva wa watalii ili kuhakikisha usalama unakuwapo kwa wageni hao.

Mkuu wa Mkoa alisema kufungwa kwa kamera hizo, kutasaidia kuondoa utata kwa baadhi ya matukio yakiwamo ya kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa askari wa usalama barabarani.

"Msimamo wa mkoa ni kuhakikisha watalii wetu hawabughudhiwi na trafiki kwa kuwa wanachangia kipato kikubwa kwa mkoa wa Arusha na kuwezesha mkoa kuchangia asilimia 86 ya pato la taifa," alisema Gambo.

Gambo alisema lazima ifike mahali kila mmoja katika sehemu yake ya kazi atangulize maslahi ya taifa badala ya kutanguliza maslahi binafsi.

Pia alisema anaamini ufungwaji kamera na ukaguzi wa vileo kwa madereva hao utakuwa mwarobaini wa kutatua malalamiko ya miaka mingi juu ya rushwa dhidi ya askari hao na kukomesha ajali zisizo za lazima kwa kukamata madereva walevi.



Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, mkoani Manyara, Flatei Massay (kulia), akishiriki na wakulima wa bonde la Bashay, kuondoa magugu kwenye shamba la vitunguu juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Jiji lajipanga kuongeza mapato ya ndani

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imepanga kukusanya Sh. bilioni 20.7 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya ndani.

Mkurugenzi wa jiji hilo, Dk. Maulid Madeni, alisema juzi ofisini kwake jijini hapa kuwa licha ya jiji hilo kuvuka malengo ya makusanyo mwaka wa fedha 2019/20 na kushika namba moja kwa majiji yote nchini, mpango sasa ni kufikia makusanyo yanayozidi Sh. milioni 30 kwa mwaka.

Dk. Madeni alisema pamoja na pongezi nyingi alizopata za kuvuka makusanyo ya ndani, kipaumbele chake si kupongezwa na wala hapokei pongezi hizo bali ni kufikia malengo ya makusanyo aliyojiwekea.

"Mimi si mtu wa kusifiwa na wala sikubali pongezi hizo. Ninachotaka bado hakijafikiwa. Lengo langu ni kufikia makusanyo ya Sh. bilioni 30," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Dk. Madeni alisema Jiji la Arusha limetenga bajeti ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi na ukumbi wa mkutano.

Alisema ujenzi huo unatarajia kuanza mapema mwaka wa fedha 2019/20 na litajengwa jirani na ofisi za sasa za halmashauri hiyo.

Pia mkurugenzi huyo alisema Jiji la Arusha limetoa Sh. milioni 140 kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijiiini (Tarura) kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati barabara zote za jiji hilo zilizoharibiwa na mvua.

Alisema barabara hizo zitafanyiwa matengenezo na kuondoa malalamiko yanayojitokeza kwa watumiaji wa barabara, wakiwamo watumiaji wa vyombo vya moto ambao wamekuwa wakilalamika kuharibika kwa magari yao kutokana na mashimo yaliyopo.

Wakati huo huo, jiji hilo limetia saini mkataba wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 3.5 itakayojengwa kwa Sh. bilioni 4.1.

Akizungumza wakati wa kutia saini mkataba huo baina ya jiji na kampuni ya ujenzi ya Sinohydro kutoka China, Meya wa Jiji la Arusha, Kalist Lazaro, alisema mradi huo ni kazi ya nyongeza ya ujenzi wa mradi wa barabara ya Kisongo Bypass inayotoka Olasiti.

Meya alisema kuwa mkandarasi huyo atafanya kazi yenye ubora kwa miezi minne kuanzia Septemba 11, mwaka huu hadi Januari 11, mwakani atakapokabidhi mradi huo.

# Maktaba ya Arusha yapatiwa vitabu 500

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHULE ya awali ya mchepuo wa kiingereza ya St. Margaret's iliyoko jijini hapa, kwa kushirikiana na klabu ya Rotary Arusha, imekabidhi msaada wa vitabu 500 vya masomo mbalimbali kwa maktaba ya Mkoa wa Arusha.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi wa Shule hiyo, Honest Tesha, alisema wamefikia hatua ya kusaidia vitabu hivyo kutokana na uhitaji wa vitabu uliokuwapo katika maktaba hiyo.

Tesha alisema vitabu hivyo vitasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza kasi ya wanafunzi kusoma kwa wingi vitabu, hivyo kuinua kiwango cha elimu kwa mkoa wa Arusha.

"Baada ya kupata taarifa ya kuwapo kwa uhitaji huo, tuliwaalika wataalamu wa maktaba hii kuja kutembelea maktaba yetu hapa shuleni na kujionea vitabu mbalimbali na kuwapatia kulingana na mahitaji waliyo nayo. Huu si mwisho kwani bado tutaendelea kuwasaidia zaidi kulingana na uhitaji uliopo," alisema Tesha.

Alitaja vitabu vilivyokabidhiwa kuwa ni pamoja na vya sayansi, hesabu na vya watoto wadogo wa elimu ya awali. Alisema lengo kubwa ni kuziba pengo la mahitaji ya vitabu katika maktaba hiyo.

Naye mwakilishi kutoka Rotary Arusha, Samantha Button, alisema hii ni mara ya kwanza kwa klabu hiyo kutoa msaada wa vitabu kwa kuwa wamekuwa wakisaidia masuala mengine mbalimbali ikiwamo uhamasishaji wa upandaji miti na uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali.

Mkutubi wa Maktaba ya Mkoa wa Arusha, Rafiki Mvamba, alisema msaada wa vitabu hivyo umekuja muda mwafaka ambao maktaba hiyo ina uhitaji mkubwa wa vitabu kutokana na kuwapo kwa ongezeko kubwa la wanafunzi wanaofika kujisomea.

Mvamba alisema pamoja na kuwapo kwa msaada huo, bado wanakabiliwa na changamoto kubwa ya vitabu vya kiada kwa kuwa vilivyopo ni vichache na vimechakaa.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni uwapo wa jengo dogo la maktaba na upungufu wa viti kwa kuwa lililopo sasa halitoshi kulingana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaofika kujisomea.

"Kama inavyofahamika kuwa hii ndiyo maktaba pekee kwa mkoa wa Arusha, hivyo idadi ya wanafunzi wanaokuja kujisomea hapa ni wengi sana. Tunaomba tupatiwe viti zaidi pamoja na kupanuliwa kwa maktaba hii kwa kiwango cha ghorofa," alisema.



# Ekari 300 za mazao Siha zakosa maji

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

ZAIDI ya ekari 300 za mazao mbalimbali ya biashara na chakula, zimekauka na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima kutokana na kukosa maji ya umwagiliaji katika kijiji cha Miti Mirefu, Siha mkoani Kilimanjaro.

Changamoto ya kukauka kwa mazao hayo, inatajwa kuwa ni kupungua kwa ujazo wa maji ya umwagiliaji yanayotokana na Mto Simba ambao chanzo chake kiko katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro.

Jana, Kaimu Meneja wa Ofisi Ndogo ya Maji ya Bonde la Kati mkoani Arusha, Dandu Joseph, alisema wanakusudia kwenda Siha kuona na kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo la kupungua kwa maji ya umwagiliaji.

Bonde hilo la kati ndilo lenye jukumu la kisheria la kusimamia ugawaji wa maji ya umwagiliaji.

**Ni kweli tumesikia kwamba kuna malalamiko ya wakulima katika kijiji cha Miti Mirefu na vijiji vya jirani kwamba mashamba yao ya mazao mbalimbali yamekauka baada ya kukosa maji.**

"Ni kweli tumesikia kwamba kuna malalamiko ya wakulima katika kijiji cha Miti Mirefu na vijiji vya jirani kwamba mashamba yao ya mazao mbalimbali yamekauka baada ya kukosa maji," alisema Dandu.

Baadhi ya wakulima wa Miti Mirefu, wanadai kwamba maji hayo yamepungua kutokana na kupelekwa mradi wa majisafi na salama kwa wananchi wa Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

"Unajua kazi ya bonde hili ni kusimamia na kutatua migogoro inayotokea katika matumizi ya maji, kukusanya na kutunza takwimu za mitiririko na hali ya maji kwenye rasilimali za maji pamoja na kusimamia na kuratibu hifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji. Sasa kwa sababu tayari kuna malalamiko, tunakwenda huko kutafuta ufumbuzi wake," alisisitiza Dandu.

Alisema ofisi yake itatuma wataalamu kwenda katika kijiji hicho kuzungumza na viongozi wa serikali wiki hii pamoja na kukikagua chanzo hicho cha Mto Simba ili kufahamu ni nini kinaendelea katika eneo hilo.

Hivi karibuni, Katibu wa Kamati ya Maji ya eneo hilo la Miti Mirefu, Israel Kileo, alisema bomba kubwa la maji lililosimikwa kwenda Wilaya ya Longido kwa zaidi ya kilometa 70, katika baadhi ya maeneo linavuja maji, hivyo kuwa moja ya kisababisha cha kupungua kwa maji.

Wakati malalamiko hayo yakiendelea, Diwani wa Indumet wilayani Siha, Simon Shija, alisema wakulima wa maeneo hayo wamepata hasara ya zaidi ya Sh. milioni 20.

Alipotafutwa Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, kutoa ufafanuzi kuhusiana na malalamiko hayo, alisema kwa ufupi, "ninazo taarifa na ninaendelea kuzifanyia kazi."



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kushoto), akiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Gairo, akiangalia miti iliyopangwa kwa ajili ya kuchoma mkaa, baada ya kufanya ziara katika Hifadhi ya Msitu wa Kumbulu, kujionea miti iliyokatwa kinyume na sheria, wilayani humo, mkoani Morogoro jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Siriel Mchembe. **PICHA: WMU**

# Wananchi 7,000 wanufaika na umeme

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imesema mpaka sasa, idadi ya wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro ambao wamenufaika na punguzo la bei la kuunganishiwa umeme vijijini kwa Sh. 27,000 bila kulipishwa gharama za nguzo wanafikia 7,000.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema jana kuwa mpango huo ulipoanzishwa Mei, mwaka huu, kwa amri ya Rais John Magufuli, watu 5,000 waliunganishiwa huduma hiyo Juni na Julai peke yake.

Alikuwa akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kyeri, wilayani Hai wakati wa uzinduzi wa umeme kwenye kaya zilizonufaika na mpango huo.

"Mkoa wa Kilimanjaro unaongoza Tanzania kwa kuwa na umeme katika maeneo mengi sawa na asilimia 87. Kilimanjaro ina kata 148 ambazo zote zina umeme, una vijiji 519 ambavyo kati yake 453 vina umeme. Ukiangalia bado kuna vijiji 66 tu ambavyo viko Hai (vitano), Siha (saba), Rombo (vinane), Mwanga (vinne), Moshi (22) na Same (20) ambavyo vinasubiri huduma hiyo," alisema Mgalu.

"Mheshimiwa Rais Magufuli ametuagiza tupunguze gharama za kuunganishia wananchi umeme vijijini kutoka Sh. 177,000 hadi Sh. 27,000," alisema.

Naibu Waziri alisema kati ya vijiji 66 vya mkoa wa Kilimanjaro ambavyo bado havijaunganishiwa umeme, vitakavyobakia hadi Desemba mwaka huu ni 35 na kati ya hivyo, serikali imeliagiza Shirika la Umeme (Tanesco) kuchukua vijiji 18 ili iviunganishe.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, mradi wa umeme vijijini awamu ya tatu ya mzunguko wa pili utaunganisha vijiji 17 tu vitakavyokuwa vimesalia.

Akiwa katika kijiji hicho, Naibu Waziri huyo wa Nishati, alitoa namba yake ya simu ya mkononi kwa wananchi wa mkoa wa Kilimanjaro na kuwaelekeza 'wambipu' ili awapigie na kutatua kero husika endapo wataambiwa na Tanesco au mkandarasi yeyote kwamba walipie nguzo, nyaya au mita wakati wakipeleka maombi ya kuunganishiwa umeme.

Aidha, Mgalu alitoa onyo kwa mameneja wa Tanesco ngazi ya wilaya na mkoa ambao watakaidi agizo la serikali linaloelekeza kuwa wananchi wote wa vijijini waunganishiwe umeme kwa gharama ya Sh. 27,000 tu.

# DC Same awatega watumishi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, amewaweka mtegoni watumishi wa serikali ambao wanaishi nje ya vituo vyao vya kazi, baada ya kutangaza kuchukua hatua za kuwasimamisha kazi watakaokaidi agizo la kuhamia kwenye vituo vyao ifikapo Septemba 30 mwaka huu.

Alitangaza uamuzi huo jana wakati akizungumza na wakazi wa Same, baada ya kuzunguka vijijini na kukutana na malalamiko hayo ya wananchi kwamba watendaji wa vijiji, kata na baadhi ya watumishi wa umma, wanaishi nje ya maeneo yao ya kazi na hivyo wanapohitaji huduma za haraka hukosa msaada.

"Idadi ya watumishi wa umma wanaoishi mjini, badala ya kukaa kwenye vituo vyao vya kazi ni kubwa na nimethibitisha kuna shida hiyo kwenye baadhi ya vijiji nilivyopita katika ziara zangu.

Zaidi aliagiza: "Sasa DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya) nakuagiza hakikisha watu wako wanahamia kwenye vituo vya kazi hadi kufikia Septemba 30 na nipate taarifa."

Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2014, inamtaka mtumishi aishi eneo kilipo kituo cha kazi na inawalazimisha watumishi wote wa umma wafuate sheria, kanuni na taratibu za utumishi na atakayeshindwa kuhamia atakuwa amejiondoa kwenye utumishi.

Kutokana na tatizo la watumishi kutokaa vituo vya kazi, Senyamule alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Anna-Claire Shija kumpelekea orodha ya majina ya watumishi wa umma watakaokaidi kuhamia katika vituo vyao ili achukue hatua kwa mujibu wa sheria.

Juni, mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwa katika ziara ya kikazi Bahi mkoani Dodoma, aliagiza watumishi wote nchini wanaoishi mjini wahamie katika vituo vyao vya kazi ili wawe karibu na wananchi.

Alielekeza kuwa watakaokaidi, wakuu wa wilaya wakabidhi orodha yao kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ili awashughulikie kwa kutotekeleza agizo lake.

**Juni, mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwa katika ziara ya kikazi Bahi mkoani Dodoma, aliagiza watumishi wote nchini wanaoishi mjini wahamie katika vituo vyao vya kazi ili wawe karibu na wananchi.**

Nipashe
# TESA
Jumanne Agosti 27, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 15

## Mradi wapunguza mimba, ndoa za utotoni Shinyanga

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

## Mkenya avunja rekodi ya dunia kwa kupika



# SIMANJIRO KATIKA TANZANIA YA VIWANDA

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# TABIA YA KUJICHUKULIA SHERIA MKONONI HAIKUBALIKI



Wananchi wakimwadhibu mtuhumiwa badala ya kumpeleka katika vyombo vya sheria.
**PICHA: MTANDAO**

KUJICHUKULIA sheria mkononi ni kitendo cha kuadhibu mtu aliyefanya kosa bila ya kufuata utaratibu wa sheria za nchi.

Vitendo vya wananchi kujichukulia sheria mkononi vimekuwa vikikithiri siku hadi siku na kuleta madhara kwenye jamii yetu ingawa tunashukuru juhudi kubwa ambazo zimekuwa zikichukuliwa na taasisi zinazohusika katika kuzuia hali hiyo isiendelee kutokea hapa nchini.

Vitendo hivi vya wananchi kujichukulia sheria mkononi vimekuwa vikijitokeza huku sheria ikiwa inakataza wananchi kutoa adhabu na badala yake watuhumiwa wapelekwe kwenye vyombo vya sheria vinavyohusika.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime, katika mahojiano na mwandishi wa makala haya alieleza kuwa jambo la kujichukulia sheria mkononi halikubaliki.

Kwamba halikubaliki popote pale duniani na hata kwenye vitabu vya dini inakatazwa kutoa uhai na kuhukumu mtu pasipo kufuata sheria zilizowekwa katika nchi sambamba na kufuata misingi ya utawala bora na haki za binadamu.

"Nchi yetu inafuata misingi ya utawala bora, hivyo hakuna mahala popote duniani ambapo utawala bora unakubali kutoa roho ya mtu bila kufuata utaratibu...vitendo hivi havikubaliki," anasema SACP Misime.

> SACP Misime anaongeza kwamba "Kwa kuwa zipo njia za utatuzi wa migogoro, sisi kama Polisi hatutakuwa na huruma ama upendeleo kwa wale wote ambao watakuwa wanavunja sheria, kanuni na taratibu ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unaimarika."

Jambo lolote au mgogoro wowote duniani suluhisho lake ni kufanya mazungumzo ya amani kwa pande zote zinazokinzana.

Hii ni miongoni mwa njia sahihi ya kutatua yale yote yanayomkera mtu kwa kufuata taratibu za majadiliano yenye manufaa kwa jamii.

Serikali za Mitaa kama taasisi zilizo karibu na wananchi zimepewa mamlaka ya kushughulikia mambo mbalimbali ndani ya jamii ikiwamo uchumi, ustawi wa jamii, ulinzi na usalama wa mitaa ambapo kupitia kamati zake mambo hayo yanatekelezwa.

SACP Misime anaongeza kwamba "Kwa kuwa zipo njia za utatuzi wa migogoro, sisi kama Polisi hatutakuwa na huruma ama upendeleo kwa wale wote ambao watakuwa wanavunja sheria, kanuni na taratibu ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unaimarika."

Kwa kauli hizo ndipo wajibu wa kila mmoja unapoonekana kwa kila mtu kutekeleza wajibu wake katika kulipinga jambo hili la watu kujichukulia sheria mkononi ili kujiepusha na madhara yatokanayo na vitendo hivyo viovu.

Mchango wa viongozi wa dini ni kufanya doria za kiroho ili kuepukana na jukumu la kujibu mbele ya Mwenyezi Mungu, na viongozi wa serikali wana wajibu wa kujibu na kukemea vitendo vinavyoendelea ambavyo havifuati utaratibu wa sheria na utu.

Wananchi kwa namna moja ama nyingine hawana budi kufuata sheria za nchi kwa kuwakamata wahalifu na kuwakabidhi kwa Jeshi la Polisi ama mamlaka zingine za kisheria ili waweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria badala ya kuwaadhibu jambo ambalo linaweza kusababisha majeruhi hata mauaji kwa watu wanaotuhumiwa kutenda uhalifu ndani ya jamii.

Imetolewa na:-
Kitengo cha Uhusiano,
Makao Makuu ya Jeshi la Polisi,
Dar es Salaam,
habariphq@gmail.com



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Twaambiwa elimu ni bahari

KICHWA hicho cha habari chatueleza kuwa bahari huwa kubwa na haina mwisho. Ndivyo ilivyo elimu kwani binadamu hakomi kujifunza mambo awapo hai.

Vilevile "Elimu ni taa, gizani huzagaa." Maana yake elimu ni kitu muhimu kama taa inavyoweza kutuangazia penye kiza. Methali hii hutumiwa kutufunza faida zinazotokana na elimu. Binadamu hawezi kuyamudu mazingira yake vizuri bila ya kuwa na elimu.

'Kamusi' ni kitabu chenye orodha ya maneno yaliyopangwa kwa alfabeti na kuelezwa fasili zake, aina, matumizi na taarifa nyingine zinazohusiana nayo.

Hivyo Kamusi la Kiswahili Fasaha (Zanzibar) linaeleza kwa ufasaha baadhi ya maneno ya Kiswahili yanayotumika vibaya. (tazama K470, K471 na K472).

Tanzania Bara maneno 'muhanga', 'kwa niaba yangu', 'ufisadi', mbele/ mbeleni, 'nyumba ndogo', 'upungufu', 'husika' n.k. ni baadhi ya maneno yanayotumiwa tofauti na maudhui (mambo yanayoelezwa katika hadithi, riwaya, hotuba, tamthilia au simulizi) yake.

Kwa mfano: 'Muhanga' ni mtu anayejitolea nafsi yake kwa kujiingiza na kufanya jambo linalosababisha kifo chake. Kifo cha mtu anayejitoa muhanga sio cha bahati mbaya, bali ni cha kupangwa na chenye dhamira maalumu. Kwa hiyo watu wanaokufa kutokana na majanga kama vita, moto, zilizala (mtikisiko; tetemeko la ardhi), mafuriko, ajali za barabarani, angani au baharini, si sahihi kuwaita 'wahanga' bali ni waathiriwa wa matokeo hayo.

Wakati mwingine wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi na kuku au hata binadamu huweza kuwa 'muhanga' wanapochinjwa au kuuawa kwa imani za kishirikina (tabia ya kuamini uwezo wa kiumbe kingine juu yako badala ya ule wa Mwenyezi Mungu). Siku hizi mauaji ya aina hii hufanywa sana humu nchini na watu wanaotaka utajiri!

Ingawa neno hili nimelitolea ufafanuzi mara nyingi bado latumiwa kwa maana potofu. Eti watu wanaokumbwa na mafuriko au wanaopatwa na ajali za aina mbalimbali huitwa 'wahanga' Hasha (sivyo kabisa)!

Mara nyingi watu husikika kwenye mikutano wakisema 'kwa niaba yangu.' Katika Kiswahili, mtu anayesema jambo linalomhusu huwa anaisemea nafsi yake. Kwa hiyo si sahihi kusema 'kwa niaba yangu'. Mtu anapotumwa, kuagizwa au kuwakilisha wengine kusema au kufanya jambo, ni sahihi kusema au kufanya 'kwa niaba' ya anaowawakilisha. Hapo anaweza kusema 'kwa niaba' ya familia yangu, wafanyakazi wenzangu, wananchi wa mtaa wangu au jimbo langu.

Ufisadi: Neno hili lina maana pana na linabeba maneno mengine yenye kunasibiana nalo. Kwa mfano, wizi, ujambazi, uzembe, ubadhirifu wa mali ya umma, ubakaji, uchukuaji wa wake au watoto wa watu, ukataji miti ovyo na mengineyo. Kwa ufupi, 'ufisadi' ni jambo linaloleta athari kwa mtu, jamii au nchi kwa namna yoyote ile.

Hivyo si sahihi na si busara kulielekeza zaidi neno hili katika ubadhirifu hasa wa mali ya umma. Kufanya hivi ni kugeuza matumizi ya neno hili katika matendo mengine kama hayo yaliyotajwa na pia kuyanyima haki maneno mengine kutumika ipasavyo katika mazingira mwafaka.

Mbele/mbeleni: Neno 'mbele' laweza kuwa maana ya siku au tarehe za usoni. Mfano: Tarehe ya uchaguzi imesogezwa mbele. 'Mbele' pia ina maana ya usoni mwa kitu au mtu, kama vile mbele ya macho, mbele ya watu.

Hata hivyo neno 'mbele' likiongezwa kipashio (sehemu ya neno yenye kazi maalumu ya kisarufi) 'ni' na kuwa 'mbeleni', basi kwa silika (tabia alizonazo mtu tangu alipozaliwa na kukua nazo) na adabu za Waswahili neno hilo hugeuka kuwa tusi, lenye maana ya sehemu za siri za mwanamke! Kwa hiyo maneno haya mawili si vibadala, kwani kila moja lina maana yake.

Nyumba ndogo: Maana halisi ya 'nyumba ndogo' ni nyumba rasmi na ya halali ya mke wa pili, wa tatu au wa nne aliyeolewa kisheria kwa ndoa ya Kiislamu. Hivyo 'nyumba ndogo' ni tofauti na mwanamke wa kinyumba. Mwanamke anapowekwa kinyumba huweza kuwa anahudumiwa kwa hali zote, lakini bado anakosa sifa ya kuwa mke wa aliyemweka na kumhudumia. Kuipa hadhi nyumba ya kimada au ya hawara na kuwa sawa na nyumba ya mwanamke aliyeolewa, kisheria ni kuhalalisha maasi!

Upungufu: Neno hili liko katika umoja, na kwa kawaida halina wingi. Upungufu katika jambo mara nyingi huelezwa kwa kukadiriwa kuliko kuhesabiwa. Mfano, taarifa iliyotolewa ina upungufu mkubwa na sio ina 'mapungufu makubwa.'

Kwa upande mwingine neno 'madhumuni' liko katika wingi, hivyo si sahihi kuliondolea kipashio 'ma' na kuliweka katika umoja kuwa 'dhumuni.' Tunasema madhumuni ya shughuli hii, madhumuni ya ziara yake na si 'dhumuni la' ziara yake n.k.

Husika: Sifa moja ya vitenzi vya Kiswahili ni kuchukua viambishi vya mtenda, wakati na mtendwa. Vipashio hivyo vina dhima (jukumu), maana na matumizi maalumu vinapotumika, kama vile kubainisha nafsi ya mtenda na mtendwa, ngeli, kuonesha umoja na wingi, na wakati wa kutokea tendo.

Kutumia neno husika bila kuliambatanisha na vipashio vyake vya mtenda, mtendwa na wakati ni kukiuka taratibu za sarufi ya lugha zilizokubalika bila ya kuwa na sababu za msingi.

Hafla/ghafla: Kitamkwa kimoja tu katika neno kinapotamkwa visivyo huweza kuleta tofauti (Wanzibari husema tafauti) ya maana ya neno au kupoteza maana yake halisi iliyokusudiwa. 'Hafla' na 'ghafla' ni maneno mawili yenye maana tofauti. 'Hafla' ni shughuli inayofanywa kusherehekea jambo maalumu. Mfano: 'Hafla ya kuwaaga wastaafu ilifana.'

'Ghafla' ni neno linaloeleza utokeaji wa jambo bila kutazamiwa. "Wageni walikuja ghafla bila ya taarifa."

**Methali: Enga kabla ya kujenga.**
**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mradi wapunguza mimba, ndoa za utotoni Shinyanga

## • Ni katika Kata ya Usanda, Shinyanga Vijijini
## • Waumini waacha kuhama makanisa

ELIMU hutajwa kuwa mwanga wa maisha ya binadamu, kwani humtoa katika ujinga na kumpatia maarifa ya namna ya kuishi maisha yaliyo na ubora, hivyo kuondokana na lindi la umaskini.

Mtu anapokuwa ana elimu walau ya ngazi ya chuo ni tarajio la wengi kwamba atakuwa na mchango mpana kwenye jamii.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba ujuzi anaokuwa ameupata unamuwezesha kuajiriwa katika sekta mbalimbali, lakini anaweza kuutumia ujuzi alioupata kujiajiri mwenyewe na hata kuajiri wengine.

Na hata kufanikisha mapambano dhidi ya maadui watatu wa enzi na enzi aliowatangaza Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, maradhi, umaskini na ujinga, kunahitaji watu walio na elimu.

Sasa pamoja na thamani ya elimu kufahamika, inashangaza kwamba bado kuna baadhi ya wazazi na walezi katika Mkoa wa Shinyanga wasiotambua umuhimu wa elimu.

Wazazi hawa wanadiriki kukatisha masomo ya watoto wao wa kike ili kuwaozesha kwa tamaa ya kupata mali au mifugo na hatimaye kuzima ndoto zao za baadaye.

Tatizo hilo linasababishwa na jamii katika mkoa huo kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo pamoja na mengine ya kutopenda kusomesha watoto wa kike kwa hofu kuwa akipata elimu atakwenda kunufaisha ukoo wa mume wake, huku wao wakiambulia hasara ya ada na gharama zingine walizoingia.

Sheria ya elimu ya mwaka 2009 inasema kila mtoto ana haki ya kupata elimu na wazazi ama walezi wana jukumu la kumhudumia mahitaji yake yote.

Sasa kwa baadhi ya wazazi au walezi katika mkoa huo ambao ni wakulima na wafugaji, sheria hiyo kwao wameipa kisogo kwa kutopenda kusomesha wanafunzi wa kike.

Kata ya Usanda katika Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga vijijini, ni miongoni mwa Kata mkoani Shinyanga ambazo zinakabiliwa na tatizo kubwa la wanafunzi kupewa ujauzito pamoja na kuolewa ndoa za utotoni.

Hilo linathibitishwa na utafiti uliofanywa na Shirika la Agape mkoani Shinyanga linaloendesha shughuli za kutetea haki za watoto na wanawake kwa kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

Mkurugenzi wa shirika hilo, John Myola, anasema mwaka 2016 walifanya utafiti kwenye Kata ya Usanda na wakabaini kuwapo kwa changamoto kubwa ya wanafunzi wa kike kukatishwa masomo yao, kwa sababu ya ujauzito na ndoa za utotoni.

Anasema baada ya kubaini changamoto hiyo, walizindua mradi wa elimu ya afya ya uzazi na jinsia kwa vijana wenye lengo la kutoa elimu kwa wanafunzi ili waache ngono katika umri mdogo na madhara yake kiafya.

Lakini mradi unalenga kuwaelimisha wazazi ili waache kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni.

"Tulianza kuutekeleza rasmi mwaka 2017, kwa ufadhili wa shirika Sida kupitia Save the Children ambao unamalizika mwaka huu 2019)," anasema na kuongeza...mradi unawahimiza wazazi wawekeze kwenye elimu ya watoto ambao watawasaidia wakishazeeka," anasema.



Mkurugenzi wa Shirika la Agape mkoani Shinyanga, John Myola (aliyesimama), akiwaasa wazazi wa Kata ya Usanda, Shinyanga vijijini, kuwekeza kwenye elimu ya watoto wao badala kuwakatisha masomo kwa lengo la kuwaozesha ndoa za utotoni. **PICHA: MARCO MADUHU**

Myola anabainisha kwamba uwekezaji kwenye elimu ya watoto bila ya ubaguzi una faida si kwa jamii na taifa kwa ujumla bali hata kwa mzazi mwenyewe.

"Kuna suala la uzee ambalo halitaakuwa shida kwa mzazi aliyewekeza kwa watoto wake kwani hatahangaika kwa sababu jeshi la watoto wake lipo kumsaidia," anasema.

### MASHUHUDA

Naomi Maige ni miongoni mwa mashuhuda wanufaika wa kuwekeza kwenye elimu ya watoto.

Naomi ambaye ni mkazi wa Shinyanga anasema sasa hivi hana nguvu tena za kufanya kazi kutokana na uzee huku akisumbuliwa na maradhi.

"Watoto wangu ndiyo wanashikilia maisha yangu kwa sasa kwani wamekuwa wakinitumia fedha za chakula na wamenikatia bima ya afya NHIF kwa ajili ya matibabu," anasema na kuongeza:

"Mume wangu alifariki miaka mingi iliyopita akaniachia watoto watatu wakiwa wadogo, lakini nilipambana ili kuhakikisha wanapata elimu, kwa kuwa nilijua kwamba ndio mkombozi wa maisha yao na ya kwangu pia... ilifikia hatua nikauza hadi kiwanja lakini leo wamenijengea nyumba na ndio wananitunza."anasema.

Anashauri wazazi kusomesha watoto wao na kuacha kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo sana sana zinatumbukiza kwenye umaskini.

### MZEE WA KIMILA

Mzee wa kimila kutoka Kata hiyo ya Usanda, Shija Kulwa, anasema sasa wakazi wa kata hiyo wanafunguka macho baada ya kupata elimu ya afya ya uzazi na jinsia kupitia mradi huo.

"Wengi sasa wanatambua umuhimu wa elimu na wanaacha kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni,"anasema.

Anabainisha kwamba katika mila za Kisukuma ilikuwa hakuna kusomesha mtoto wa kike kwa sababu akipata elimu na kazi nzuri atakwenda kunufaisha ukoo wa mumewe.

"Hivyo ilikuwa mtoto akianza kuonekana tu ameiva tayari anatafutiwa mume na kuozeshwa... haijalishi hata kama ana soma," anasema na kuongeza:

"Kama wazee wa kimila tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia kwenye mikutano mbalimbali tukisisitiza tuachane na mila na desturi zilizopitwa na wakati, tusomeshe watoto wetu watakaokuja kutusaidia tutakapozeeka."

### MWENYEKITI

Daudi Michaeli ni mwenyekiti wa kitongoji cha Manyada, Kata ya Usanda Shinyanga vijijini.

Anasema katika kumpigania mtoto wa kike kielimu, wameshapiga marufuku wanafunzi wa kike kucheza shoo kwenye harusi na sherehe ambazo zilikuwa zinachochea vishawishi vya wanafunzi kutongozwa na hatimaye kupata mimba, hivyo kuacha shule.

### MCHUNGAJI

Kwa upande wake, Mchungaji wa Kanisa la (AICT) kwenye Kata hiyo Lameck Makungu, anasema wao kama viongozi wa dini walikuwa wakikabiliwa na wakati mgumu kila walipohimiza wananchi kuachana na mila potofu za kuozesha watoto wao wadogo badala ya kuwasomesha.

"Tulikuwa tukiingizwa kwenye mitego ya kufungisha ndoa hizi za utotoni na tunapogoma basi familia husika inahama kusali kwenye kanisa letu na kwenda dhehebu jingine," anasema na kuongeza:

"Lakini sasa baada ya wananchi kutambua umuhimu wa kusomesha watoto bila ya kuwabagua na sisi wachungaji tunapoendelea kuhubiri na kukemea ndoa hizi za utotoni, waumini wanaelewa na hakuna tena hamahama ya madhehebu."

### OFISA MAENDELEO

Ofisa Maendeleo wa Kata hiyo, Halima Tendega, anasema miaka ya nyuma, Kata ilikuwa ikiongoza kwa utoro na mimba za wanafunzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga vijijini, lakini sasa hali inapungua kufuatia mradi wa Agape.

Akitoa takwimu za hali ya mimba za utotoni, Mratibu wa Elimu wa Kata hiyo, Sospeter Kasonta anasema mwaka 2016, wanafunzi 21 walipata mimba, mwaka 2017 walikuwa 16, mwaka 2018 wanafunzi wanne walipata mimba na kuanzia kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu ni mwanafunzi mmoja ndiye ambaye amepata mimba.

"Napongeza mashirika yasiyo ya kiserikali kwani yamekuwa na msaada mkubwa ndani ya jamii kwa kubadilisha mitazamo potofu... sasa hivi hata utoro shuleni kwa wanafunzi wa kike umepungua tofauti na zamani, na nina imani hata ufaulu utaongezeka kwa wasichana," anasema Kasonta na kuongeza:

"Mkakati ambao nataka kuufanya kwenye Kata hii ya Usanda ni kufungua kituo cha vijana (Vijana Center), ambacho kitakuwa kinakutanisha vijana na kupeana elimu ya maisha juu ya namna ya kufikia malengo yao, na kuacha ngono zembe ili kuchochea ukuaji wa elimu."

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo Emmanuel Maduhu, anasema wao kama viongozi wa Serikali kwenye Kata hiyo kwa kushirikiana na wenyeviti wa vitongoji pamoja na diwani wamekubaliana moja ya ajenda iwe ni kutoa elimu ya kutokomeza ukatili zikiwamo mimba na ndoa za utotoni.

"Kauli mbiu yetu inasema 'Usanda Ukatili Sasa Basi'...hatutaki turudi nyuma tulikotoka...tunaka jamii yetu iishi salama, bila mimba wala ndoa za utotoni...wazazi wasomeshe watoto wao ambao watakuja kuwa tegemeo la familia na taifa," anasema Maduhu.

## TEKNOLOJIA

**NOVATUS MAKUNGA, MANYARA**

# Simanjiro katika Tanzania ya viwanda

• Yazindua chuo cha VETA kupika wataalamu wa fani mbalimbali •Inaanza na fani ya uashi

ILIKUWA nadra sana katika miaka ya nyuma kukuta vijana wa jamii ya wafugaji wa kabila la Wamaasai wakichangamkia fursa za kujiunga na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi.

Hii ilitokana na mila na desturi ya jamii hiyo kwani tangu mtoto anapozaliwa alikuwa akilelewa katika misingi ya maisha yanayoendeshwa kwa kutegemea uchumi wa ufugaji mifugo, kwa maana ya kuchunga ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Mfumo huo wa maisha ulishazoeleka na kila kijana katika maeneo ya jamii ya wafugaji akishavuka rika fulani, akahitimu elimu ya msingi bila ya kupata fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari, moja kwa moja huingia katika shughuli za ufugaji.

Hata hivyo sasa hali hiyo imekuwa tofauti, jamii hiyo imeingia katika mageuzi kwa kasi kubwa na ndicho kilichoshuhudiwa katika Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara hivi karibuni.

Jamii yenyewe imejiongeza na kuchagua kipaumbele cha kujengewa chuo kitakachotoa mafunzo kwa vijana wao ili wawe na utaalamu wa nyanja mbalimbali za ufundi stadi.

Mageuzi hayo katika Wilaya ya Simanjiro na wilaya jirani ya Kiteto zote zikiwa katika Mkoa wa Manyara yameshuhudia vijana 24 wakianza mafunzo ya ufundi uashi mapema katika chuo hicho kilicho Kata ya Emboret.

Hatua hiyo imekuja baada ya kukamilika kwa chuo pekee cha ufundi katika wilaya hizo kilichojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 531.

Kinatarajiwa kuzinduliwa rasmi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Oktoba 19 mwaka huu.

Kimejengwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la ECLAT Development Foundation kwa ufadhili wa shirika la Upendo Society la Ujerumani, na tayari kimeshakabidhiwa kwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Nchini (VETA).



Mwenyekiti wa ECLAT, Peter Toima(kushoto) na Mwenyekiti wa Shirika la Upendo Society la Ujerumani, Dkt. Fred Heimbach (kulia) wakitoa maelekezo kwa msimamizi wa miradi inayotekelezwa na mashirika hayo, Masham Bakiri(katikati)



Mkufunzi wa chuo cha ufundi VETA Simanjiro, David Mrutu, akikagua vifaa vya kufundishia ufundi uashi katika chuo hicho

**DIWANI**

Diwani wa Kata ya Emboret, Christopher Kuya, anasema chuo hicho kitawakomboa vijana wengi wanaozurura mitaani kutokana na kukosa fursa ya kuendelea na elimu ya juu baada ya kuhitimu elimu ya msingi na kidato cha nne.

Kuya anabainisha kwamba kwa kuhitimu katika fani mbalimbali za ufundi, kutawawezesha kujiajiri, pia kuajiriwa kama mafundi wa ngazi ya kati ambao wanahitajika katika mwelekeo wa serikali ya sasa ya Tanzania ya viwanda.

Anasema kwamba kwa hivi sasa katika maeneo ya Umasaini kuna kasi ya ujenzi wa nyumba za kisasa na ununuzi wa pikipiki maarufu kama bodaboda, hivyo mafundi wengi wanahitajika.

Kitawanufaisha vijana wa Wilaya za Simanjiro na Kiteto, miongoni mwa wilaya sita za mkoa wa Manyara ambazo hazikuwa na chuo chochote cha ufundi, kikihudumiwa na VETA Kanda ya Kati, inayojumuisha vilevile mikoa ya Singida na Dodoma.

Huo ni mwendelezo wa Serikali iliyozindua mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2012/2013 hadi 2016/2017 unaoazimia kujenga vyuo vya ufundi stadi katika kila wilaya nchini. Tanzania ina wilaya 169 na mikoa 32.

Hatahivyo kazi ya utekelezaji wa azimio hilo ulionekana kusuasua kutokana na kasi ndogo ya ujenzi wa vyuo hivyo na hivyo kuwaacha maelfu ya vijana wakikosa nafasi za kujiunga na vyuo vya VETA.

**PROFESA NDALICHAKO**

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako wakati akizindua Chuo cha Ufundi stadi cha Wilaya ya Urambo mkoani Tabora hivi karibuni serikali imetenga Sh. bilioni 40 kwa ajili ya kujenga vyuo 25 kwenye wilaya mbalimbali mwaka huu wa fedha wa 2019/2020.

Anabainisha kwamba lengo ni kuhakikisha vijana wengi zaidi wanapata fursa ya mafunzo ya ufundi stadi ili kuendana na kasi na maono ya serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa viwanda.

Anasema ujenzi wa vyuo vya mikoa unaendelea Geita na Rukwa huku ujenzi wa vyuo vya Simiyu, Kagera na Njombe ukitarajiwa kuanza muda mfupi ujao.

**MRATIBU WA KANDA**

Mratibu wa VETA Kanda ya Kati, Abdulkadiri Yussuf, anasema wameamua chuo hicho cha Simanjiro kianze na mafunzo ya fani ya uashi kutokana na mahitaji ya mafundi ujenzi katika wilaya hizo.

"Kuna kasi kubwa ya ujenzi wa nyumba katika Wilaya ya Simanjiro lakini changamoto kubwa ni ya mafundi... wengi kwa hivi sasa wanatoka jijini Arusha kuja kujenga nyumba hapa," anasema.

Yussuf anasema katika awamu ya pili ya chuo hicho, ndipo kutaanzishwa fani zingine zinazoendana na ujenzi wa majengo yakiwamo ya shule, zahanati na vituo vya afya pamoja na maghala.

"Tutaanzisha fani za ufundi seremala, umeme na bomba katika awamu hiyo...Aidha kwa kuwa jamii hii pia imeanza kujiingiza katika kilimo, tutaanzisha mafunzo ya ufundi wa zana na mitambo ya kilimo," anasema na kuongeza:

"Zana kama vile matrekta na mashine za kupukuchua mazao,majembe ya kukokotwa na wanyama pamoja na mashine za kukoboa nafaka."

Anasema kutokana na mahitaji ya nguo kuwa bayana katika maeneo hayo kama ilivyo kwa sehemu zingine nchini, wataanzisha vilevile ufundi wa ushonaji wa nguo.

"Kikikamilika chuo kitakuwa kinachukua wanafunzi 250," anasema na kuongeza:

Anasema kwa mwaka huu wa fedha, wameshatenga Sh. milioni 81 kwa ajili ya kujenga bweni jingine litakalokuwa na uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 24.

**MWENYEKITI ECLAT**

Mwenyekiti wa shirika la ECLAT ambaye pia ni mzaliwa wa Wilaya ya Simanjiro, Peter Toima, amefafanua kwanini waliamua k u j e n g a

**Inaendelea Uk. 18**

## JIELIMISHE

### KAMPUNI YA NEURALINK YAINGIZA TEKNOLOJIA YA UDUKUZI WA UBONGO

KAMPUNI ya N e u r a L i n k , iliyoanzishwa na Elon Musk ili kutafuta mbinu za kuunganisha ubongo wa binadamu na tarakilishi, imewasilisha ombi kwa mamlaka za udhibiti nchini Marekani la kuanza kupima mfumo wa kifaa chake miongoni mwa binadamu.

Mfumo huo umejaribiwa kwa tumbili ambaye aliweza kudhibiti tarakilishi na ubongo wake kwa mujibu wa Musk.

Lengo la kampuni hiyo ni kutafuta mbinu za kuchochea ubongo wa binadamu aliye-pooza kumwezesha kudhibiti tarakilishi.

Kampuni hiyo ilikuwa inalenga kuangazia wagonjwa wenye matatizo ya uti wa mgongo, neva na ubongo miongoni mwa binadamu.

Hatahivyo, lengo la Musk ni kudukua ubongo wa binadamu kupitia tarakilishi.

MFUMO ULIVYO

Mfumo ambao kampuni imeutengeneza una kifaa kidogo kinachoweza kuchun-guza, chenye electrodes zaidi ya 3,000 zilizounganishwa na nyuzi zinazoweza kubadilika.

Nyuzi hizo ni nyembamba kuliko nywele za binadamu na zinaweza kufuatilia shughuli za neuroni 1,000.

Umuhimu wa mfumo huo, ni kutokana na kulenga maeneo fulani katika ubongo, hatua inayofanya upasuaji kuwa salama kwa mujibu wa kam-puni hiyo.

Pia kinaweza kutath-mini yaliyorekodiwa kupitia mashine ambayo itaamua ni aina gani ya matibabu atakay-opewa mgonjwa.

Hata hivyo, Neuralink haikutoa maelezo jinsi mfumo huo unavyoweza kubadilisha vitendo vya ubongo ama jinsi kifaa hicho kinavyoweza kuchochea seli za ubongo.



Kifaa kinachodhibiti tarakilishi na ubongo wa binadamu kutoka kampuni ya NeuraLink.**PICHA: MTANDAO**

"Si kwamba tayari tutakuwa tuna uwezo wa kushiriki-sha ubongo wa binadamu katika tarakilishi na kuchukua udhibiti wa bongo zao," anasema Musk na kuongeza:

"Kitu hiki kitachukua muda mrefu, lakini wale watakao-taka kutumia mfumo huo, uta-saidiana na ule wa tarakilishi."

Awali Musk alisema kuwa intelijensia ya mashine hiyo inaweza kuharibu jamii ya binadamu.

Aidha, uunganishaji wa ubongo na tarakilishi utaima-risha zaidi ubongo wa bin-adamu.

"Tayari watu wamekuwa wakifurahia hilo kupitia simu zao kwa maana ya jinsi wanasayansi wanavyolenga kudukua ubongo wa binada-mu," anasema.

VIPIMO

Musk alifichua kwamba kifaa hicho cha Neuralink kinafanya kazi na kwamba tayari kimefanyiwa vipimo kwa tumbili ambapo mnyama huyo aliweza kudhibiti tarak-ilishi na ubongo wake.

Sasa kampuni hiyo im-ewasilisha ombi la kutaka kuufanyia majaribio mfumo huo kwa binadamu ambapo ruhusa hiyo inabidi na kitengo cha usimamizi wa chakula na dawa nchini Marekani.

Aidha, Musk analenga kuajiri mwanasayansi mmoja zaidi katika kampuni hiyo ambayo kufikia sasa inaendeshwa na wafanyakazi 100.

Hata hivyo, kampuni hiyo inasema itachukua miaka mingi ya kazi kufanywa ili kukabiliana na changamoto za kiteknolojia pamoja na kimaadili ili mfumo huo utumike.

Pamoja na hayo, teknolojia hiyo huenda ikawa ni hatua kubwa katika kukabiliana na matatizo sugu ya kiafya kama vile ugonjwa wa kifafa na ule wa kutetemeka.

MIRADI MINGINE

Musk amekuwa na miradi mingi inayojaribu kufanya yale yanayowezekana.

Mojawapo ya miradi yake ni wa Space X unalenga kuanzi-sha utalii wa kuelekea katika sayari ya Mars.

Mradi mwingine ni ule unaofanywa na kampuni ya Boring inayojaribu kujenga mahandaki chini ya mji wa Los Angeles nchini Marekani.

**BBC**

# Simanjiro katika Tanzania ya v

Inatoka Uk. 17

chuo hicho cha ufundi.

"Tuliamua kujikita katika ujenzi wa Chuo hiki kwa lengo la kuunga mkono mpango wa serikali wa kujenga vyuo vya ufundi stadi kwa kila wilaya, huku tukizingatia kipaumbele cha wananchi wenyewe wa Simanjiro," anasema.

Toima ambaye amewahi kushika nafasi za ukuu wa wilaya katika wilaya za Tunduru mkoani Ruvuma, Rombo mkoani Kilimanjaro na Kakonko mkoani Kigoma anasema lilikuwa wazo la wananchi wenyewe wa Simanjiro.

"Hiyo ni baada ya kuona umuhimu wa kuwa na vijana wenye maarifa kutokana na ukweli kwamba dunia inakwenda kwa kasi sasa hivi katika uga wa sayansi na teknolojia," anasema na kuongeza:

"Tayari kulikuwa na eneo la ekari 100 likiwa na majengo mawili yaliyotelekezwa na hivyo katika awamu hiyo ya kwanza tumetumia Sh. milioni 531 inayohusisha ujenzi wa madarasa, bweni moja, jiko, vyoo, kisima kirefu cha maji, umeme wa nishati ya jua na vifaa vya kufundishia uashi."

**SHIRIKA LA UPENDO**

Mwenyekiti wa shirika la Upendo la Ujerumani ambao ndio wafadhili wa mradi huo, Dk. Fred Heimbach akizungumza na wanafunzi katika siku yao ya kwanza ya masomo anawaasa kusoma kwa bidii.

"Ninawaasa hivyo kwa sababu mmepata fursa ambayo inawahakikishia ajira na baadaye muweze kuendesha maisha yenu," anasema.

**MKUU WA WILAYA**

Mkuu wa wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula anatoa wito kwa vijana wa kike na kiume kuchangamkia fursa hiyo ya mafunzo ya ufundi kwa lengo la kujikomboa kiuchumi.

Anasema kuwepo kwa nafasi kama hizo kutapunguza hata tabia ya vijana wa jamii ya Kimasai kutimkia mijini kwa lengo la

## JE, WAJUA?




Maliha Mohammed akiwa katika shughuli za upishi zilizomfanya avunje rekodi.**PICHA: MTANDAO**

# Mkenya avunja rekodi ya dunia kwa kupika

• Aingia kwenye kitabu cha Guiness

MALIHA Mohammed, mpishi maarufu kutoka Mombasa nchini Kenya, amevunja rekodi ya dunia ya kitabu cha Guiness kwa kupika kwa muda mrefu zaidi.

Mwanamke huyo amekuwa mtu wa kwanza kuvunja rekodi hiyo barani Afrika.

Maliha alipika kwa muda wa saa 75 bila kuchoka na hivyo kuvunja rekodi ya dunia Jumapili iliyopita katika hoteli ya kitalii ya Bay Beach mjini Mombasa.

Muda mrefu zaidi kuwahi kufikiwa ulikuwa ni wa saa 68 dakika 30 na sekunde moja, na ulivunjwa na Rickey Lumpkin mjini Los Angeles, Marekani mwaka 2018.

Mwanamke huyo mwenye umri wa miaka 36 alikuwa ameandaa mapishi 400 ya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya mashindano hayo ili kuweka jina lake katika kitabu hicho cha rekodi za dunia cha Guiness.

Vyakula alivyoandaa vitatolewa kwenye nyumba za hisani na zile za yatima kama mojawapo ya kutoa hamasa na kuwasaidia wasiojiweza mjini Mombasa.

Katika jaribio lake la kwanza mwezi Mei mwaka huu, mama huyo wa watoto wawili alipika vyakula 100 katika muda wa saa 36 bila kuchoka.

Baadaye mwezi Julai, mpishi huyo alipika vyakula 200 kwa saa 54 kabla ya kuelekea katika fainali iliyosimamiwa na maofisa wa kitabu cha rekodi za dunia za Guiness.

Akisaidiwa na takriban watu 40 waliokuwa wakifanya kazi kwa zamu, Maliha alikuwa ameonyesha matumaini ya kushinda rekodi hiyo awali.

Anasema, juhudi zake za kushindana mwaka 2018 zilishindwa, kutokana na matatizo ya kifedha.

Kitabu cha rekodi za dunia cha Guinness huchapishwa kila mwaka, kikiorodhesha rekodi za dunia zilizovunjwa na binadamu.

"Niliwasilisha ombi langu mwezi Desemba mwaka jana kwa wasimamzi wa kitabu hicho na wakajibu Aprili mwaka huu kwamba ombi langu la saa 75 lilikubaliwa," anasema.

Maliha alifadhiliwa na kampuni ya mafuta ya kupikia ya Pwani Oil Products Limited, ambayo ilimsaidia kwa kumpatia mafuta na vitu vingine vinavyohitajika katika mapishi, huku wahisani wengine wakisaidia jiko la kupikia.

"Mwaka uliopita nilipojiondoa kwenye mashindano, sikuvunjika moyo. Kupitia fedha kidogo nilizokuwa nimechangisha, niliamua kubadilisha sebule yangu kuwa jiko na nikiwa na rafiki zangu 20, tulipika kwa zaidi ya saa 72 bila kuchoka," anasema.

**JE MSUKUMO WAKE UNATOKA WAPI?**

Maliha anasema kwamba alipata msukumo wa kuingia katika shindano hilo kama njia ya kuisaidia jamii.

Aliyekuwa akishikilia rekodi hiyo Rickey alijaribu kuvunja rekodi hiyo ili kuchangisha fedha kuwafadhili watoto kupitia shirika lisilo la serikali la World Vision.

"Nikiwa na miaka 36, nataka kuwa mfano wa kuigwa na wasichana na jamii katika eneo ninalotoka,"anasema. **BBC**

# UTAFITI

## JE, VINYWAJI VYA SUKARI HUSABABISHA SARATANI?

VINYWAJI vya sukari yakiwemo maji ya matunda vinaweza kuongeza hatari ya saratani, kwa mujibu wa wanasayansi wa Ufaransa.

Uhusiano huo unafichuliwa na utafiti uliochapishwa katika jarida la matibabu nchini Uingereza ambao uliwachunguza watu 100,000 kwa kipindi cha miaka mitano.

Wanasayansi hao kutoka Chuo Kikuu cha Srbonne Paris Cite, wanadai kwamba ongezeko la viwango vya sukari katika damu, huenda ndio sababu kuu.

Hatahivyo, utafiti haukupata ushahidi kamili na kwamba watafiti wametaka kazi zaidi kufanywa.

**KINACHOHESABIKA KAMA KINYWAJI CHA SUKARI**

Watafiti wanasema kinywaji chochote kilicho na zaidi ya asilimia 5 ya sukari kinahesabika kama cha sukari. Vinywaji hivyo vinajumuisha maji ya matunda ambayo hayajaongezwa sukari, Pia vinywaji visivyo na pombe, vinywaji vya kuongeza nguvu, chai na kahawa yenye sukari.

Aidha, watafiti hao walichunguza vinywaji visivyo na kalori, vinywaji vilivyo na sukari yake lakini hawakubaini uhusiano wowote na saratani.

**JE HATARI YA SARATANI NI YA KIWANGO GANI ?**

Utafiti ulifichua kwamba unywaji wa mililita 100 za ziada za vinywaji vilivyo na sukari kwa siku na chupa mbili kwa wiki kutaongeza hatari ya saratani kwa asilimia 18.

Kwa kila watu 100 katika utafiti huo, kuna 22 wenye saratani.

Hivyo basi iwapo wote watakunywa mililita 100 kwa siku, itasababisha aina nyingine nne za saratani na kuongeza jumla hiyo kufikia 26 kwa 1000 katika kipindi cha miaka mitano, kulingana na watafiti.

Kati ya visa 2,193 vilivyopatikana wakati wa utafiti huo, aina ya saratani 693 zilikuwa zile za matiti, 291 zilikuwa za tezi dume na visa 166 vilikuwa vya saratani ya mwisho wa utumbo.

**JE HILI NDIO THIBITISHO KAMILI?**

Hapana...jinsi utafiti ulivyofanyika inamaanisha unaweza kupata mifano katika data, lakini hauwezi kuelezea.

Hivyo, unaonyesha kwamba watu waliokunywa sana takriban mililita 185 kwa siku, ndio walikuwa na visa vingi vya saratani ikilinganishwa na wale waliokunywa chini ya mililita 30 kwa siku. Maelezo yanabainisha kuwa vinywaji vya sukari vinasababisha saratani lakini pia watu wanaobugia vinywaji vya sukari wanaweza kuwa na matatizo mengine ya kiafya.

Kutokana na maelezo hayo Dk. Amelia Lake kutoka Chuo Kikuu cha Teesside anasema kwamba utafiti huo hauwezi kuhitimisha kuwa vinywaji vya sukari ndio chanzo cha saratani.

"Wakati utafiti huo ukishindwa kutoa ushahidi kamili kuhusu sukari na saratani, unaonyesha mpango uliopo wa kupunguza kiwango cha sukari," anasema na kuongeza.

"Pamoja na hayo, kupunguza kiwango cha sukari katika chakula ni suala muhimu sana."

**JE UNENE UNAHUSIKA KWENYE SARATANI?**

Kunenepa kupita kiasi ni sababu mojawapo inayosababisha saratani, na matumizi ya juu ya vinywaji vya sukari husababisha mtu kunenepa. Hatahivyo, utafiti unasema si visa vyote.

"Kunenepa kupita kiasi kunakosababishwa na kunywa vinywaji vingi vya sukari kunahusishwa na saratani, lakini uhusiano wote haukuelezwa kwa kina," anasema Dk. Mathilde Touvier, mmoja wa watafiti.

# viwanda

kutafuta kazi za ulinzi.

Kanda ya Kati ya VETA ina vyuo vinne katika Wilaya ya Babati mkoa wa Manyara, Singida na Dodoma pamoja na hicho cha Simanjiro.

Aidha, chuo kingine kinaendelea kujengwa Babati.

Kwa mujibu wa mratibu wa VETA wa kanda hiyo, kuna vijana 2,178 wanaochukua mafunzo ya ufundi.



Baadhi ya madarasa ya chuo cha VETA Simanjiro

## UCHAMBUZI WA KITABU;

# Embracing Life after Loss (Maisha baada ya kuondokewa)

**Na Allen Klein**

MAISHA ni zawadi pale ambapo watu huendelea kuishi. Ila wanapoondoka na kuwa mbali nasi kwa njia ya kifo na kutokuwa na matumaini ya kuwaona tena, ndipo maisha hugeuka na kuonekana ni mateso na maumivu yasoweza kuelezeka.

Ila kupoteza watu wetu wa karibu ni jambo lisiloweza kukwepeka maishani. Maana hata sisi siku moja tutaondoka na kuwaacha watu wengine.

Si kitu rahisi kukabiliana na hali za kuondokewa na wapendwa wetu katika maisha. Huumiza na wakati mwingine hufanya tuone maisha hayana huruma na sisi.

Licha ya haya yote, ukweli bado utabaki kuwa hali ya kupoteza watu wetu wa karibu itaendelea kuwapo maana ni sehemu ya maisha kamilifu.

Mwandishi wa kitabu hiki anajaribu kutushirikisha namna maisha ya kuondokewa tunavyoweza kukabiliana nayo.

Kuanzia hatua ya mshituko wa habari za kuondokewa, kujifunza kutokana na kuondokewa, kuishi baada ya kuondokewa na watu wetu wa karibu na mwisho kufurahia maisha ambayo bado yataendelea baada ya watu wetu wa karibu muda wao wa kuishi kimwili kwisha.

Ni kitabu cha mwongozo mzuri sana katika kuturudisha kuyaona maisha kwa kina na kushukuru nafasi ambayo inakuwepo ya kuishi na watu wetu wa karibu kabla siku hawajatutoka.


Mshituko ni hali ya kawaida inayotokea pale unaposikia mtu unayemfahamu au mpendwa wako amefariki. Lakini wakati huu unavyotokea unatukumbusha namna ilivyo kwamba maisha ni mafupi na watu hawadumu milele.

Wakati kama huu wengine hujiuliza kwanini mimi hili limenitokea. Ni maswali mazito ambayo watu hujiuliza kuona namna kuondokewa kumewajeruhi sana ndani yao.

Mwandishi anasema wakati kama huu ni muhimu kujikumbusha kuwa maisha ni mafupi na nafasi kwetu kuangalia jinsi tuishivyo na kuongeza uzito kuwajali na kuwapenda watu wengine walobakia.

Watu wanapoondoka na kutuacha ni dhahiri kumbukumbu zao ndizo hutuumiza sana kiasi kwamba tunatamani saa zingerudi nyuma, tuseme nao jambo au kufurahi pamoja.

Kwa kuwa wengi hatujui ni wakati gani wa watu kuondoka, inakuwa ngumu kuona jambo hili la kuondokewa kuwa ni la kujifunza na kutafakari maisha yetu yalipo na nini sisi tunavyojiandaa kukikabili kifo kitapobisha hodi maishani mwetu.




Katika hili, linapotokea huturejeshea kumbukumbu zao za maisha itupayo kuona maisha ni alama tu inayobaki mtu akishakufa.

Hali za kuondokewa zinapoangaliwa kwa jicho pana ndizo ambazo hutupa mwanzo mpya katika maisha. Hizi hali ndizo ambazo zinatufungua na kutuzindua tuwe na tathimini kubwa juu ya maana ya maisha.

Hizi ndizo nyakati ambazo zinamfanya mtu aimarike na kuona maisha kwa sura ya mabadiliko mapya ambayo huja kila mara ambapo kitu au mtu kuwa mbali nasi kimwili.

Kama ilivyo ngumu kujaza kitu katika chombo kilichojazwa ndivyo suala la kuondokewa liwapo na uwazi wa kufungua kurasa mpya za maisha, fursa mpya na kuumba mtizamo mpya.

Si jambo rahisi kuzoea pale ambapo hali za kuondokewa zibishapo hodi ndani ya mtu.

Maisha huendelea mbele licha ya kujawa na kuondokewa na watu wetu wa karibu. Hivyo kuendelea kuumia kwa kuondokewa ni kupoteza muda wa kuyatafakari maisha yako ya sasa.

Kweli ni hali inayoumiza lakini muda na kikomo cha kutafakari thamani ya maisha yako nayo ni muhimu kufikiriwa kwa uzito.

Samehe na kumbuka nafasi nzuri ambazo ukumbukazo za namna mliishi na mtu huyo ambaye kwa sasa hayupo tena na wewe. Kwa kukumbuka namna maisha yako yalikuwa bora, namna yeye angeendelea kuishi angetamani ufanikiwe basi unajipa matumaini ya kuendelea mbele na kuyafurahia maisha kama wengine walopitiwa yafananayo na hayo.

Mwandishi anasema tunapokuwa katika hali ya kuondokewa, tukumbuke kuwa sisi si wa kwanza kupitia hizo hali, kuna watu wengi wamepitia na wamepoteza watu wao kwa namna nyingi.

Kuukubali ukweli huu kuwa kuondokewa ni sehemu ya maisha, kunatengeneza umakini na kuchukulia uzito wa maisha kama zawadi.

Pale ambapo watu huchukulia uzito maisha ndipo ambavyo huthamini watu wanaowazunguka wakijua kuwa si wakati wote tutaendelea kuwa nao.

Kushukuru kwa zawadi ya kuwa hai na kuthamini wengine ni himizo la mwandishi ambalo anasema tulione kwa uzito.

Tuone nafasi ya kuwajali wengine wakiwa hai, tufurahie maisha pamoja nao na kuwa tayari kuishi kitoshelevu.

Kuishi kitoshelevu ni pamoja na kuishi kwa kutambua maisha yetu ni mafupi sana na wakati wowote ule tunaweza kuyapoteza au kuwapoteza watu ambao wanatuzunguka.

Maisha ni zawadi yape uzito siku zote. Furahia na wanaokuzunguka na waonyeshe upendo maana siku moja hutapata nafasi kama hiyo kuifanya kwao.


Ukiwa na maswali, maoni au jambo ungetamani kulijua kwa kina kupitia uchambuzi huu, basi usisite kuniandikia kupitia barua pepe.

***Mchambuzi ni Dk. Raymond Nusura Mgeni anapatikana kupitia raymondpoet@yahoo.com +255 676 559 211. Dar-es-Salaam***




# WADAU SABATO KASIKA

**KABLA ya wanafunzi kujiunga na sekondari huwa kuna fomu zinazoainisha taratibu za shule ikiwamo rangi za sare na mishono, lakini baadhi yao hushona wanavyotaka wenyewe. Wadau wanasemaje?**



**GODFREY RUTAZAA (MWANAFUNZI WA MWAKA WA TATU CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM)**

SABABU kubwa ya yote haya ni kuiga tabia za wanafunzi walio katika madarasa ya juu kama kidato cha tatu, cha nne na kuendelea, ambao wengi wao ndio huwa mstari wa mbele kwenda kinyume na sheria zilizoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule (Joining instruction), hasa kwa sababu wanakuwa wameshaizoea shule, hivyo kutofuata tena sheria za shule. Vile vile athari za utandawazi na maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyokuja na uvumbuzi wa vitu vipya na kufanya dunia kuwa kama kijiji kwa maana ya kuwapo kwa mitandao ya kijamii kama vile instagram na facebook. Hivyo baadhi ya wanafunzi huiga aina ya mavazi wanayovaa watu maarufu au wasanii mfano nguo fupi na suruali za kubana (modo), hadi wanafunzi kutumia aina hii ya mavazi hata kwenye sare za shule. Pia aina ya malezi ya wanayopata kutoka katika familia zao na watu wanaowazunguka au mazingira anayotoka mwanafunzi husika. Mfano kama mwanafunzi anatoka kwenye mazingira ambayo wakazi wengi aina yao ya mavazi ni nguo fupi au hata wazazi husika wanavaa aina ya mavazi kama hayo, ni rahisi kwa mtoto naye kufuata nyendo za wazazi wake. Cha kufanya ili kumaliza tatizo hili ni wazazi kutimiza wajibu wao wa malezi bora kwa watoto, kwa kuwa mfano bora kwa watoto wao ikijumuisha mienendo yao ya aina ya mavazi na namna ambavyo wanaendesha familia zao. Sambamba na hilo wazazi wanapaswa kuwa karibu na watoto wao kwa maana ya kuwafuatilia kwa ukaribu ili kujua mienendo yao shuleni na hata nyumbani. Hii itasaidia kujua tabia zao na kuwarekebisha watakapogundua kuwa tabia na mienendo si ya kuridhisha.



**BRIDGETER PILLA (HAKIMU MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO TEMEKE)**

TATIZO ni kwamba watoto wetu wanapenda sana kuiga kila kitu hata mabaya. Hii inatokana na utandawazi kwani umechangia yote haya. Watoto wengi wanaiga kwa kuangalia mitandao ya kijamii. Kwa mfano watoto wananunuliwa simu wakiwa bado wanafunzi, hivyo huiga mambo yanayokinzana na tabia nzuri ya mtoto. Wakati mwingine kiburi cha mtoto kinasababisha akaidi maelekezo ya wazazi au walezi wake. Hebu fikiria, mzazi ameingia gharama kushona sare za shule kwa ajili ya mtoto wake, halafu mtoto huyo huyo anakwenda kwa fundi kubadili mshono wa sare za shule! Ninashauri wazazi wawe karibu na watoto wao, kukagua mavazi yao kama walivyoshonewa ndivyo yalivyo. Kwa njia hiyo itakuwa ni rahisi kuwabana watoto wakorofi, vinginevyo wataharibika.




**MAIKA MAPUNDA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA tatizo hili wazazi hatuwezi kujitetea kutokana na ukweli kwamba wanatoka nyumbani kwenda shuleni, tunawaona wanavyovaa, sasa kama watakuwa wanavaa vibaya halafu hatuwakemei, maana yake ni kwamba tumewaruhusu wafanye hivyo. Mfano mmojawapo ni huo wa sare za shule, mzazi umenunua kitambaa umeshona kulingana na maelekezo ya shule, halafu mtoto anakwenda kwa fundi kubadili mshono bila wewe kuchukua hatua. Hii ni sawa na kwamba umeruhusu, na ndipo utakuta mwanao anavaa suruali imeshuka chini ya makalio, huku wa kike amebana sketi ya shule. Hebu wazazi pamoja na kwamba tuna shughuli nyingi, bado kuna haja ya kutenga muda kwa ajili ya malezi, tusiachie jukumu hilo walimu, matokeo yake ni watoto kuvaa 'vimodo' na vimini bila kukemewa. Yaani unakuta baadhi ya wanafunzi wanavaa mlegezo huku wengine wakibana sketi, halafu wanatoka kwa wazazi wao kwenda shule. Inashangaza sana. Wakumbuke hakuna shule isiyokuwa na utaratibu na sheria. Ndiyo maana kabla ya mwanafunzi kujiunga huwa kuna fomu za maelekezo zinazoeleza kila kitu ikiwamo rangi za sare na jinsi zinavyotakiwa kushonwa. Sasa wanapotokea baadhi yao wanabadili mishono huku wazazi wakiwa wamegharimia fedha nyingi kuwanunulia sare, hii ni utovu wa nidhamu na kutojali gharama hizo.



**MECTILDA RUKOIJO (OFISA ELIMU MSINGI, WILAYA YA TEMEKE)**

HAPA kuna vitu vingi vinachangia ikiwa ni pamoja na kulegealegea kidogo kwa walimu kutokagua wanafunzi mara kwa mara au wazazi kutoangalia mavazi ya watoto wao ya kila siku kwa sababu ya shughuli nyingi za kutafuta maisha. Lakini malezi bora ni jambo la muhimu zaidi kuliko kuhangaikia maisha. Kwa hiyo shughuli za kila siku zisiwe kikwazo cha kutokulea watoto katika maadili mema, bali wazazi na walezi watenge muda wa kukaa na watoto wao ili kujua shida zao au tabia zao kuliko kuwaacha wakijiendea tu. Mtindo huu upo kwenye baadhi ya shule zisizofuatilia wanafunzi na kwa wazazi wasiofuatilia mienendo na malezi bora kwa watoto wao, lakini shule makini huwezi kukuta mwanafunzi anayethubutu kufanya upuuzi huo wa kubadili mshono wa sare za shule ili ziwe kama anavyotaka yeye na wala mzazi hawezi kukubaliana naye. Kwa maana nyingine niseme kuwa wakati mwingine wanafunzi wanafanya hivyo baada ya kuona hakuna anayewafuatilia kuanzia nyumbani hadi shuleni. Tabia hii iwe chachu ya kuwaamsha wazazi na shule ambazo hazifuatilii mienendo ya wanafunzi ili kuzinduka na kuchukua hatua haraka badala ya kuona kama jambo la kawaida, kumbe ni hatari kwa baadaye. Kikubwa zaidi ni kuwapo kwa ushirikiano mzuri kati ya wazazi, walimu na wanafunzi wenyewe na taasisi za dini kupitia viongozi wao ili kwa pamoja kuhakikisha watoto wanakua katika maadili mema kwenye jamii yetu.



**BAHATI MWANJA (MWALIMU CHUO CHA UFUNDI TEMEKE)**

JAMBO muhimu ni kujitahidi kuwa na malezi bora, ingawa wazazi wengi wamekuwa na kazi nyingi hadi wanashindwa kukaa na watoto wao. Ningewashauri watenge muda japo mara mbili kwa mwezi kukaa na watoto wao badala ya kuwaacha wakajitawala.Kwa suala hili la kubadili sare za shule na kushona wanavyotaka, wazazi wawashirikishe watoto wao wanapopata fomu zenye maelekezo na kuwaambia jinsi ambavyo sare zinatakiwa kushonwa. Aidha, watoto wenyewe wazingatie, wasifuate mambo ya kuiga ambayo kimsingi hayana faida kwa maendeleo ya shule na hata kwa maisha yao ya baadaye. Lakini kama tatizo likiendelea kuwa kubwa, basi sare zote zishonwe shuleni ili kuondoa kadhia hiyo ambayo chimbuko lake ni utovu wa nidhamu. Walimu nao wawafuatilie wanafunzi kwa karibu ili kuwabaini wenye tabia hiyo na kuwarudisha nyumbani ili wakalete wazazi wao kwa ajili ya kujadili mwenendo huo kwa lengo la kuutafutia ufumbuzi, hasa kwa kuzingatia kwamba shule siyo sehemu ya kwenda kufanyia vitendo vya kihuni bali kusoma tu. Ninajua kwamba malezi ya wazazi yamekuwa ni duni sana ndio maana hayo yote yanatokea. Lakini bado hatujachelewa, hivyo tuchukue hatua mapema kabla hali haijawa mbaya, kama tunataka kujenga taifa bora la baadaye. Wazazi wasiogope kukemea matendo maovu yanayofanywa na watoto wao na ikiwezekana watumie viboko pale inapobidi kwani baadhi ya watoto hawawezi kubadilika bila kuchapwa.



# Wakulima watakiwa kuzingatia ushauri

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wameshauriwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu unaotolewa na maofisa ugani ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ambao utawasaidia kuongeza kipato ndani ya familia zao.

Ushauri huo ulitolewa jana na mtaalamu kutoka Taasisi ya Kilimo Trust inayojihusisha na kutoa ushauri wa kilimo, Robert Mwaluseke, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazojihusisha na kilimo zimekuwa zikitoa elimu kwa wakulima matumizi sahihi ya ardhi, lakini changamoto ni baadhi yao kutokuzingatia ushauri huo na kuendelea kulima kilimo cha mazoea hali inayosababisha kupata hasara.

Mwaluseke alisema kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa wakulima wengi wamekuwa wakipata hasara kwenye mazao yao kutokana na kutofahamu nyakati sahihi za kuandaa mashamba, hivyo maofisa ugani wana kazi ya kuendelea kutoa elimu.

"Kilimo ndio tegemeo la taifa kwa maendeleo ya nchi, hivyo lazima tuongeze nguvu ikiwamo kuwapatia wakulima elimu ya kilimo bora, pembejeo za uhakika lakini pia kuwatafutia masoko ili wanufaike na kilimo chao badala ya kupata hasara kwa sababu ya mazao yao kuharibika au kukosa wateja," alisema Mwaluseke.

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha wakulima wananufaika na Taasisi ya Trust, Mwaluseke alisema mpaka sasa jumla ya wakulima 18,000 wa Mkoa wa Mbeya wamenufaika na elimu ya kilimo cha kisasa kupitia mradi wa Chips na 12,000 kupitia Mradi wa Sikia.

Baadhi ya wakulima mkoani Mbeya akiwamo Paulina Leonard, alisema baadhi yao wanatumia teknolojia za zamani kwenye kilimo hali inayosababisha kupata mavuno duni ukilinganisha na wale wanaotumia teknolojia za kisasa.

Alisema sababu ya kutumia teknolojia duni kwenye kilimo ni ukata wa fedha unaosababishwa na umaskini na kuiomba serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kuwakopesha wakulima teknolojia za kisasa kwa masharti nafuu.

# DIT yatenga mil. 19/- kuboresha majengo

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

**Baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya madarasa, mabweni na nyumba za watumishi tutaimarisha vilevile upanuzi wa mafunzo yetu.**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salam (DIT) tawi la Myunga Halmashauri ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe, imetenga Sh. milioni 19 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ili kuboresha madarasa, mabweni na nyumba za watumishi.

Mkurugenzi wa tawi hilo, Frank Lujaji, alisema hayo wakati wa hafla ya kuhitimisha mafunzo ya udereva wa awali kwa waratibu wa elimu kata 32 wa Wilaya ya Momba.

Alisema waliamua kutenga Sh. milioni 19 ili kukamilisha ujenzi wa miundombinu ambayo itasaidia wanafunzi kusoma kwa utulivu, lakini watumishi kupata makazi maalum ya kuishi.

"Baada ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya madarasa, mabweni na nyumba za watumishi, tutaimarisha vilevile upanuzi wa mafunzo yetu yatakayozingatia ubunifu na vitendo hususani kwenye viwanda ili kuzalisha wanafunzi watakaokidhi ushindani wa soko la ajira," alisema Lujaji.

Alisema DIT itaendelea kusaini mikataba ya ushirikiano wa vyuo na viwanda mbalimbali vya ndani na nje ya nchi na mpaka sasa jumla ya mikataba 28 imetiwa saini miongoni ikiwa ni Chuo cha Ufundi Stadi (Veta).

Hata hivyo, Mratibu wa Veta, Mkoa wa Mbeya, Rajabu Mliku, alisema mkataba waliousaini na taasisi hiyo una lengo la wanafunzi kujifunza udereva wa awali na kubeba abiria pamoja na kozi ndefu za Tehema (Vocational training in Information, Communication and Technology, ICT,).

Mwakilishi wa Mkuu wa Songwe ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo, aliishauri DIT kuongeza kozi nyingine kuanzia ngazi ya Veta na ufundi sanifu ili kupanua wigo wa ajira.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene (katikati), akizungumza katika kikao na watendaji wa mkoa wa Iringa jana, juu ya namna walivyojipanga katika kutunza vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla ikiwa ni sehemu ya ziara yake katika mikoa ya Morogoro na Iringa. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi na Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Prof. Esnat Chaggu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vikundi vya wakulima vyapewa msaada

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

KAMPUNI inayojihusisha na ununuzi wa mpunga wilayani Kyela mkoani wa Mbeya, Kyela Rice Company Limited, imetoa msaada wa pawatila tisa zenye thamani ya Sh. milioni 134 lengo likiwa ni kuwasaidia wakulima kutumia teknolojia za kisasa kwenye kilimo chao.

Msaada huo umetolewa kwa vikundi tisa vyenye wakulima 120, na kampuni hizo zimekuwa zikiwajengea uwezo wakulima namna bora ya kuandaa mashamba.

Akitoa msaada huo mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Moses Mwaipopo, alisema waliamua kutoa msaada huo kwa vikundi hivyo baada ya wakulima hao kuonyesha nia ya kutaka kulima kilimo cha kisasa na chenye tija.

Alivitaka vikundi vilivyopata pawatila hizo kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuongeza uzalishaji wa kilimo cha mpunga kwa kutumia kilimo cha kisasa.

"Nia na madhumuni ya msaada huu ni kuona wakulima wanaachana kulima kilimo cha mazoea na zana hizo za kilimo zitawasaidia kuongeza uzalishaji, lakini nawasisitiza wakulima kuendelea kutunza mavuno badala ya kuuza kiholela na kusababisha baa la njaa," alisema Mwaipopo.

Meneja wa kampuni hiyo, Thobias Mwamkonda, aliwashauri wakulima kuwatumia maofisa ugani waliopo kwenye maeneo yao ili kupata ushauri wa kitaalamu na kuongeza uzalishaji wa mpunga.

Alisema kampuni hiyo imekuwa msaada kwa wakulima wilayani Kyela kwa zana mbalimbali za kilimo, awali walitoa maksai 300 kwa wakulima wadogo wilayani humo.

Kaimu Mkurugenzi wa wilaya hiyo, Polycarp Benedict, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuwasaidia wakulima na kuahidi halmashauri kusimamia kwa karibu zana hizo za kilimo ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Atupakisye Mwambulukutu, aliyenufaika na msaada huo, alisema miongoni mwa changamoto inayowakabili wakulima wa Kyela ni uhaba wa mvua ambao unasababisha mazao mengi kukauka mashambani.





# Naibu Waziri awaonya wanaompinga JPM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya watu wenye Ulemavu, Stella Ikupa, amesema watu wanaobeza na kupinga jitihada kubwa zinazofanywa na Rais John Magufuli, watakuwa wanapingana na Mungu.

Ikupa aliyasema hayo jijini Dodoma wakati akifunga kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Wanawake wa CCM [UWT] kwa mkoa wa Dodoma.

Aliwaambia wajumbe kuwa mambo mengi yaliyokuwa kwenye ilani ya uchaguzi mkuu mwaka 2015, kwa CCM yametekelezwa na kubainisha kuwa mtu ambaye hajaguswa na jitihada za Rais Magufuli atakuwa mwongo.

**Kwa sasa tumebaini na kushughulikia upatikanaji wa viwanja vya uwekezaji na hili tumelifanya kila wilaya nia yetu tujitegemee na tusiwe tegemezi.**

Aidha, Ikupa alitaja nyanja ambazo serikali imezifanyia kazi kikamilifu kuwa ni pamoja na kupambana na dawa za kulevya ambazo zilikuwa zikipoteza vijana na kurudisha nyuma uchumi wa nchi na kujenga pamoja na kuimarisha miundombinu ya umeme. Aidha, imejenga barabara, reli na usafiri wa anga pamoja na uwezeshaji wa mikopo kwa makundi maalum ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Naibu Waziri alichangia mabati 10 yenye thamani ya Sh. 360,000 kwa UWT Dodoma kwa ajili ya mradi wa elimu, huku jumla ya Sh.1,850,000, zikichangwa kwenye harambee ya baraza hilo.

Awali akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dodoma, Neema Majule, alisema tangu wanaingia madarakani waliahidi mambo matatu ikiwamo kuijenga UWT yenye upendo, umoja na mshikamano kupitia mikutano mbalimbali.

"Kwa sasa tumebaini na kushughulikia upatikanaji wa viwanja vya uwekezaji na hili tumelifanya kila wilaya nia yetu tujitegemee na tusiwe tegemezi," alisema Majule.

Kwa upande wake mjumbe wa Baraza Kuu Taifa UWT, Chiku Mugo, alimpongeza Naibu Waziri Ikupa kwa mchango huo huku akiwapongeza wadau wengine kwa kuendelea kuiunga mkono UWT katika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo.



Mkurugenzi wa Shirika la Tanganyika Christian Refugee Service (TCRS) Kituo cha Morogoro, Rehema Samwel (kulia), akizungumza wakati wa warsha ya kutathmini hali halisi ya utafiti wa mazingira ya wafanyabiashara ndogo Mkoa wa Dodoma uliofanywa na Chuo Kikuu Huria Tanzania kwa niaba ya shirika hilo, mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sido yafunza vijana kusindika ngozi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA linalohudumia Viwanda Vidogo nchini (Sido) mkoani Dodoma limewataka wajasiriamali kujitokeza kwa wingi kupata ujuzi wa kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi ili waweze kutoa ushindani katika soko.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Sido mkoani Dodoma, Sempeho Manongi, wakati wa ziara ya kutembelea majengo ya kituo cha uongezaji thamani ya bidhaa za ngozi Kizota jijini Dodoma.

Manongi, alisema hivi sasa kituo hicho kimeboreshwa kwa kiasi kikubwa na kina vifaa vya kutosha kwa ajili ya kumwezesha mjasiriamali kujifunza jinsi ya kuongeza thamani ya bidhaa za ngozi ambazo wanatengeneza.

Kutokana na hilo alisema hakuna sababu ya vijana kubaki nyuma na badala yake waende kupata mafunzo ambayo yatawasaidia kuanzisha biashara ikiwamo kujiajiri wenyewe ili kuwaingizia kipato.

"Naomba wajasiriamali wa Dodoma na mikoa jirani mjitokeze kuja kupata mafunzo katika kituo cha kufundisha uzalishaji wa ngozi tunahitaji kuona mnatengeneza bidhaa zenye ubora," alisema Manongi.

Alieleza kuwa hivi sasa Sido inajiandaa na maonyesho ya Wiki ya Bidhaa za Ngozi hivyo ni vema wajasiriamali wajitokeze katika kituo hiko kupata mafunzo ambayo yatawasaidia kupeleka bidhaa bora katika maonyesho hayo ambayo yatajumuisha wajasiriamali kutoka sehemu mbalimbali.

Alisema lengo lao ni kuona vijana wajasiriamali wanakuwa bora katika uzalishaji wa bidhaa hasa ukizingatia taifa linaelekea katika uchumi wa viwanda, hivyo tunahitaji kuona bidhaa zinazozalishwa zinakuwa na ubora mkubwa.

Mbali na hilo alisema tayari wameboresha majengo ambayo yatatumiwa na wajasiriamali mbalimbali katika kuendesha biashara zao za kila siku hapa jijini Dodoma.

Alisema Sido Dodoma inatoa kipaumbele kwa wajasiriamali wenye malengo ya mbele ambayo yatawasaidia wakulima wa mkoa wa Dodoma katika usindikaji wa mazao ya chakula na biashara.

Alifafanua kuwa majengo hayo yana uwezo wa kuchukua wafanyabiashara nane na kuendelea hivyo kuwataka watu kuchangamkia fursa hizo mapema ambazo zitawawezesha kuendesha biashara zao katika maeneo mbalimbali yanayowazunguka.

Alisema fursa hizo ni muhimu kutokana na kwamba zinalenga kuleta maendeleo kwa wajasiriamali na taifa kwa ujumla.

# Wamachinga watakiwa kufuata sheria

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewataka wafanyabiashara wadogo -wamachinga kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa na Halmashauri ya Jiji ikiwamo kuheshimu maeneo yasiyo rasmi katika kufanya biashara zao.

Dk. Mahenge alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara ofisini kwake waliondolewa eneo la stendi ya Sabasaba, ambapo wametakiwa kuondoka kufuatia mgomo wa madereva wa daladala waliokuwa wameshinikiza wamachinga hao kuondoka kwa madai kuwa wanaweza kusababisha ajali sehemu hiyo.

Akizungumza na wafanyabiashara hao wadogo aliwataka kuzingatia sheria na kanuni zilizopo na zilizowekwa kwa mujibu wa taratatibu za halmashauri ya jiji ambazo zinalinda maslahi yao pamoja na serikali kwa ujumla.

Alisema hakuna sababu ya kukaidi kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi wakati bado kuna nafasi zinazoweza kufanikisha shughuli zao.

"Ninawaagiza wafanyabiashara kuhakikisha mnazingatia sheria na kanuni hizi zitaweza kuwalinda nyinyi wenyewe pamoja na mali zetu hata kama mtajiona mnasumbuliwa," alisema Mahenge.

Katika hatua nyingine akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Ofisa Masoko wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema kuwa wafanyabiashara wote waliondolewa kwenye eneo hilo la stendi ya Sabasaba wameshapangiwa maeneo.

Alisema jumla ya wafanyabiashara 165 walikuwa wakifanya biashara zao kwenye eneo hilo la Sabasaba tayari wameshapangiwa sehemu ya kufanya biashara zao ikiwamo kwenye soko la Bonanza, Majengo na Sabasaba yenyewe.

"Ndugu wanahabari Halmashauri ya Jiji la Dodoma tayari tumeshawahamisha wafanyabiashara 165 wenye meza ili waende wakafanye biashara zao kwenye maeneo hayo badala ya kuendelea kung'ang'ania kwenye eneo hilo ambalo limesongamana kutokana na wingi wa daladala," alisema Yuna.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Soko la Bonanza jijini hapa, Goha Magwai, alisema kuwa tayari wamepokea wafanyabiashara 100 na kuwapatia maeneo kwa kushirikiana na ofisa masoko wa jiji hilo.



# Umri sasa changamoto Mahakama ya Watoto

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAHAKAMA ya Watoto Vuga Mjini Zanzibar imesema baadhi ya watoto wanaokinzana na sheria kupitiliza umri wa miaka 17 ni changamoto kwa mahakama hiyo kwa kuwa huwa wanakataliwa katika kituo cha kurekebisha tabia (TAI).

Akizungumza mbele ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ ya Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti wa Mahakama hiyo, Fatma Muhsin Omar, alisema watoto wanaokinzana na sheria hupelekwa katika kituo cha kurekebisha tabia, lakini baadhi yao hukataliwa kwa sababu wameshavuka umri wa miaka 17.

Pia changamoto nyingine inayoikabili mahakama hiyo ni wafanyakazi kutokuwa na mafunzo ya kutosha ya uendeshaji wa kesi za watoto.

Alisema mahakama hiyo imefungua kesi 167 kwa mwaka uliopita wa Julai 2018 hadi Juni 2019 na kati ya hizo kesi 99 zimemalizika na 68 zinaendelea kusikilizwa.

**Lengo la kuanzishwa kwa mahakama hiyo ni kuharakisha uendeshaji wa kesi na utoaji wa uamuzi kwa kesi zote zinazohusu watoto walio chini ya umri wa miaka 18.**

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mahakama hiyo ni kuharakisha uendeshaji wa kesi na utoaji wa uamuzi kwa kesi zote zinazohusu watoto walio chini ya umri wa miaka 18.

Kamati hiyo imeiomba Wizara ya Katiba na Sheria kuhakikisha kuwa wanazifanyia matengenezo baadhi ya mahakama ambazo majengo yake ni chakavu.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Suleiman Makame Ali, alisema hatua hiyo itasaidia kuhakikisha watendaji pamoja na wanaofika mahakamani kupata huduma bora kwa utulivu.

"Kwa vile ujenzi wa mahakama mpya inayotegemewa kujengwa Tunguu fedha zake zinatoka katika Mfuko wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ni vyema pia mkatenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya mahakama zilizoharibika kwa upande wa Unguja na Pemba," alisema.

Aliiomba jamii iwe tayari kukemea na kuhakikisha kesi za watoto katika masuala ya udhalilishaji hazipati nafasi ndani ya jamii na hata katika familia.

Kwa upande wake Waziri wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalim, akitoa taarifa ya utekelezaji robo ya nne ya wizara hiyo mbele ya kamati hiyo, alisema katika kuimarisha mfumo wa sheria za Zanzibar imeandaa miswaada mitano ya sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi hatimaye kupitishwa.

Alisema misaada yote hiyo imetiwa saini na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein na sheria hizo zimeanza na zinaendelea kutumika.

Alisema ofisi ya mkurugenzi wa mashtaka imepokea jumla ya kesi za 467 za jinai na kufunguliwa katika mahakama mbalimbali za Unguja na Pemba.



Baadhi ya wananchi wakiangalia ndege isiyo na rubani katika maonyesho ya teknolojia yaliyobuniwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. Joseph Tanzania, yaliyofanyika katika viwanja vya Mapinduzi Square, Michezani mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Serikali yaahidi jengo la hospitali kutumika

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, imeahidi kuchukua hatua za haraka kuhakikisha jengo la hospitali ya Shehia ya Mbuzini linaanza kutumika kabla ya mwaka 2020.

Waziri wa wizara hiyo, Haji Omar Kheri, alieleza hayo katika mwendelezo wa ziara zake katika Mkoa wa Mjini Magharibi kwa Wilaya ya Magharibi A kwa kuangalia miradi ya maendeleo na kuona baadhi ya changamoto ziliopo katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo.

Alisema kwa sasa wizara yake itashirikiana na uongozi wa mkoa, wilaya na manispaa ili kutekeleza agizo la serikali la kuifanya hospitali hiyo kuwa ya Wilaya ya Magharibi (A).

"Jengo hili lina maelekezo na maagizo ya mheshimiwa rais na hakuna mtu mwingine wa kubadilisha maagizo hayo kwa sasa, sisi Wizara ya Tawala za Mkoa ndio tuliokuwa na dhamana na dhima ya eneo hili, sasa si vyema ukamaliza mwaka 2020 hapa pakawa hapajaanza shughuli zozote tutafanya kila tuwezalo ili kuona matarajio ya Rais tunayatimiza," alisema Waziri Kheir.

Aliuagiza uongozi wa Wilaya ya Magharibi A na Manispaa ya Wilaya hiyo, kuendelea kulisimamia na kulilinda eneo la jengo la hospitali hiyo ili lisije kuvamiwa kwa ujenzi wa makazi ya wananchi.

"Ninachotaka eneo hili liwe na uangalizi maalum wasije kutokezea baadhi ya wajanja wakataka kukata viwanja na kuuza na nimeshasikia hapa kama kuna baadhi ya eneo limeshakatwa viwanja sita," alisema.

Katika hatua nyengine Waziri Kheir alizitaka kamati za ulinzi ya mkoa na wilaya kushirikiana na uongozi wa Mamlaka ya Vyombo vya Usafiri Baharini (UMCA) kutafuta eneo maalum ambalo litatumika kwa ajili ya kukarabati vyombo hivyo, huku akiagiza mamlaka hiyo kuvihamisha vyombo vilivyopo eneo la Mtoni kwa ajili ya kuimarisha usalama wa eneo hilo.

Akizungumzia kuhusu eneo la kuanika dagaa, Waziri Kheri, alisema kwa sasa eneo lililotengwa na serikali kwa shughuli hizo ni Kihinani na kuutaka uongozi wa wilaya hiyo na manispaa kuwaondoa wafanyabiashara wanaofanya shughuli hizo katika eneo la Bububu kwa kuwa sio rasmi kwa kazi hiyo.

# Wanafunzi wastaafu watakiwa kuhamasisha

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, ameutaka umoja wa wanafunzi wastaafu kushirikiana na kuwahamasisha wengine kusoma ili kuongeza idadi ya ufaulu.

Akizungumza wakati alipofungua umoja wa wanafunzi wastaafu wa Shule ya Sekondari Hamamni Mjini Unguja, alisema ni vyema kukaa vizuri na wanafunzi waliopo shuleni pamoja na wazazi kuwaelimisha umuhimu wa elimu katika maisha yao, kwa kuwa bado kumeonekana baadhi ya wazazi kutojali elimu kwa mtoto wao.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya kila jitihada ili kuhakikisha elimu ya Zanzibar inakua kwa kuwa imeipa kipaumbele zaidi sekta hiyo na afya kutokana na umuhimu wake katika maisha ya mwanadamu.

Aliwashauri kutumia vizuri magrupu yao ya mitandao ya kijamii katika kusambaza masuala ya msingi na yenye faida kwa jamii kwa kuwa zinaenea kwa haraka.

Aliwapongeza wanafunzi hao waliomaliza shule kwa kuamua kujikusanya na kuanzisha umoja wao kwa lengo la kuchangia na kusaidia sekta ya elimu.

Hata hivyo, aliwataka kutoushirikisha umoja wao na masuala ya kisiasa na badala yake wachangie na kupeana taarifa njema kama malengo ya kuundwa umoja huo.

Akisoma risala ya kuanzishwa kwa umoja huo, Mwalimu Khamis Haji, alisema lengo la kuanzishwa kwa umoja huo ni kujenga umoja na mshikamano baina yao baada ya kupoteana katika kipindi cha miaka 20, pamoja na kukuza maendeleo yao ikiwamo kuongeza idadi ya ufaulu wa wanafunzi wao.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Hamamni, Ali Rashid, alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vitabu vya masomo ya sayansi na idadi kubwa ya wanafunzi.

Shule ya Sekondari Hamamni ilianzishwa mwaka 1999 baada ya serikali kuifanyia matengenezo makubwa.

# ZSTC kuanza kuzalisha tani 7,000 majani ya mkaratusi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

SHIRIKA la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) limesema litazalisha tani 7,000 ya majani ya mkaratusi ambayo yatazalisha tani 100 za mafuta kwa mwaka yenye thamani ya Sh. bilioni 3.4.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi chini ya mwenyekiti wake, Mwinyihaji Makame, Mdhamini wa ZSTC, Abdalla Ali Ussi, alisema shirika limeshanunua mbegu za mkaratusi kutoka Australia na hatua za utayarishaji zinaendelea.

Alisema shirika hilo limetafuta mashamba matano yenye ukubwa wa eka 281 kwa ajili ya kilimo hicho katika Wilaya ya Micheweni, ambapo wataanza kuchimbua shamba la Kishindeni la eka 155 na shamba la Mwamoja lililopo Shumba Viamboni la eka 45.

"Lengo letu hasa ni kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mkaratusi hadi tani 2000 kwa mwaka, ambapo asilimia 80 wataiuzia kampuni ya Kunshan Asia Aroma ya China ambayo iliingia makubaliano ya kibiashara Agosti 4 mwaka 2018," alisema mdhamini huyo.

**Lengo letu hasa ni kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mkaratusi hadi tani 2000 kwa mwaka, ambapo asilimia 80 wataiuzia kampuni ya Kunshan Asia Aroma ya China ambayo iliingia makubaliano ya kibiashara Agosti 4 mwaka 2018.**

Alieleza kampuni hiyo ilikubali kukifanyia matengenezo kiwanda cha Makonyo kilichopo Wawi Chakechake Pemba, ikiwamo ufungaji wa boila (boiler) moja jipya pamoja na kufunga vyungu vitano vipya vya kuzalishia mafuta ya mkaratusi.

"Hii ilikuja kufuatia ziara ya mwenyekiti wa kampuni hiyo kutembelea kiwanda hicho na shamba la Mtakata na changamoto zilizoonekana hususan uzalishaji mdogo wa mafuta unaosababishwa na uchakavu wa mitambo ya kiwanda cha Makonyo, uhaba wa vyungu vya kuzalishia mafuta pamoja na eneo dogo la miti ya mkaratusi," alifafanua.

Alisema ufungaji wa boila jipya lenye uwezo wa kuzalisha tani nane za mvuke wa maji kwa saa na vyungu vitano vyenye uwezo wa kuchakata tani 22,500 za majani ya mkaratusi na kuzalisha mafuta tani 320 kwa mwaka yenye thamani ya Sh. bilioni 10.8 inatarajiwa kumalizika hivi karibuni.

"Kwa kweli mradi huu unatarajiwa kutoa ajira nyingi kwa wananchi ambao wataweza kufanya kazi katika mashamba ya mkaratusi kwa kazi ya kilimo na uvunaji na katika kiwanda kipya cha kuzalishia mafuta," alisema.

Wakati huo huo, kamati ilitembelea kitengo cha mizani na vipimo ambapo Mkurugenzi wa Idara ya Biashara na Kitengo hicho, Khamis Ahmada Shauri, alisema jumla ya Sh. 26,345,000, zinatarajiwa kukusanywa katika kitengo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia vianzio vyake mbalimbali vya mapato.

Alisema mwaka jana kitengo kilikadiria kukusanya Sh. 15,000,000, lakini zilikusanywa Sh. 10,622,500.

Alieleza kuwa, katika kutekeleza majukumu ya kazi ya uhakiki wa vipimo, wanakabiliwa na changamoto za uhaba wa wataalamu wa fani za vipimo, kutokuwa na eneo maalumu kwa ajili ya uhakiki wa magari ya mafuta, ukosefu wa usafiri, uhaba wa vitendea kazi ikiwamo kompyuta na samani za ofisi.

Naibu waziri wa Wizara ya Biashara, Hassan Khamis Hafidh, alisema kitengo hicho kimepiga hatua kubwa ya kuwaokoa wananchi kwa kukagua vianzio hivyo, kwani wafanyabiashara wengi ni wababaishaji.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akifanya usafi katika mtaro wa Barabara ya Uhuru, eneo la Kariakoo, jana, ili kuweka mazingira safi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Uelewa umeme jua sasa uko juu'

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya usambazaji wa huduma na vifaa vinavyotumia umeme unaotokana na nishati ya jua (Mobisol), imesema kwa sasa Watanzania wengi wana uelewa mkubwa juu ya matumizi ya umeme huo.

Imesema uelewa huo umewasaidia wananchi wengi wasiofikiwa na umeme wa kawaida, kufanya shughuli zao za maendeleo na kujiongezea kipato.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja Mauzo wa Mobisol Kanda ya Pwani, Wesley Muyenze, alisema kuna haja sasa kuongeza jitihada ya kuelimisha baadhi ya wananchi ambao bado hawajafahamu umuhimu wa nishati hiyo.

Alisema umeme wa jua ni nishati mbadala ambayo kila nyumba inapaswa iwe nayo ili kunapotokea tatizo la umeme isaidie kuendesha shughuli nyingine za maendeleo.

"Hii ni nishati mbadala na muhimu kuwapo majumbani, tunaona nchi nyingi zinaitumia, ni wakati sasa na sisi Watanzania tuanze kuitumia kwa kasi, tusitegemee tu umeme wa kawaida kwa sababu wakati mwingine unapokatika watu husitisha shughuli zao.

"Tuache haya mazoea, sisi kama Mobisol tayari tumeshawahudumia watu 500,000 na tunaendelea kuwaelimisha ili waitumie.

"Tunatambua kuwa kuwahudumia wateja zaidi ya 500,000 si kazi ndogo, lakini lengo letu tunataka kila mtu aendeshe shughuli zake bila kuwa na wasiwasi wa kukatika kwa umeme," alisema.

Muyenze alisema nchi haiwezi kufikia uchumi wa viwanda bila kuwa na umeme wa uhakika katika maeneo mengi ya nchi na kwamba wanaiunga mkono serikali katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda.

# Mkakati wabuniwa kuongeza makusanyo mapato wilayani

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Nachingwea mkoani Lindi imeandaa Wiki ya Elimu ya Mlipakodi kwa ajili ya kuelimisha wakazi wa wilaya hiyo, ili waweze kutambua wajibu wa kulipa kodi na tozo za serikali bila usumbufu.

Mkuu wa wilaya hiyo, Rukia Muwango, aliliambia gazeti hili jana kwa njia ya simu kuwa kampeni hiyo itaanza leo na kuendelea kwa wiki moja ikishirikisha wadau wa maendeleo.

Muwango alisema wazo la kampeni hiyo aliliibua baada ya kubaini kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa mambo ya kodi na tozo za serikali, na hawatambui kwamba wana wajibu wa kufanya hivyo.

"Hawatambui kuwa wana wajibu wa kutoa kodi na tozo mbalimbali, kulingana na mahitaji, matokeo yake wanadai tu haki ya kupata huduma mbalimbali za serikali, kulaumu miundombinu bila kujua kwamba hayo yote yanatokana na kodi ambazo zinalipwa na sisi wenyewe Watanzania," alisema Muwango.

Alisema ameona siyo muda wa kunyoosheana vidole, kulaumiana bali yeye na timu yake wapo kwa ajili ya kuelimisha wananchi, kuwaelekeza kuwafahamisha na ndipo akaibuka na wazo la kutoa elimu hiyo.

"Zoezi hili litakuwa endelevu kadri tutakavyojipanga, katika utoaji wa elimu hii ninashirikiana na TRA kuanzia makao mkuu, mkoa na wilaya, wote tutashiriki katika wiki nzima tutajipanga kwa ajili ya kutoa elimu," alisema.

Aliongeza kuwa elimu hiyo ni muhimu kwa vile hata Mtanzania mwingine anapokosa huduma nzuri za afya kwa sababu watu kutolipa kodi ni sawa na kujirudisha nyuma wenyewe.

"Lakini katika kufanikisha hili kuna wadau ambao wametuunga mkono wakiwamo Mashujaa FM, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na kampuni kama Hyseas na Sunshine," alisema.

HABARI KIMATAIFA

# Wanasheria 96 wamtetea Omar kortini

**KHARTOUM,** Sudan

RAIS wa zamani wa Sudani, Omar Hassan al-Bashir, amekana mashtaka dhidi yake, huku timu yake ya utetezi, inayoundwa na wanasheria 96, ina matumaini kuwa mteja wao ataachiliwa kwa dhamana.

Al-Bashir alifikishwa mahakamani Jumamosi, huku akitabasamu. Hii ni mara ya pili kesi yake ya ufisadi kusikilizwa mahakamani mjini Khartoum. Hata hivyo wanasheria wake wameomba achiliwe kwa dhamana.

**Tunaomba mahakama imuachilie kwa dhamana mtuhumiwa.**

Kesi ya kiongozi huyo iliyowasilishwa na Jeshi la nchi hiyo Aprili 11 baada ya kudumu madarakani miaka 30, ilifunguliwa Agosti 19.

Al-Bashir anakabiliwa na mashtaka ya kumiliki fedha za kigeni, ufisadi na kutumia madaraka vibaya.

Agosti 19, mchunguzi mmoja alidai kwamba Omar al-Bashir alikiri kupokea pesa nyingi kutoka Saudi Arabia kwa pesa taslimu kiasi cha dola milioni 90 (sawa na euro milioni 80).

Mwishoni mwa wiki, Jaji alisikiliza mashahidi watatu, ikiwa ni pamoja na wachunguzi wawili ambao walifanya ukaguzi kwenye makazi yake na kupata pesa nyingi.

Wakati huo huo, upande wa utetezi umeiomba Mahakama imwachie kwa dhamana mteja wao ambaye ni Al Bashir.

"Tunaomba mahakama imuachilie kwa dhamana mtuhumiwa," alisema mmoja wa wanasheria wake Hashem Abu Bakr.

Hata hivyo, Jaji alieleza kuwa atatathmini ombi hilo na kutangaza kwamba kesi itasikilizwa tena Agosti 31.

Baada ya kusikilizwa, Omar Hassan al-Bashir amerejeshwa gerezani. **RFI**



Familia ikiwa nje ya nyumba yao baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha vifo vya watu 62 na nyumba takribani 37,000 kuharibiwa Sudan. **PICHA: AFP**

## Watu 62 wafariki kutokana na mafuriko

**KHARTOUM,** Sudan

SHIRIKA la Habari la Sudani (SUNA) limesema mvua kubwa za msimu zinazoendelea kunyesha Sudan zimesababisha vifo vya watu 62 na kujeruhi 98.

Umoja wa Mataifa (UN) umeeleza kuwa takribani watu 200,000 wamekosa eneo la kuishi, huku nyumba zaidi ya 37,000 ziliharibiwa, ikinukuu idadi kutoka kwa ofisa wa serikali aliyetoa majibu katika matukio ya majanga ya kiasili

Sudan imekumbwa na mvua kubwa za msimu tangu mwanzoni mwa Julai ambapo zimeathiri takribani watu 200,000 katika majimbo yapatayo 15 nchini humo ikiwamo Mji Mkuu Khartoum.

Eneo lililoathiriwa vibaya ni jimbo la West Nile lililopo kusini mwa nchi hiyo.

Hivi karibuni UN ilieleza kuwa watu 54 walikufa kutokana na mvua kubwa.

UN ilisema kwamba wafanyakazi wa kutoa msaada wa dharura wana wasi wasi wa kutokea mafuriko zaidi ikiongeza kuwa msimu wa mvua ulitarajiwa kuendelea hadi Oktoba mwaka huu.

Ofisi ya UN inayohusika kuratibu masuala ya kibinadamu ilisema dola milioni 15 za ziada zilihitajika kutoka kwa wafadhili katika kukabiliana na hali ya dharura iliyojitokeza ikiongezwa kwenye mfuko wa dola bilioni 1.1 zilizotakiwa kwa ajili ya kukabiliana na shughuli nzima za dharura nchini humo.

## Mwanamke kuongoza wizara nyeti

**KINSHASA,** Congo

JAMHURI ya Demokrasia ya Congo (DRC), imepata serikali mpya, ikiwa imepita miezi saba tangu kuapishwa kwa Rais wa taifa hilo, Felix Tshisekedi.

Serikali hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kupambana na rushwa na umasikini.

Katika serikali hiyo mpya, Chama cha Rais wa zamani, Joseph Kabila kimechukuwa wizara muhimu zikiwamo sheria, ulinzi, fedha na akiba.

Serikali hiyo ilitangazwa saa 11 alfajiri jana baada ya kusubiriwa usiku mzima.

Vile vile, Katika serikali hiyo mpya, wanawake wamepewa asilimia kumi na saba ya mawiziri na wanaume asilimia 83. Tangazo la serikali hiyo lilitolewa ikulu moja kwa moja kupitia televisheni ya taifa. Serikali hiyo mpya ina mawaziri 66 pamoja na waziri mkuu.

Rais Tshisekedi alichelewesha kutangazwa kwake kutokana na kwamba alitaka kuwapo na waziri anayewawakilisha walemavu.

Kwenye serikali hiyo, chama cha FCC kinachoongozwa na Joseph Kabila kimepata mawaziri 42, wakiwamo wa Sheria, ulinzi, fedha, madini, akiba na mipango ya serikali, huku chama cha CACH kinachoongozwa na Rais Tshisekedi kikishikilia wizara ya mambo ya ndani, wizara ya mambo ya nje na bajeti.

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Congo, Wizara ya Mambo ya Nje itaongozwa na mwanamke.

Mwanamama huyo, Marie Ntumba Nzenza anatoka chama cha UDPS cha Rais Thisekedi lakini hajulikani na waliowengi nchini humo.

Serikali hiyo itakuwa na manaibu watano wa mkuu akiwamo Elysee Munembwe kutoka FCC ambae ataongoza Wizara ya Mipango ya Serikali, na Jean Baudouin Mayo Katibu Mkuu wa chama cha UNC cha Vital Kamerhe aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu anayehusika na bajeti.

Hata hivyo, serikali hiyo ina idadi ndogo ya wanawake, kwa jumla ni aslimia 17 pekee ya wanawake.

Wananchi wa Kinshasa wamepongeza kuwako na serikali ambayo ina sura mpya na hasa vijana.

Miongoni mwa mawaziri waliokuwa kwenye serikali ya Kabila na waliobahatika kurejea kwenye serikali hii mpya ni pamoja na Azarias Ruberwa Waziri wa Majimbo na Thomas Luahaka Waziri wa Elimu ya vyuo vikuu. Majimbo yote 26 yamewakilishwa kwenye serikali hiyo.

Aliyekuwa gavana wa kivu ya kaskazini, Julien paluku ameteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda. Serikali ya Rais Tshisekedi haikuwashirikisha wapinzani. **DW**

## Namibia, Angola wazozana kisa mamba kuuawa

**WINDHOEK,** Namibia

MAMBA wapatao watano wamekutwa wameuwawa Kaskazini Magharibi mwa mpaka wa Namibia na Angola.

Chanzo cha vifo hivyo hakijafahamika bado ingawa inasadikiwa kuwa waliwekewa sumu.

Ofisa mahusiano wa Wizara ya Mazingira Namibia, Romeo Muyunda, aeleza: "Inawezakana kuwa kuna baadhi ya watu ambao walidhuriwa na mamba hao kwa namna moja au nyingine. Labda mamba hao waliwauwa wanyama wao au wapendwa wao hivyo wakaamua kuwawekea sumu ili wafe". Alisema na kuongeza.

"Lakini pia inawezekana sio sumu pekee kwa sababu baadhi ya mamba wamekutwa wakiwa na majeraha, mfano kuna mamba mmoja aliokutwa amekatwa kichwa na wengine mkia".

Alisema hakuna ushahidi wa moja kwa moja unaoeleza kuwa ni binadamu au wanyama waliotenda kitendo hicho.

Alisema licha ya kwamba kuna baadhi ya watu ambao wanakula mamba lakini sio upande wa Namibia labda Angola.

Mamlaka ya Namibia imeweka sera ambazo zinawalinda mamba na kunufaisha raia wa nchi yake hivyo inawawia vigumu kuamini kuwa ni raia wa Namibia ndio wamefanya vitendo hivyo. **BBC**

## Uandikishaji daftari la mpigakura waahirishwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UANDIKISHAJI wa maboresho ya daftari la kudumu la mpigakura mkoani Shinyanga, umehairishwa baada ya kudaiwa kutokea tatizo la kiufundi na kusogezwa mbele.

Uandikishaji wa daftari hilo ulikuwa uanze mkoani Shinyanga kuanzia juzi na kuhitimishwa Septemba Mosi mwaka huu, kwa kuandikisha watu ambao wameshafikisha umri wa miaka 18 na ambao kadi zao zimeharibika na kupotea.

Akizungumza na Nipashe jana, Msimamizi wa Uchaguzi mkoani Shinyanga, Amos Machilika, ambaye pia ni Katibu Tawala Msaidizi Utumishi na Utawala mkoani humo, alisema maboresho ya daftari hilo yameahirishwa hadi Sepemba 2, mwaka huu.

Agost 15, mwaka huu, Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Balozi Omari Ramadhani Mapuri, akiwa mkoani Shinyanga na wadau wa uchaguzi alitangaza kuanza uandikishaji huo mkoani humo Agosti 26.

Alisema tume imefanya kikao na wadau hao, wakiamini kuwa elimu ya kujitokeza kujiandikisha kwenye maboresho ya daftari hilo kwa wananchi litafanikiwa kwa asilimia 100.

## Ujenzi wa vivuko waanza

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa), imeanza ujenzi wa vivuko vipya viwili vya Bugorola na Ukara, Ukerewe pamoja na Chato-Nkome Geita, vitakavyogharimu zaidi ya Sh. bilioni saba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Mwanza baada ya kuweka jiwe la msingi katika vivuko hivyo, Mtendaji Mkuu wa Temesa, Japhet Masele, alisema vivuko hivyo vinatarajia kukamilika Februari, mwakani.

Alisema kivuko cha Bugorola na Ukara kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 100 na abiria 300 na magari madogo 10 na mizigo, wakati kivuko cha Chato-Nkome kitakuwa na uwezo wa kubeba tani 100, abiria 200, magari madogo 10 na mizigo.








Katibu wa CCM Mkoa wa Mara, Shaibu Ngatiche (katikati), akiendesha harambee ya kuchangia fedha na vifaa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya Shule za Msingi za Nyaminya 'A' na 'B', wakati wa hafla ya kuaga wanafunzi wa shule hizo, wanaojiandaa kufanya mtihani wa darasa la saba, shuleni hapo, katika Kata ya Tegeruka, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaeleza sababu za ndege kukamatwa Sauzi

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema ndege yake aina ya Air Bus A220-300 inayoshikiliwa Afrika Kusini ni kutokana na deni linalodaiwa na raia wa nchi hiyo, Hermanus Steyn dhidi ya Tanzania.

Ndege hiyo inashikiliwa tangu Jumamosi kutokana na kesi iliyofunguliwa na Steyn.

Katika ufafanuzi wake kupitia Shirika la Taifa la Utangazaji (TBC), Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, kesi iliyofunguliwa na Steyn nchini humo haihusiani na suala la ubia kati ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na la Afrika Kusini.

"Kwenye hii kesi kuna mkanganyiko kidogo, wengi wanaihusisha na madeni ya zamani kwenye Shirika la Ndege kati ya Air Tanzania na Shirika la Ndege la Afrika Kusini," alisema.

"Hii ni kesi tofauti kabisa, ni kesi kati ya serikali (Tanzania) na huyu bwana, haihusiani na masuala ya ndege ni kesi iliyoanzia nyuma miaka ya 80, huyu bwana kuna mali zake zilitaifishwa hapa Tanzania.

Alisema mtu huyo alikuwa akiishi Tanzania na kwamba alikuwa na mashamba, mifugo na mali nyingi.

"Sasa kwa sababu ambazo serikali iliziona wakati huo, mali zake zilitaifishwa na serikali na yeye mwenyewe kimsingi aliridhia, lakini hoja ikawa ni fidia, alipwe fidia kiwango gani?"

"Mgogoro huu ukitaka kuuchimbua asili yake, unatoka miaka ya 80, kwa hiyo ni mgogoro wa shilingi ngapi alipwe fidia mtu huyu, wakati fulani walikubaliana na serikali, miaka ya 90 walikubaliana kiwango wakaja wakabishana ikafika miaka 2000, lakini mwishowe ilifika hatua serikali na huyu bwana walikubaliana kiasi gani kitalipwa, ikabaki kiasi kidogo.

"Ukiangalia hii kesi ya Afrika Kusini ni kwamba amekwenda kutekeleza kuiomba mahakama ya Afrika Kusini imsaidie kutekeleza alipwe kiasi kilichobaki ndiyo msingi wa kesi ulivyo hivi sasa."

Kuhusu makubaliano ya serikali na mtu huyo, Dk. Abbas alisema kwenye awamu zote kulikuwa na makubaliano hayo.

"Kiasi kikubwa cha malipo kilifanyika awamu ya nne (utawala wa Rais Jakaya Kikwete) na kubakia kiasi hicho kidogo," alisema.

"Ni mfumo wa kawaida wa sheria, na sheria itafuata mkondo wake kwa sababu ukiisoma ile hukumu inaturuhusu na sisi kuipinga, kwa hiyo nafikiri wanasheria wetu wataichambua na wataona hatua gani za kuchukua.

"Lakini ni mfumo wa sheria na sisi kama serikali tunaufuata, tuna uheshimu lakini tunachowahakikishia Watanzania tutasimamia maslahi ya taifa na ndege yetu itarudi na kuendelea na shughuli zake.

"Hukumu tunayo, ukiisoma kuna mambo makubwa mawili, kesi ya msingi haijasikilizwa, kesi ya msingi kama nilivyosema nitumie sheria za Afrika Kusini kuomba kutekeleza hukumu ya nchi nyingine kwa hiyo hukumu ambayo imeshapatikana huku kwetu, yeye akaomba itekelezwe kule Afrika Kusini ya kile kiasi kilichobaki kama tutakikubali tukilipe au tutapingana nacho haijasikilizwa.

"Isipokuwa ameomba maombi madogo ambayo kuna taratibu mbili, mkasikiliza wote pande mbili au kusikilizwa peke yake. Yeye alichagua asikilizwe na mahakama bila ya sisi kuwapo, kwa hiyo hatua za mwanzo sisi hatukuwa na ufahamu huo, tutaangalia sheria inasemaje, lakini nafahamu kama wakili hukumu iliyotolewa upande mmoja inaweza kubatilishwa," alisema.

"Mawakili wetu wapo kazini hicho ndicho cha kwanza napenda kuwahakikishia Watanzania wanafanya kazi nzito ya kuichambua kesi hii, wataona ni eneo gani sasa tuchukue hatua ili kupambana kimahakama, lakini ipo siku ndege yetu itarudi," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO



## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



215388502

**Agape Krizostom** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4848-0096** kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari African Rainbow .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: DAR/GOG/RB/228239/2019**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;159/2019

Ombi la **LUSIA TIMOTHI HAULE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MATHAYO SLAA LEHARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 30/08/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/08/2019

215389502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**
**SHAURI LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**
**SHAURI NA 76 LA 2019**
**EZBON RWEYEMAMU................................MDAI**
**DHIDI YA**
**1. DR FRANK PAUL MARTIN MPELUMBE**
**2. NAOMI BIRUSHA STEPHEN**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

**KWA: DR. FRANK PAUL MARTIN MPELUMBE**
**NAOMI BIRUSHA STEPHEN**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yenu katika baraza la Ardhi na nyumba mkoa wa Mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 29.08.2019 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.

Kwa hivyo mnatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo ninyi wenyewe, wakili wenu au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAENI- mkijua kwamba kushindwa kufika , baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila ninyi kuwepo.

Imetolewa nami kwa amri na chapa ya baraza leo tarehe 14/08/2019

215390502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MKOA WA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI**
**NO 39 OF 2019**
**GALANI BULILO GALANI..............................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. MASIKU MASHANA MWITA**
**2. STEPHEN BUDEBA NDAKI**
**3. ACCESS BANK LTD**
**4. KIBOKO AUCT. MART.......................................WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

WAJIBU MAOMBI POPOTE PALE MLIPO, KWA KUWA, mleta maombi ameleta madai yake ya kesi ya madai na yameelezwa katika mahakama ya hakimu mkazi mkoa wa Mwanza. Shauri lilipangwa kutajwa tarehe 02.09.2019 saa mbili na nusu asubuhi mbele ya mheshimiwa **NGAMILANGA(INCHARGE OF RESIDEN'S COURT OF MWANZA)**

**HIVYO BASI,** mnatakiwa kufika mahakamani nyinyi wenyewe au mawakili wenu au watu walio ruhusiwa kisheria na kutakiwa kuleta majibu yenu kwa maandishi kuanzia tarehe mliyopata taarifa hii kupitia tangazo hili.

ANGALIA, kama hamtaudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu mahakama itasikiliza shauri hili upande mmoja na kutoa uamuzi upande mmoja

**IMETOLEWA NA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MKOA WA MWANZA**

**TAREHE 23/08/2019**
**HAKIMU**
**MH. NGAMILANGA**

215390602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**

**SHAURI NA. 169 LA 2019**
**WILLIAM CHARLES**
**GENYA...............................................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1. AHMED HUSSEIN ALLY**
**2. MWANZA CITY COUNCIL ................MJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

KWA: AHMED HUSSEIN ALLY

Unafahamishwa kwamba Mleta maombi hapo juu amefungua Shauri/Ombi dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Mkoa wa Mwanza. Ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 23/09/2019 katika Chumba cha Baraza, barabara ya Posta. Jengo liko mkabala na Mahakama Kuu ya Biashara, Tanzania.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza siku hiyo wewe mwenyewe, Wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria kujibu ombi hilo.

KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, Baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na Chapa ya Baraza leo tarehe 20/08/2019.

215390702

---

## CHETI KIMEPOTEA



215389002

**ESTER YOHANA NGHATA** anatangaza kupotelewa na cheti cha **CHUO CHA UUGUZI MIREMBE** kilichotolewa mwaka 1991 -DODOMA.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**taarifa ya polisi:**
**CHAM/RB/717/2019.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;162/2019
Ombi la NDIWELA ALFRED SICHONE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PAUL RICHARD MREMA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/08/2019

215389202

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA ARUSHA-ARUSHA**
**MAOMBI MADOGO NA 209 MWAKA 2018**
**GAUDENSIA PANTALEO............MDAI**
**DHIDI YA**

**SADICK MWACHA**
**ROSE KILAVU..................WADAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

KWA: SADICK MWACHA
ROSE KILAVU.........POPOTE MLIPO

Gaudensia Pantaleo,amefungua shauri hili mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Arusha.Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 7/8/2019 saa tatu kamili asubuhi. Hivyo basi, mnatakiwa kuleta utetezi wenu ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba Arusha. Endapo hamtatekeleza haya, shauri hili litaisikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa dhidi yenu. Ofisi za Baraza zipo katika Jengo la Mkuu wa Wilaya Arusha.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 11 mwezi July mwaka 2019.

215389302

---


Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

NI
JIBU LAKO

Kwa Habari

Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

Tupigie

0767 223 311

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MBAPPE, CAVANI WAIPA PIGO PSG



**PARIS,** Ufaransa

WACHEZAJI Edinson Cavani na Kylian Mbappe waliondoka uwanjani wakiwa majeruhi wakati Paris Saint-Germain ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Toulouse kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu ya Ufaransa juzi, Jumapili.

Eric Maxim Choupo-Moting alifunga mara mbili kipindi cha pili, wakati mabingwa watetezi PSG wakipata ahueni baada ya kutoka kufungwa mabao 2-1 na Rennes wiki iliyopita.

Mchezaji wa kimataifa wa Cameroon, Choupo-Moting, ambaye aliingia kuchukua nafasi ya Cavani, aliipita ngome ya Toulouse defence kuandika bao la kwanza katika dakika ya 50 kabla ya Matthieu Goncalves kujifunga na kuizawadia PSG bao la pili dakika tano baadaye.

Penalti ya Angel Di Maria iliokolewa na Baptiste Reynet kabla ya Choupo-Moting kuongeza bao la tatu dakika ya 75 na Marquinhos akafunga la nne.

Mbappe aliondoka katika dimba hilo la Parc des Princes kwa machela na atafanyiwa uchunguzi zaidi, huku kocha wa PSG, Thomas Tuchel akiiambia Canal+ kwamba wachezaji wote wawili wameumia misuli.

# Guardiola amjaza sifa Silva

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amemwagia sifa kiungo wake wa kati, David Silva, kama mmoja wa wachezaji wake wazuri zaidi aliokutana nao, baada ya kuchangia katika mabao yote matatu katika ushindi wa 3-1 dhidi Bournemouth ugenini juzi Jumapili.

Akicheza mechi yake ya 400 kwa City, Silva alionyesha umahiri wake huku mabingwa hao wakipanda hadi nafasi ya pili katika msimamo wa ligi wakiwa pointi mbili nyuma ya Liverpool.

Son Heung-min, akiichezea Tottenham kwa mara ya kwanza msimu huu baada ya kumaliza kifungo cha mechi tatu, alishindwa kuona lango la wageni hao licha ya kupata fursa za wazi.

Na hayo yakijiri mabao mawili ya Sergio Aguero yaliisaidia Man City kuilaza Bournemouth ugenini.


Mchezaji huyo baadaye alimpatia pasi nzuri mshambuliaji matata wa timu hiyo, Raheem Sterling kwa bao la pili kabla ya Aguero kujaza bao la tatu.

Kocha Guardiola alimwagia sifa tele Silva kwa kuchangia katika mabao yote.

"Alicheza vizuri. Yeye huwa mzuri katika mechi kama hizi ambapo timu zinalinda lango," alisema Guardiola.

"Yeye ni miongoni mwa wachezaji bora zaidi kukutana nao, staili yake ya uchezaji inasaidia zaidi timu na ni mchezaji muhimu kwa kikosi chetu."

Licha ya kuwa na masihara mengi katika safu yao ya ulinzi, City ilitawala mchezo huo kwa asilimia kubwa.





## Pochettino: Spurs haijatulia

**LONDON,** England

MAURUCIO Pochettino amesema timu yake ya Tottenham ipo kwenye matatizo kwa sababu dirisha la usajili bado halijafungwa Ulaya.

Spurs walifungwa bao 1-0 na Newcastle Jumapili licha ya kucheza kwa kumiliki mpira kwa asilimia 80, lakini walishindwa kuipenya ngome ya Newcastle.

Newcastle walipata pointi yao ya kwanza chini ya kocha, Steve Bruce, wakati Joelinton alipofunga bao moja la kipindi cha kwanza na kuipa ushindi wa 1-0.

Huku majaliwa ya Christian Eriksen yakiwa hajajulikana, mchezaji huyo raia wa Denmark akianzia benchi, Pochettino amesema atakuwa mtu mwenye furaha mara tu dirisha la usajili litakapofungwa Septemba 2, mwaka huu.

"Bado dirisha la usajili halijafungwa Ulaya na sisi timu yetu haijatulia, kwani ni kundi ambalo bado lina matatizo.

"Bila shaka, nitakuwa mtu mwenye furaha kubwa ndani ya siku 10 zijazo baada ya kufungwa kwa dirisha la usajili, na tunajua tutakuwa na wachezaji hadi dirisha litakapofunguliwa tena Januari."

HABARI MICHEZO

# Manchester City, QNET zajifunga miaka 10

**MANCHESTER,** England

KLABU ya soka ya Manchester City imeongeza muda wa ushirikiano wake na Kampuni ya mauzo ya moja kwa moja ya Asia (QNET), hatua ambayo itadumisha ushirikiano huo kwa kipindi cha miaka kumi, hivyo kuongeza wigo kwa familia zenye kipato cha chini kuweza kunufaika na mafuzo ya soka na kozi fupi za lugha ya Kiingereza kote duniani.

Ushirikiano huo wa muda mrefu utaifanya Kampuni ya QNET kuendelea kuwa muuzaji rasmi wa moja kwa moja wa timu ya wanawake na wanaume ya Manchester City.

Aidha, ushirikiano huo unaashiria hatua kubwa kwa Mei mwaka jana wakati Manchester City ilipoikaribisha Kampuni ya QNET kama mshirika wa kwanza wa lebo za mikononi (sleeves) katika Ligi ya Wanawake ya Super League.

Na katika kipindi chote kijacho cha ushirikiano huo Kampuni ya QNET itaendelea kutoa kliniki za mpira wa miguu zinazosimamiwa na Manchester City duniani kote, pamoja na kujihusisha na watumiaji na wasambazaji kupitia uhusiano huo na klabu ya City.

Katika kusherehekea tangazo hilo, QNET imezindua toleo dogo la saa za mkononi inayojulikana kama 'QNETCity Champions' zinazoundwa na kuzalishwa na mafundi mashuhuri wa nchini Uswisi.

Makamu Rais Mwandamizi wa Ushirikiano wa City Football Group, Damian Willoughby, alitoa maoni yake na kueleza: "Tunafuraha kutangaza kwamba QNET imekuwa mshirika wa hivi karibuni kuongeza muda wa ushirikiano na Manchester City katika makubaliano ya muda mrefu ambayo yatashuhudia tukisherehekea miaka kumi ya kufanya kazi kwa pamoja.

"Ushirikiano huu uliweka historia pale QNET ilipokuwa mshirika wa kwanza wa lebo za mikononi (sleeve) katika ligi ya wanawake ya Super League na tunafuraha kuingia katika ukurasa mwingine kwa pamoja."



# WAKALA WA DYBALA AFICHUA SIRI MAN UNITED

**TURIN,** Italia

WAKALA wa Paulo Dybala amesema madai yanayosemwa kuhusu kukwama kwa uhamisho wake wa kwenda Manchester United na Tottenham Hotspur ni ya uongo.

Nyota huyo wa Juventus alikuwa akisakwa na wababe hao wa Ligi Kuu England, lakini dili zote zimekwama baada ya kudai kwamba Dybala alikuwa akitaka kulipwa mshahara mkubwa.

Madai ya kwamba Dybala alitaka kulipwa mshahara mkubwa na kamisheni aliyotaka kulipwa wakala wake ndicho kitu kilichovuruga dili la kwenda kwenye Ligi Kuu England kukwama hadi dirisha lililofungwa mapema mwezi huu.

Ripoti zinadai kwamba Dybala alitaka kulipwa mshahara wa kibosi pamoja na kamisheni ya pauni milioni 13.7 ili kukamisha dili kitu ambacho wakala wake, Jorge Antun amedai kwamba hakuna ukweli wowote.

Antun alisema: "Nimezungumza na klabu hizo za England, lakini hizi habari za kamisheni si za kweli. Kulikuwa na mambo mengine kabisa kuhusiana na klabu hizo."

Man United walikuwa kwenye mjadala na wenzao wa Juventus kwa ajili ya kubadilishana wachezaji Dybala na Romelu Lukaku, lakini waliamua kumpiga bei straika huyo wa Kibelgiji kwenda Inter Milan baada ya mazungumzo ya kuhusu Dybala kuvunjika.

Juventus wao wanavyoonekana kwa sasa wanachokitaka ni kumwondoa Dybala kwenye kikosi chao huku PSG wakipewa nafasi ya kunasa saini yake kabla ya dirisha la usajili la majira ya kiangazi huko Ulaya kufungwa.

# Ramos amvuta Neymar Madrid

**MADRID,** Hispania

SERGIO Ramos amesema Neymar ni mwanasoka bora zaidi duniani, huku akishindwa kuficha kama Mbrazili huyo atakwenda kujiunga na Real Madrid katika dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto.

Nahodha huyo wa Los Blancos, amecheza dhidi ya Neymar mara kadhaa, hasa katika kipindi chake alichokuwa kwenye kikosi cha Barcelona na kukutana katika mechi za El Clasico.

Neymar kwa sasa yupo kwenye mazungumzo mazito baina ya klabu yake ya sasa ya PSG, waajiri wake wa zamani Barcelona na Real Madrid wanaochuana kutaka saini yake kabla ya dirisha la usajili halijafungwa Septemba 2, mwaka huu.

Real Madrid wanahitaji sana saini ya staa huyo wakiamini atakwenda kuwa msaada kwenye timu yao ili kuwa bora zaidi, lakini Barcelona wamekuwa na hofu kwamba Neymar akienda kwa wapinzani basi hali yao itakuwa ngumu zaidi.

Alipoulizwa kuhusu Neymar, Ramos alisema: "Neymar ni mchezaji wa kiwango cha juu, mmoja kati ya wachezaji watatu wa kiwango cha juu duniani. Kuzungumzia usajili ni kuikosea heshima timu hii mahiri.

"Mambo kama haya yamekuwa yakizungumzwa hapa Real Madrid na pengine zaidi kipindi usajili unapokuwa wazi. Wachezaji wanapaswa kuwa watulivu katika mambo kama haya."

Neymar aliweka wazi mwishoni mwa msimu uliopita tu kwamba anataka kuachana na PSG na sasa kinachosubiriwa ni kitu gani kitatokea kabla ya dirisha kufungwa. Maofisa wa Barcelona walizungumza na mkurugenzi wa michezo wa PSG, Leonardo wiki moja iliyopita, lakini hakuna makubaliano yaliyofikiwa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN AANZA KUIGA UTUPIAJI WA MESSI BARCA

●●● Ndiyo, nimemuona akifanya hivi kwenye mazoezi na niliiga kwake, ila ni vizuri wakati...

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann amefunga bao lake la kwanza Barcelona tangu alipojiunga na klabu hiyo kwa euro milioni 120 akitokea Atletico Madrid, dhidi ya Real Betis, akifunga mara mbili na kueleza bao la pili ameiga ufundi kutoka kwa Lionel Messi.

**Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa alivumilia kipindi kigumu katika mechi yake ya kwanza wakati wakishitukizwa kwa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Athletic Bilbao wiki iliyopita, lakini akafungua akaunti yake ya mabao kwenye La Liga akiwa na Barca katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Camp Nou.**

Griezmann akiiongoza safu ya ushambuliaji kufuatia kutokuwapo kwa nyota wawili Lionel Messi na Luis Suarez ambao ni majeruhi, alipokea pasi murua kutoka kwa Sergi Roberto ambapo aliunyanyua mpira na kuuchonga mithili ya upinde wa mvua ambao ulimshinda kipa Dani Martin katika dakika ya 41 na kuiandikia Barca bao la kusawazisha baada ya Nabil Fekir kutangulia kuifungia Real Betis dakika ya 15.

Katika ushindi walioupata wa mabao 5-2, Mfaransa huyo alirudi tena kimyani dakika ya 50 huku mabao mengine yakifungwa na Carles Perez, Jordi Alba na Arturo Vidal.

Lakini akizungumzia mabao yake, Griezmann alifunguka kwamba alikuwa akijaribu kumuiga Messi namna anavyozamisha mabao kimyani baada ya bao lake la pili kulizamisha kimyani katika kona ya lango.

Griezmann ambaye pia alitoa pasi ya mwisho katika mechi hiyo iliyohudhuriwa na mashabiki 80,000, licha ya Lorenzo Garcia kuifungia Betis bao la pili katika dakika ya 79 wakati huo wakiwa wameshalala kwa mabao matano, muda haukuwatosha tena kuweza kusawazisha.

Akizungumza na Movistar baada ya mechi, Griezmann alikiri kwamba bao lake la pili dhidi ya Real Betis alijaribu kuiga namna ya ufungaji wa Messi.

"Ndiyo, nimemuona Leo (Messi) akifanya hivi kwenye mazoezi na niliga kwake."

"Sherehe? Nilipenda alichokifanya LeBron (James) na kujaribu kumuiga."

Wakati alipoulizwa kuonyesha nuru kwa Barcelona kufuatia kuwapo kwa majeruhi mwanzoni mwa msimu na kwa namna gani ilivyo vigumu kuweza kuzoea pasipo washambuliaji vinara wa timu hiyo, Griezmann, 28, alisisitiza kuhusu timu kucheza.

"Mwishoni, wakati watu muhimu wakikosekana, timu iliendelea na leo imekuwa kama hivyo."

"Siwezi kulifanya hili pekee; kama ninafunga ama kutoa pasi ya mwisho shukrani kwa wachezaji wenzangu. Sisi ni timu."

"Ni vizuri wakati mnapokabiliwa na majeruhi, watu wanaingia wanaweza kujibu."

Barcelona itacheza dhidi ya Osasuna Jumamosi ijayo wakati nguli wao, Messi anatarajiwa kucheza sehemu ya mchezo huo baada ya kukosa mechi mbili za mwanzo za La Liga kutokana na majeraha ya kigimbi cha mguu.

## ZISIKUPITE

### INTER BADO INAYE SANCHEZ

INTER Milan imefungua mazungumzo tena na Manchester United kuhusu kumnasa mshambuliaji wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 30, na inataka kukamilisha dili hilo kwa mkopo ndani ya saa 72 zijazo kuanzia jana. ***(Mirror)***

### WANYAMA AKARIBIA BRUGES

KIUNGO wa Spurs na Kenya, Victor Wanyama amepewa ofa ya mkataba wa miaka mitano na Club Bruges utakaomuwezesha kupokea pauni milioni 65,000 kwa wiki wakati huu dili hilo likikaribia kukamilika. ***(Scottish Sun)***

### BARCA HIYO TENA KWA NEYMAR

BARCELONA imetoa ofa mpya kwa Paris St-Germain ikitaka huduma ya Neymar, 27, ambayo inajumuisha "fedha zaidi na wachezaji". ***(Telefoot - in French)***

### ERIKSEN AITIA HOFU SPURS

TOTTENHAM inahofu itampoteza kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, kwa kiasi kidogo cha pauni milioni 30 kabla ya dirisha la usajili la Ulaya kufungwa. ***(Star)***

### FIORENTINA KUMFUATA FRED

MIAMBA ya Serie A, Fiorentina inajiandaa kutoa ofa kwa kiungo wa Manchester United na Brazil, Fred, 26. ***(Calciomercato - in Italian)***

### BUTLAND ATEGWA NORWICH

NORWICH itamfuata kipa wa Stoke na England, Jack Butland, 26, dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa endapo dau lake sokoni litashuka. ***(Sun)***

### ELNENY AWINDWA BORDEAUX

BORDEAUX inamtaka kwa mkopo kiungo wa Arsenal na Misri, Mohamed Elneny, akaisaidie kwenye Ligue 1. ***(Foot Mercato - in French)***

### PHILLIPS, LEEDS WAZUNGUMZA

LEEDS imeanza mara moja mazungumzo na kiungo Kalvin Phillips kuhusu kumpa mkataba mpya. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anataka pauni 40,000 kwa wiki ili kubaki hapo Elland Road. ***(Football Insider)***

### AANIKA ALIVYOKATAA VIGOGO

BEKI wa pembeni wa zamani wa Chelsea, Filipe Luis, 34, amekataa ofa kutoka Manchester City, Lyon na Borussia Dortmund majira haya ya joto kabla ya kujiunga na Flamengo ya kwao Brazil. ***(Globo Esporte - in Portuguese)***

### SIMPSON, AMIENS WATETA

BEKI wa zamani wa Leicester, Danny Simpson, yupo katika mazungumzo na klabu ya Ligue 1, Amiens. ***(Sun)***

### LAMPARD AMWALIKA CHRISENE

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amemwalika kiungo wa Exeter, Ben, 15, kujifua na klabu hiyo. Kinda huyo wa England alicheza mechi yake ya kwanza katika kikosi cha kwanza mwezi huu. ***(Sun)***

### BRUCE KUMPA NAFASI ASHES

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce amesema wiki ijayo atazingatia kumchezesha beki mpya wa kati, Muingereza, Ashes. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

# ZFF kuongeza marefa zaidi Fifa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limejipanga kuendelea kuwawezesha waamuzi ili kuhakikisha soka linachezwa kwa misingi inayokubalika na Shirikisho la Soka la Dunia (Fifa), huku lengo likiwa ni kuongeza idadi ya marefa wanaokubalika na shirikisho hilo lenye dhamana ya soka duniani.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho hilo, Ali Mohammed Ameir katika hafla ya kufungua mafunzo ya siku tatu ya waamuzi wa soka yaliyoanza na mtihani wa utimamu wa mwili unaofanyika Uwanja wa Amaan mjini hapa na kushirikisha jumla ya waamuzi 34 ambapo 10 kati ya hao ni wapya na wanawake wakiwa wawili.

Alisema katika kujipanga huko wameona waamuzi ni sehemu moja wapo ya kuhakikisha misingi hiyo inafikiwa kwani ili soka liendelee, waamuzi ni sehemu muhimu.

Ameir alisema waamuzi wamekuwa na kazi kubwa katika kutekeleza wajibu wao tofauti kutokana na kwamba maamuzi yao ambayo wanayafanya, huyafanya hapo hapo tofauti na idara nyingine ambapo mara nyingi maamuzi yake yanaweza kufanywa kwa wakati mwengine.

Alisema ZFF itaendelea kuwawezesha waamuzi ili kupata marefa wengi wanaotambuliwa na Fifa ikilinganishwa na hivi Sasa ambapo idadi yao ni ndogo.

"Uamuzi ni kitu kikubwa na kazi wanayofanya ni ngumu hasa katika kutafsiri sheria na baadaye unatoa maamuzi hapo hapo, kitu ambacho kinahitaji kuwa makini," alisema na kuongeza.

"Lazima ifike wakati waamuzi kubadilika ili kuondosha malalamiko ambayo yalikuwa yakitolewa miaka ya nyuma.

"Mpira umebadilika na taaluma yake imekuwa kubwa zaidi, kwa hivyo kila mwamuzi awajibike na mwamuzi ambae hatofaulu kupitia mitihani watakayopewa hatoruhusiwa kuchezesha," alisema.

Mapema Katibu wa Kamati ya Waamuzi Zanzibar, Muhsin Ali Kamara, alisema mtihani wa utimamu wa mwili umefanikiwa kwa asilimia 99 na sasa kazi iliyobaki ni waamuzi hao kushiriki katika mafunzo ya darasani ili kujiweka sawa zaidi.

Alisema mara baada ya kumaliza mtihani huo wa utimamu wa mwili sasa kutakuwa na mitihani mingine miwili ikiwamo ya vitendo na kutafsiri sheria wakiwa darasani na uwanjani.

# MCHENGA KUIVAA TMK HEROES 16-BORA SPRITE BBALL KINGS

**Na Sabato Kasika**

BINGWA wa mashindano ya Sprite Bball Kings 2018, timu ya Mchenga Bball Stars, ni miongoni mwa timu zilizoingia hatua ya 16-bora baada mechi za mtoano zilizoshirikisha timu 43 juzi jijini Dar es Salaam.

**Na kutokana na droo ya 16-bora iliyochezeshwa jana, Mchenga Bball sasa itakutana na TMK Heroes katika michuano ya kumsaka bingwa mpya wa ikiwa ni mwendelezo wa kumpata bingwa mpya wa Sprite Bball Kings 2019.**

Timu nyingine zilizotinga 16-bora ni Flying Dribblers ambayo itakutana na Oysterbay, wakati Tamaduni ikivaana na Nothing But Nets, Water Institute dhidi ya Styles na JK Ballers dhidi ya Ukonga Hitmen.

Mbali na hizo, timu nyingine ni Weusi, ambayo itakwaana na TMT, KG Dallars dhidi ya Wagalatia na Yo Street itakayopambana na Dream Chasers.

Baada ya kumalizika droo ya kupata timu hizo, Msemaji wa Mashindano hayo, Goza Chuma, alisema mchakamchaka wa kuwania ubingwa huo unatarajia kuanza Jumamosi na kuendelea Jumapili ijayo kwenye viwanja vya Don Bosco, jijini Dar es Salaam.

"Timu nane zitakutana Jumamosi na nyingine nane Jumapili, ila katikati ya wiki zitajulikana zipi zitaanza, lakini kwa sasa hatuwezi kutaja zitakazoanza, kwa sababu bado kuna utaratibu tunaupanga," alisema Chuma.

Michezo ya mtoano ilichezwa Jumapili iliyopita kwenye viwanja vya JK Youth Park, Kidongo Chekundu jijini Dar es Salaam, ikifunguliwa na timu za Ukonga Warriors dhidi ya Mbagala Hard Core na Kigamboni City dhidi ya Ukonga Hitmen.

Mashindano hayo yanaandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite, lengo likiwa ni kuibua vipaji vya mpira wa kikapu nchini.

East Africa Televisheni na East Africa Radio ni vyombo vya habari vinavyoziunganisha nchi za Afrika Mashariki zikiwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 ili kuwahabarisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali.




Mwenyekiti wa Chama cha Waamuzi Dar es Salaam (Bareda), Prosper Mushi (kushoto), akichezesha droo ya kupata timu 16-bora za mashindano ya Sprite Bball Kings 2019, akiwa sambamba na Kamisaa wa Taifa, William Mziray. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Burundi wamhofia Ndayiragije Stars*

**Somoe Ng'itu,** ASMARA

HOFU imeanza kutawala katika kambi ya timu ya Soka ya Taifa ya Burundi ambayo inatarajia kuikaribisha Tanzania (Taifa Stars) katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia inayotarajiwa kuchezwa Septemba 4, mwaka huu mjini Bujumbura, imefahamika.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa juzi, Makamu wa Rais wa Shirikisho la Soka Burundi (FFB), Aimable Habimana, alisema mbali na kikosi cha Taifa Stars kuwa na wachezaji wazuri na wenye uzoefu, ila uwapo wa Kaimu Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, kwao unaweza kuwasumbua.

Habimana alisema Ndayiragije anawafahamu vema wachezaji wa Burundi kwa kuwafundisha na kuujua vizuri mfumo wa uchezaji, ambapo anaamini hali hiyo itaongeza ushindani.

Kiongozi huyo alisema pia Taifa Stars kumalizia nyumbani kwao ni faida sana, lakini hilo haliwakatishi tamaa kwa sababu wanafahamu lolote linaweza kutokea katika mpira ambao utachezwa kwa jumla ya dakika 180 (nyumbani na ugenini).

"Kwa maandalizi kila mmoja anajipanga kuwa na kikosi imara, ila lazima niseme ukweli, Ndayiragije atakuwa msaada mkubwa kwa Tanzania, unajua yeye ni Mrundi na anajua vema falsafa ya Burundi, ni faida kubwa wanayo wapinzani wetu, ila kwa historia, tumekuwa tunaisumbua sana timu yenu (Taifa Stars)," alisema Habimana.

Aliongeza kuwa katika kujiandaa na mchezo huo, kikosi cha Burundi kilitarajia kuingia kambini jana na hadi kufikia Ijumaa, wachezaji wote wanaocheza nje ya Burundi watakuwa wamewasili mjini Bujumbura kwa ajili ya kuungana na wenzao kujiandaa kuikabili Taifa Stars.

Timu hizo zitarudiana Septemba 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na mshindi wa jumla ataingia hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali hizo za Kombe la Dunia zitakazochezwa Qatar mwaka 2022.

Ndayiragije ataikabili Burundi akiwa na kumbukumbu ya kuitoa Harambee Stars ya Kenya kwenye michuano ya Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), katika mchezo ambao kipa wa Taifa Stars, Juma Kaseja, akiibuka shujaa baada ya kupangua penalti mbili.

Kocha huyo Mrundi ambaye aliwahi pia kuzifundisha Mbao FC na KMC FC zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, amerithi mikoba iliyoachwa na Mnigeria Emmanuel Amunike katika kikosi cha Stars.

Michezo
Jumanne Agosti 27, 2019
Nipashe



Wakala wa Dybala afichua siri Utd UKURASA 28



Wanaume wa kazi, Yanga. **PICHA: MAKTABA**

# Zahera aisubirisha Zesco, Aussems ajadiliwa Simba

## Abaini shida ya washambuliaji Yanga, huko Msimbazi nako mashabiki wasema kocha wao...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanikiwa kutinga raundi ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, ametaja 'kituo kinachofuata', lakini akianika tatizo analokwenda kulifanyia kazi katika safu ya ushambuliaji kutokana na kulibaini.

**Jumamosi iliyopita Yanga ikiwa ugenini Botswana ilifanikiwa kusonga mbele kwenye michuano hiyo baada ya kuichapa Township Rollers ya nchini humo bao 1-0, hivyo kuitoa kwa jumla ya mabao 2-1 kufuatia sare ya bao 1-1 katika mechi ya awali Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere juzi usiku, Zahera alisema kwa sasa anaiweka kwanza pembeni timu ya Zesco ya Zambia watakayokutana nayo kwenye raundi ya kwanza ya michuano hiyo na kuelekeza mipango yake kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ruvu Shooting.

"Siwezi kuzungumzia kuhusu mechi dhidi ya Zesco kabla ya iliyopo mbele yangu ya Ligi Kuu Jumatano (kesho) dhidi ya Ruvu Shooting, hivyo tunahitaji kwanza kumaliza mechi hiyo," Zahera alisema.

Kuhusu suala la safu yake ya ushambuliaji kukosa mabao mengi, alisema amebaini kinachowasumbua ni kukosa 'timing' (makadirio) pindi wanaponasa mpira kuanzia wanapokuwa umbali wa yadi 30 kabla ya kulifikia lango.

"Kwa kuwa tutakuwa na muda kabla ya mechi dhidi ya Zesco, tunaweza kulifanyia kazi suala la 'timing' linalowasumbua washambuliaji," alisema Zahera baada ya kuulizwa haoni kuna shida kubwa katika safu hiyo ya ushambuliaji kutokana na mabao yake yote kupata kwa penalti ama faulo.

Katika mechi ya kirafiki ya Wiki ya Mwananchi Yanga ililazimika kutokea nyuma na kusawazisha kwa mkwaju wa penalti wakati ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Kariobangi Sharks, kabla ya kupata matokeo kama hayo ikitokea nyuma tena kwa bao la penalti dhidi ya Township Rollers Uwanja wa Taifa na kisha Botswana ikishinda kwa mpira wa faulo.

Lakini kwa watani zao, Simba ambao walikutana na balaa kwa kutolewa katika michuano hiyo nyumbani, Uwanja wa Taifa kwa faida ya bao la ugenini na UD Songo ya Msumbiji kufuatia sare ya bao 1-1 baada ya mechi ya awali ugenini kutoka suluhu, sasa mashabiki wamejawa na hofu kuhusu hatima ya Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mbelgiji Patrick Aussems.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya mechi hiyo juzi, walisema hata kama hakufikia malengo aliyowekewa katika michuano hiyo hakuna haja ya kumtimua kwani Simba ilicheza soka safi ikimiliki mpira kwa asilimia 65, na kilichowagharimu ni kukosa tu bahati.

"Unajua kocha aliwekewa malengo kufika nusu fainali na ikishindikana robo fainali, lakini safari hiyo imesitishwa leo (juzi), hatuoni sababu ya kutimuliwa, anachotakiwa ni kuijenga timu kwa msimu ujao, kwani kubadili makocha nako kunaigharimu timu," walisikika mashabiki wakijadili baada ya Simba kutolewa kwa faida ya bao la ugenini juzi.

# Wakali wawili wajishindia milioni 825/- za SportPesa

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Jackpot iliyodumu kwa muda mrefu zaidi tangu kuingia kwa michezo ya kubashiri matokeo michezoni nchini Tanzania, imepata washindi baada ya wakali wawili kupatia matokeo ya mechi 13, na kujishindia jumla ya Sh. milioni 825.9 kupitia Kampuni ya SportPesa.

Waliolamba bingo hiyo ni Kingsley Pascal kutoka Biharamuro ambaye ni mtumishi wa umma pamoja na Askari Magabe Marwa wa Serengeti, Mugumu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baada ya kutangazwa washindi, Pascal alisema: "Nimefurahia sana ushindi huu, mpaka sasa hivi siamini. Napenda kuwashauri Watanzania waamini kuwa huu mchezo ni wa kweli na hakuna usanii wowote, wasikate tamaa hata kama wakijaribu bahati yao mara kwa mara, SportPesa ni kampuni ya kuaminika maana malipo yao ni papo hapo pesa inaingia kwenye akaunti yako."

Kwa upande wake Marwa, alisema: "Namshukuru sana mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kushinda, nafahamu wengi wameweka ubashiri, lakini mimi kuibuka mshindi ni jambo la kihistoria. Bado siamini kama mimi ni mshindi mpaka kichwa kinauma, nahisi kadiri siku zinavyoendelea nitazoea hii hali."

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema jumla ya pesa zitakazolipwa kwa washindi hao ni Sh. milioni 997 na pesa hizo zitasaidia pia serikali kwa namna moja ama nyingine kwa kulipa kodi ya zaidi ya Sh. milioni 199.

"Tangu tumeanza kuendesha kampuni hii nchini washindi wamevuna Sh. bilioni 4.4 na kodi ya zaidi milioni 864 za serikali zimelipwa," alifafanua.

Aidha, alisema washindi hao watawasili jijini Dar es Salaam muda wowote kuanzia sasa ili kuweza kukabidhiwa pesa zao na kuwasikia kiundani muda walioshiriki hadi kuibuka kushinda.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002